

**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR**

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

- | | |
|--------------------------------------|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Hamad Masoud Hamad | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole. |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |
| 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa |
| 12.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando |
| 13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa. |
| 14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe |
| 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |

16.Mhe. Abdillan Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasiza Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete

36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinda Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thalathini na Mbili – Tarehe 30 Julai, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2012/2013 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamuomba Mhe. Waziri kuja kusoma hotuba ya makadirio, naomba niwatambulishe wageni wetu, ambao wapo pale juu katika eneo la wageni.

Waheshimiwa Wajumbe, wageni wetu wa leo tarehe 30/07/2012 ni Wageni wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, ambao ni Umoja wa Serikali ya Wanafunzi wa Skuli Binafsi Zanzibar, na wala hawakutajwa wanafunzi wangapi, lakini nawaomba wanafunzi hao wasimame ni wale pale. Vijana nakushukuruni sana na karibuni kushiriki na kuona shughuli zetu. Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kuna jambo ambalo nataka tuliamue, lakini naona idadi ya Wajumbe tuliopo kwa kufanya maamuzi haitoshelezi. Kwa hivyo, tungojee mpaka tupate *quorum* ya kutosha, ili Wajumbe msaidie kuona shughuli zetu zinakwenda namna gani. Kwa hivyo, kwa wakati huu nichukue nafasi kumuomba Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi karibu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ifuatayo ni Hotuba inayohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, likae kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana tukiwa katika hali ya amani na utulivu katika nchi yetu. Kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa hekima na busara.

Pia napenda kuwapongeza Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa busara na hekima yao katika kumsaidia na kumshauri Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hakika ufuatiliaji wao wa karibu wa kazi zinazofanyika na maelekezo yao kwetu, umetuwezesha kupata mafanikio makubwa katika utendaji wa kazi zetu za kila siku za kuwahudumia wadau wote wa sekta za mifugo na uvuvi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Baraza letu la Wawakilishi kwa hekima, busara na juhudi hali inayopelekea Baraza letu kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Pia napenda kuwapongeza wasaidizi wako, wakiwemo Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza hili, Katibu wa Baraza na Maafisa wa Baraza wanaokuwezesha kufanya kazi zako kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kutoa shukrani zangu za dhati na kuipongeza Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezesaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi, kwa kuendelea kutoa ushauri na maelekezo adhimu katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara yangu ili kuweza kufikia maendeleo makubwa. Umahiri na uzoefu wa kiutendaji alionao Mwenyekiti wa Kamati hii, Mhe. Asha Bakari Makame pamoja na wajumbe wa Kamati yake unaisaidia sana Wizara yangu kiutendaji katika kufikia malengo iliyojipangia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Magogoni kwa kuendelea kunipa mashirikiano yao makubwa katika kuleta maendeleo ya jimbo letu katika kipindi cha mwaka mmoja kilichopita. Ni imani yangu kwamba wananchi hao wa jimbo langu wataendelea kunipa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya jimbo langu na ya kitaifa kwa jumla.

Mhe. Spika, Mapinduzi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, kama ilivyoelekezwa katika hotuba muhimu ya Mhe. Rais, ni suala la lazima katika kuongeza uzalishaji na tija kwa wafugaji na wavuvi na hatimae kuinua maisha ya wananchi na kupunguza umasikini. Kazi hii ni mwendelezo wa utekelezaji wa Dira 2020, Ilani ya Uchaguzi na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA II) pamoja na sera mbali mbali zinazoongoza sekta zetu. (*Makofi*)

HALI YA SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI NCHINI

SEKTA YA MIFUGO:

Mafanikio katika Sekta ya Mifugo:

Mhe. Spika, sekta ya mifugo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 imeweza kupata mafanikio kadhaa. Miongoni mwa hayo ni kama yafuatayo:-

- a) Kupatikana kwa Sera ya Mifugo nchini;

- b) Kuzifanyia marekebisha Kanuni ndogo ndogo za kudhibiti ukatili dhidi ya wanyama, ili kupunguza unyanyasaji wa wanyama uliokithiri;
- c) Kuimarika kwa Vituo vya kutoa Huduma za Mifugo kama vile Maabara ya Mifugo Maruhubi, Kituo cha huduma za mifugo Maruhubi, Chinjio la Kisakasaka na Kituo cha Huduma ya Mifugo cha Mangapwani kwa Unguja na kwa upande wa Pemba maabara ya mifugo ya Chake Chake na vituo vya huduma za mifugo vya Konde, Micheweni na Kengeja kwa kupatiwa vifaa na madawa;
- d) Kuimarika kwa utoaji wa huduma za uzalishaji na utabibu wa mifugo;
- e) Kuongezeka kwa uelewa wa kujikinga na maradhi ya mifugo yanayoweza kumwambukiza binadamu (*zoonotic diseases*) na kinga ya mifugo yenyewe;
- f) Kuongezeka kwa huduma za upandishaji ng'ombe kwa sindano;
- g) Kuongezeka kwa usindikaji wa bidhaa za mifugo kama vile samli, siagi, mtindi na kadhalika kutokana na kuongezeka kwa vikundi vya uzalishaji.
- h) Kuongezeka kwa mwamko wa ufugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa.

Mhe. Spika, sekta ya mifugo hivi sasa imeweza kutoa ajira kwa kaya 34,000 na inachangia asilimia 4.2 ya pato la taifa.

Changamoto katika Sekta ya Mifugo:

Mhe. Spika, Sekta ya Mifugo imepiga hatua za maendeleo, lakini bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo:-

- a) Upungufu wa wataalamu mbali mbali wa sekta ya mifugo;
- b) Bei kubwa za madawa na chakula cha mifugo;
- c) Upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi kama vile vyombo vya usafiri kwa watoa huduma za ugani;
- d) Upungufu wa vifaa vya kudhibiti maradhi ya mifugo;
- e) Uvamizi wa maeneo ya wizara unaofanywa na wananchi;
- f) Uhaba wa malisho hasa wakati wa kiangazi na uchache wa maeneo ya malisho.

Mtazamo wa baadae katika sekta ya mifugo:

Mhe. Spika, katika jitihada za kuimarisha sekta ya mifugo nchini, mtazamo wa Wizara ni kama ufuatao: -

- a) Kuongeza taaluma kwa wafanyakazi waliopo na kuajiri wataalamu zaidi ili kuongeza nguvu kwa watendaji waliopo hivi sasa;
- b) Kuandaa mpango maalumu wa kuwasaidia wafugaji wadogo wadogo;
- c) Kuendelea kuimarisha huduma za usafiri kwa watendaji ili kuwafikia wafugaji wengi zaidi;
- d) Kuongeza vifaa vya kudhibiti maradhi ya mifugo;
- e) Kupata hati miliki za maeneo yote ya wizara, ili kuwa na uwezo na nguvu za kisheria za kudhibiti maeneo yake;

- f) Kuendelea kutoa elimu kwa wafugaji kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa za mifugo;
- g) Kufanya utafiti wa malisho yanayostahamili ukame na kutoa elimu ya uhifadhi wa malisho;
- h) Kuanzisha Vituo vya Utafiti na kuendeleza Utafiti wa Mifugo;
- i) Kuendelea kushajiisha uundwaji wa jumuiya za wafugaji zenye nguvu kwa kushirikiana na taasisi nyengine;
- j) Kuendelea kuimarisha maabara, ukarabati wa majosho pamoja na vituo vya mifugo;
- k) Kuanzisha maeneo mapya ya karantini za mifugo;
- l) Kuimarisha mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi;
- m) Kuongeza ajira kwa vijana kupitia shughuli za uzalishaji wa mifugo;
- n) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Mifugo;
- o) Kuendeleza utafiti wa kuku wa kienyeji katika kuongeza uzalishaji kwa kuimarisha vinasaba na utunzaji bora wa kuku; na
- p) Kuendelea kuhamasisha na kupandisha ng'ombe kwa njia ya lindano, ili kuongeza ubora wa ng'ombe wa maziwa

SEKTA YA UVUVI:

Mafanikio katika Sekta ya Uvuvi:

Mhe. Spika, hali ya Sekta ya Uvuvi hivi sasa imezidi kuimarika baada ya wananchi wengi kushajiika na kuanza kufuga mazao ya baharini kwenye maeneo yao. Kiwango cha uvuvi wa samaki kimeongezeka kutoka tani 25,693 mwaka 2010 mpaka tani 28,759 mwaka 2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 5.6. Uzalishaji wa mwani umeongezeka kutoka tani 12,516 mwaka 2010 mpaka tani 13,040 mwaka 2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.

Mchango wa Sekta ya Uvuvi katika pato la taifa umeongezeka kutoka asilimia 6.1 mwaka 2010 hadi 6.7 mwaka 2011.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Sekta ya Uvuvi imepata mafanikio yafuatayo:

- a. Kukamilika kwa majengo ya ofisi kuu ya Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja na Pemba, jengo la Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na majengo ya maeneo ya hifadhi za *MIMCA*, *MENAI* na *PECCA* ambazo zitaimarisha huduma kwa wadau;
- b. Kukamilika kwa ununuzi wa mitambo ya barafu minne (*flake ice machines*) kwa ajili ya kuhifadhia samaki;
- c. Kukamilika kwa ununuzi wa boti tano za doria kwa ajili ya kufanya doria katika bahari kuu;
- d. Kumalizika kwa mchakato wa kuanzisha Kitengo cha Hifadhi (*MCU*) kitakachosimamia bahari ya Mjimkongwe na kisiwa cha Tumbatu kwa kuanzisha sheria ndogo;

- e. Kuweka maboya ya mipaka katika eneo la Ghuba ya Chwaka na maeneo mengine ya hifadhi;
- f. Kuongezeka kwa shughuli za ufugaji wa viumbe vya baharini kama vile samaki, kaa, kasa, majongoo na chaza;
- g. Kusajiliwa kwa Jumuiya ya Wakulima wa Mwani Zanzibar (JUWAMWAZA);
- h. Kuwapatia fursa wajasiriamali 18 na wafanyakazi 12 kutoka Unguja na Pemba ya kushiriki mafunzo juu ya mbinu bora za ufugaji wa mazao ya baharini nchini China;
- i. Kuanzishwa mabwawa mawili ya kufugia samaki katika maeneo ya Kiungoni na Pujini Pemba kama ni mashamba darasa kwa wafugaji wa samaki;
- j. Kukamilika kwa uchambuzi yakinifu wa kuangalia njia bora za kuendeleza shughuli za ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kibiashara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO);
- k. Kukamilika kwa uchambuzi yakinifu wa awali (*pre-feasibility study*) wa ufugaji wa viumbe vya baharini kwa kutumia vizimba (*sea cages*);
- l. Kuongezeka kwa idadi ya samaki kulikotokana na kuimarishwa usimamizi wa maeneo ya hifadhi na elimu kwa wavuvi; na

Mafanikio katika Mradi wa *MACEMP*:

Mhe. Spika, ninapenda kulijulisha Baraza lako kuwa Mradi wa *MACEMP*, ambao ulianza mwaka 2006 hadi 2011 na kuombewa muda wa ziada, sasa unatarajiwa kumalizika rasmi tarehe 31 Agosti 2012.

Mhe. Spika, mradi wa *MACEMP* umepata mafanikio makubwa katika kipindi chote cha miaka saba. Mafanikio hayo yameoneshwa kwenye Kiambatisho namba 1.

Changamoto za Sekta ya Uvuvi:

Mhe. Spika, Sekta ya Uvuvi inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo: -

- a) Kuongezeka kwa shindikizo la uvuvi (*fishing pressure*) katika maeneo ya hifadhi kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wavuvi;
- b) Uharibifu wa makaazi ya samaki unaosababishwa na matumizi ya uvuvi haramu wa nyavu za macho madogo (*illegal fishing*), nyavu za kukokota na mfumo mbaya wa mitego inayobuniwa na wavuvi inayovua samaki wachanga;
- c) Uharibifu wa matumbawe unaotokana na kuganda kwa nyavu chini ya bahari;
- d) Kupauka kwa matumbawe (*coral bleaching*) kunakosababishwa na ongezeko la joto baharini (*global warming*);
- e) Migogoro baina ya wavuvi na wawekezaji wa sekta ya utalii na kati ya wakulima wa mwani na wawekezaji (*hoteliers*);
- f) Migogoro baina ya kijiji na kijiji inayosababishwa na matumizi ya mitego haramu na mitego tofauti kutumika kwa wakati mmoja (nyavu, madema, mishipi n.k.);
- g) Uwezo mdogo wa jamii wa kukeza katika ufugaji wa mazao ya bahirini kutokana na gharama kubwa za uwekezaji (*capital investment*);
- h) Uhaba wa taaluma katika fani ya ufugaji wa mazao ya baharini kwa jamii.

Mtazamo wa Baadae katika Sekta ya Uvuvi:

Mhe. Spika, mtazamo wa baadae katika sekta ya uvuvi ni kama ifuatavyo:-

- a) Kuhamasisha uvuvi wa kina kirefu cha maji (*offshore fishing*) na kufanya tafiti ili kutambua maeneo mapya ya uvuvi “potential fishing grounds” na kuweka matumbawe ya kienyeji (*FADS*) ndani ya maeneo ya hifadhi;
- b) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za bahari;
- c) Kushajihisha wajasiriamali kujiunga katika vikundi vya kuweka na kukopa na kuwapatia nyenzo;
- d) Kuimarisha shughuli za ukulima wa mwani kwa kuimarisha vikundi vya ushirika;
- e) Kusaidia kujenga uhusiano mzuri kati ya wakulima na wafanya biashara ya mwani;
- f) Kuongeza wataalamu wa fani ya ufugaji wa mazao ya baharini; na
- g) Kuongeza uzalishaji wa samaki wa kufuga badala ya kutegemea samaki wanaovuliwa.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2011/2012:

Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeundwa na Idara sita ambazo ni Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; Idara ya Uendeshaji na Utumishi; Idara ya Uzalishaji wa Mifugo; Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo; Idara ya Maendeleo ya Uvuvi; Idara ya Mazao ya Baharini na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/12 Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitekeleza malengo iliyojipangia kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:

Mhe. Spika, idara hii ina majukumu ya kuandaa, kutekeleza na kutathmini mipango, programu, sera na miradi ya maendeleo katika sekta ya mifugo na uvuvi. Vilevile Idara hii, ina wajibu wa kuratibu shughuli zote za wizara na taasisi za ndani, za kikanda na za kimataifa.

Malengo ya Mwaka 2011/2012:

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, ilikuwa na malengo yafuatayo:-

- a) Kukamilisha utayarishaji wa Sera ya Mifugo na kuzifanyia mapitio sheria ndogo ndogo za mifugo na uvuvi;
- b) Kutayarisha Mpango Mkuu wa Kuendeleza Uvuvi (*Fisheries Master Plan*);
- c) Kuanzisha kitengo cha habari, pamoja na kutoa nakla 1,000 za “Jarida la Mvuvi na Mfugaji” na kulisambaza kwa wafugaji na wavuvi;
- d) Kuratibu mashirikiano na taasisi mbali mbali za kitaifa na kimataifa;
- e) Kubuni na kutayarisha miradi mbali mbali ya maendeleo; na
- f) Kuratibu kazi za utafiti wa sekta za mifugo na uvuvi.

3.1 Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ilifanikisha utekelezaji wa mambo yafuatayo:-

- a) Sera ya Mifugo ya Zanzibar imekamilika na sheria ndogo ndogo za mifugo zinazohusu udhibiti na ukatili kwa wanyama zimefanyiwa mapitio;
- b) Mpango Mkuu wa Kuendeleza Uvuvi (*Fisheries Master Plan*) haukufanyika kutokana na ukosefu wa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo (Benki ya Dunia);
- c) Ukusanyaji wa takwimu za mifugo na uvuvi umeimarishwa kwa kuzifuatilia takwimu na kuwapatia mafunzo wakusanyaji wa takwimu 60 walioko kweye vyanzo mbali mbali;
- d) Kitengo cha habari kimeanzishwa na kukipatia vifaa vya kutendea kazi pamoja na kufanikiwa kutoa nakla 500 za “Jarida la Mvuvi na Mfugaji” kwa lengo la kusambaza taaluma zaidi kwa wadau;
- e) Wizara imefanya mazungumzo na mashirika ya Maendeleo ya Korea ‘*KOICA*’, Shirika la Kilimo na Chakula Duniani- *FAO*, Ubalozi wa Watu wa China, kwa ajili ya kusaidia kuimarisha shughuli za ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini. Aidha, mazungumzo yalifanywa kati ya Wizara na Ubalozi wa India na Shirika la *USAID* kwa kusaidia kutoa taaluma kwa wafanyakazi wa sekta ya mifugo;
- f) Miradi na programu zifuatazo zimetayarishwa: Mradi wa Kusaidia Wafugaji wadogo wadogo wa Mifugo, Mradi wa Kudhibiti Maradhi Yasiyokuwa na Mipaka, na Programu ya Kuendeleza Uvuvi (Uvuvi wa maji ya kina kirefu na Ufugaji wa samaki). Aidha Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Ufugaji imeanzishwa.
- g) Kukamilika kwa rasimu ya awali ya uundwaji wa Baraza la Utafiti la Mifugo na Uvuvi. Taratibu za kukamilisha uundwaji wa Baraza hilo zinaendelea. Pia wafanyakazi 25 wa Wizara wamepatiwa mafunzo ya kuandaa mapendekezo ya utafiti.

Malengo ya Mwaka 2012/2013:

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 idara inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Kuendelea kutayarisha mipango kazi, mipango ya utekelezaji na miradi ya maendeleo kwa sekta za mifugo na uvuvi;
- b) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za mifugo na uvuvi;
- c) Kuratibu kazi za utafiti wa mifugo na uvuvi;

- d) Kuzifanyia mapitio Sheria ya Mifugo na Sera ya Uvuvi na Mazao ya Baharini; na
- e) Kuendeleza mashirikiano na taasisi za serikali na zisizo za kiserikali za ndani, kikanda na kimataifa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa jumla ya shilingi 332,585,000/=, kutekeleza kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 221,453,000/= ni kwa mishahara na shilingi 111,132,000/= ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2012 jumla ya shilingi 99,454,000/= zimepatikana kwa matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 89. Kwa upande wa miradi ya maendeleo Idara ilipangiwa shilingi 243,000,000/= kutekeleza Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo na hadi kufikia Aprili 2012 programu ilishapatiwa shilingi 108,253,750/= ambayo ni sawa na asilimia 44.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaombewa jumla ya shilingi 239,001,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 73,327,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 165,674,000/= ni kwa ajili matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara itatekeleza Programu moja ya Kuendeleza Miundombinu ya Ufugaji, ambao unaombewa jumla ya shilingi 200,000,000/= ([Kiambatanisho nam. 2](#)).

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI:

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inaunganisha Idara zote za Wizara

katika kusimamia na kuratibu taasisi za Wizara, kusimamia uendeshaji wa kazi za

kila siku, kuweka kumbukumbu za wafanyakazi, kuhakikisha wafanyakazi wanapata

taaluma, haki na kutimiza wajibu wao, utunzaji wa mali za Serikali zilizo chini ya Wizara na kuhakikisha kuwa sheria, kanuni na taratibu zote zinazohusu matumizi ya mali hizo zinafuatwa.

Mhe. Spika, Wizara yetu hadi kufikia April 2012 ina jumla ya wafanyakazi 739 ambapo 561 wapo katika vituo vya Unguja na 178 wakiwa Pemba. Kijinsia, wafanyakazi 220 ni wanawake na 519 wanaume (Kiambatisho nam 3). Katika mwaka wa fedha 2011-2012 wafanyakazi 7 wamestaafu kazi na mfanyakazi mmoja amefariki dunia (Mungu amlaze mahali pema Peponi, Amin). Wizara bado inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wafanyakazi. Hivyo inahitaji kuingeza idadi ya wataalamu wa kiwango cha juu kwani hivi sasa wizara ina mtaalamu mmoja tu ambaye ana kiwango cha *PhD*, 13 *MSc*, 24 *BSc*, *Diploma* 180 wakati wenye kiwango cha chini cha elimu ni 280 (Kiambatisho nam 4).

Malengo ya Mwaka 2011/2012:

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Uendeshaji na Utumishi

ilijiwekea kutekeleza malengo yafuatayo: -

- a) Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za wafanyakazi wa wizara;
- b) Kuwaendeleza wafanyakazi kielimu katika maeneo ya kazi na kutafuta fursa za masomo kwa wafanyakazi hao kutoka taasisi mbali mbali zinazotoa fursa za masomo ndani na nje;
- c) Kuendelea kusimamia haki na maslahi ya wafanyakazi na kuhakikisha wafanyakazi hao wanatekeleza wajibu wao kwa kufuata Sheria za Utumishi Serikalini;
- d) Kutunza mali za Serikali zinazomilikiwa na Wizara;

- e) Kufuatilia upatikanaji wa Hati Miliki kwa maeneo yote ya Serikali yanayomilikiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi;
- f) Idara itashirikiana na taasisi nyengine katika kuendelea kuwashajiisha wadau wake kubadili tabia, ili wajikinge na maambukizo ya maradhi ya UKIMWI, matumizi ya madawa ya kulevya na kutowanyanyapaa wale waliopata maambukizo. Hii itasaidia kukuza sekta ya uvuvi na ufugaji;
- g) Kuimarisha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi, ili kuweza kutoa huduma kwa ufanisi zaidi kwa wananchi ikiwemo kuwapatia vitendea kazi;
- h) Ujenzi wa joshu la kwanza katika Wilaya ya Mkoani kisiwani Pemba katika Shehia ya Mjimbini; na
- i) Kuendelea na utaratibu wa kuzifanyia ukarabati nyumba za Wizara zilizoko Mkoroshoni kisiwani Pemba na Mkwajuni kisiwani Unguja.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2011/2012:

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo: -

- a) Uwekaji kumbukumbu za wizara umeimarika kwa kuwapatia wafanyakazi wa kitengo cha masjala nafasi za masomo na kuhudhuria warsha mbali mbali kuhusu kazi zao;
- b) Wafanyakazi 16 wameendelezwa kielimu kwa kulipiwa masomo yao;
- c) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, idara imefuatilia utekelezaji wa ulipwaji wa mishahara mipya ya wafanyakazi iliyoanza kutolewa Oktoba, 2011 na kila mfanyakazi kulipwa kulingana na stahiki yake;
- d) Mali za Serikali zilizomo ndani ya Wizara zimetunzwa ikiwa ni pamoja na kuvifanyia matengenezo vyombo vya usafiri na zana nyengine;
- e) Maeno yote yaliyo chini ya Wizara yameshapimwa na taratibu za kuyapatia hati miliki zinaendelea;
- f) Kwa kushirikiana na Tume ya UKIMWI na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Wanawake, Vijana na Watoto, Idara iliendesha semina kwa wafanyakazi 50 Unguja na 23 Pemba na kutoa elimu juu ya athari ya maradhi ya UKIMWI na elimu ya jinsia. Pia mfanyakazi mmoja (mkufunzi) alipatiwa mafunzo ya elimu ya ulemavu;
- g) Idara imewapatia wafanyakazi zana na vitendea kazi pamoja na vyombo vya usafiri ikiwemo kompyuta 3, vespa 1, pikipiki 2, baskeli 2, sare kwa walinzi 6;
- h) Taratibu zote za kupata kiwanja kwa ujenzi wa joshu katika shehia ya Mjimbini Wilaya ya Mkoani zimekamilika na tuko katika hatua za kukiomba hati miliki.
- i) Ukarabati wa nyumba ya Mkwajuni kisiwani Unguja umekamilika. Aidha Idara inatafuta utaratibu wa kukamilisha ukarabati wa nyumba ya Mkoroshoni kisiwani Pemba uwezo wa kifedha utakaporuhusu.

Malengo ya Mwaka 2012/2013:

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo: -

- a) Kuwaongezea uwezo wa kitaalamu wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu;
- b) Kutoa mafunzo ya Sheria mpya ya kazi (Utumishi wa Umma) ya mwaka 2011 kwa wafanyakazi;
- c) Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi;
- d) Kushajiisha uzalishaji katika vikundi vya jamii;
- e) Kuongeza taaluma juu ya mambo mtambuka ikiwemo elimu ya UKIMWI, jinsia, ulemavu, utawala bora, mazingira na matumizi ya madawa ya kulevya;
- f) Kuimarisha ushirikiano na taasisi nyenginezo za kitaifa, kikanda na kimataifa;

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, idara ilipangiwa kupata shilingi 397,463,685/= kutekeleza shughuli za kawaida. Kati ya hizo shilingi 292,842,685/= ni kwa mishahara na shilingi 104,621,000/= kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2012, jumla ya shilingi 97,463,814/= zilikuwa zimepatikana kwa matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 93.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Uendeshaji na Utumishi inaombewa jumla ya shilingi 585,412,000/= kutoka Serikalini ili kutekeleza kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 244,800,000/= ni kwa matumizi mengineyo na shilingi 340,612,000/= ni kwa mishahara.

IDARA YA UZALISHAJI MIFUGO:

Mhe. Spika, Idara ya Uzalishaji wa Mifugo ina jukumu la kupanga, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mikakati na programu za maendeleo ya mifugo. Aidha, Idara hii hutoa taaluma ya ufugaji bora wa mifugo na usarifu wa mazao yake, ili kuleta tija kwa wafugaji na wananchi kwa ujumla. Pia Idara ina jukumu la kuimarisha uzalishaji wa mifugo ya asili kwa kubadilisha vinasaba.

Malengo ya Mwaka 2011/2012:

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ilikusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Kushajiisha vijana kujiajiri katika kazi za ufugaji wa kibiashara.
- b) Kuendelea kuimarisha kituo cha Upandishaji ng'ombe kwa sindano Maruhubi kwa kukarabati jengo la afisi na kulizungushia uzio eneo hilo la kituo, na kutayarisha ardhi kwa kupanda majani kwa ajili ya malisho ya ng'ombe wa mbegu;
- c) Kuendeleza kazi za upandishaji ng'ombe kwa sindano ambapo ng'ombe 6,000 wanatarajiwa kupandishwa;
- d) Kufundisha taaluma ya kupandisha mbuzi kwa sindano kwa wapandishaji (CAHW's) Unguja na Pemba na kuendeleza utafiti wa mbuzi bora. Katika hili la utafiti, naomba kutoa taarifa kwamba mwekezaji Sheikh Ali Yousouf amekubaliana na Idara ya Uzalishaji Mifugo, kufanya utafiti wa pamoja juu ya kabila ya mbuzi bora kutoka Cyprus ambao wana uwezo wa kuzaa ndama watatu kwa mpigo na kutoa maziwa lita sita hadi inane kwa siku.
- e) Kuimarisha ufugaji wa kuku wa kienyeji wanaofugwa na wananchi wengi walio masikini kwa kuwahasisha juu ya utumiaji wa majogoo bora, ili kuongeza

uzalishaji wa mayai na ukuaji wa kuku wanaozaliwa pamoja na kushajiisha matumizi ya chanjo ya mahepe;

- f) Kuanzisha kampeni ya unywaji wa maziwa na ulaji wa mayai katika jamii yetu;
- g) Kuanzisha utafiti shirikishi wa kuku katika kupata kuku wanaokuwa haraka, wanaotaga zaidi na wanaostahamili maradhi;
- h) Kuimarisha mfumo wa elimu kwa wafugaji kwa kutumia mashamba darasa, radio na TV, vijarida na vipeperushi, pamoja na kuongeza idadi ya na uwezo wa kitaaluma kwa wataalamu wa fani hiyo. Jumla ya wafugaji 15,000 watapatiwa elimu kwa kupitia njia hizo;
- i) Kushajiisha ufugaji wa kuku wa kisasa kwa mashirikiano baina ya wawekezaji na wafugaji, ili kuongeza uzalishaji wa ndani wa mayai na nyama. Naomba nitoe habari njema kwamba kampuni ya Sheikh Ali Yousouf na wizara yangu zimo katika hatua za kutayarisha hati ya makubaliano ya uanzishaji uwekezaji mkubwa wa kuku wa mayai hapa Zanzibar. Ni imani yangu kwa Sheikh Ali Yousouf tunavyomfahamu hasa sisi wajumbe wa Baraza lako tukufu, uwekezaji wake utaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya mifugo hapa Zanzibar.
- j) Kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Idara itashajiisha uundaji wa jumuiya za ufugaji na kuzipatia mafunzo ya fani ya mifugo na uendeshaji.
- k) Kuzidisha mwamko wa usindikaji na matumizi ya mazao ya mifugo (nyama, jibini, maziwa, siagi na samli) pamoja na kushajiisha wafugaji kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kisasa vya kusindika mazao ya mifugo sambamba na kutoa mafunzo ya usindikaji na masoko.
- l) Kuendeleza ushajiishaji wa matumizi ya gesi itokanayo na samadi na kufunga mitambo 5 mipya kwa wafugaji watakojitokeza; na
- m) Kukimarisha kituo cha mbegu za majani Kizimbani, kuendelea na mazungumzo na wawekezaji kwa kuyaendeleza mashamba ya Kipange, Kitumba, Hanyegwa mchana, Chamanangwe, Magome na mengineo.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2011/2012:

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 idara imeweza kutekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Mikutano saba (7) ya kuwashajiisha vijana kujiajiri kupitia sekta ya mifugo ilifanyika. Mikutano hiyo iliwajumuisha vijana 300 katika wilaya zote za Unguja na Pemba;
- b) Kazi za uwekaji msingi wa uzio wa ukuta katika kituo cha Upandishaji Ng'ombe kwa sindano imeanza, Madume bora mawili ya mbegu yamenunuliwa. Pia, kituo kimepatiwa vifaa vya kupandishia kutoka Programu ya *ASSP/ASDP-L*;
- c) Ng'ombe 2,867 wamepandishwa kwa njia ya sindano Unguja na Pemba. Aidha hatukuweza kufikia lengo la kupandisha ng'ombe 6,000 kutokana na umeme unaotumika kutengeneza "*liquid nitrogen*" kushuka (*voltage interference*) na kusababisha upungufu wa mbegu katika vituo vidogo vidogo vya Wilayani.
- d) Kutokana na sababu za kifedha, taaluma ya upandishaji mbuzi kwa sindano pamoja na utafiti wa kuendeleza mbuzi bora haikufanyika, licha ya mahusiano yetu tunayoendelea nayo na Sheikh Ali Yousouf;

- e) Majogoo bora 511 yamesambazwa kwa wafugaji Unguja na Pemba ili kuongeza uzalishaji wa kuku wa kienyeji kwa njia ya vinasaba;
- f) Kampeni ya unywaji wa maziwa ilifanyika tarehe 21 hadi 27 Mei 2012 kwa kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kunywa maziwa kwa kutumia vyombo vya habari na matangazo mengine kama mabango na vipeperushi. Pia kulifanyika maonyesho ya wazalishaji wa maziwa na bidhaa zake pamoja na kugawa maziwa kwa wanajamii;
- g) Utafiti shirikishi wa kuku unaendelea na hadi sasa aina 3 za kuku chotara zimeshapatikana nazo ni mchanganyiko wa Kishingo na *Australop*, *Rhode Island Red* na *White Legon*. Mchanganyiko huu wa damu umezingatia zaidi sifa za uzalishaji na ulezi;
- h) Jumla ya wafugaji 6,499 wametembelewa na kupatiwa ushauri wa kitaalamu. Aidha, kwa kushirikiana na programu ya *ASSP*, mashamba darasa ya mifugo 107 mapya yameanzishwa, hivyo kufikia jumla ya mashamba darasa ya mifugo 219 hadi Disemba, 2011 yakiwemo ya wafugaji ng'ombe wa maziwa, mbuzi na kuku. Aidha, jumla ya vipindi 8 vya radio na 6 vya TV vimerushwa pamoja na jumla ya vipeperushi 1,525 vimegaiwa kwa wafugaji. Halikadhalika jumla ya maafisa ugani 15 wamepatiwa mafunzo msasa juu ya mbinu bora za elimu kwa wafugaji;
- i) Katika kushajiisha ufugaji wa kuku wa kisasa, Wizara imefanya mazungumzo na wawekezaji mbali mbali ikiwa pamoja na hatua za awali za kumpatia ardhi mwekezaji Sheikh Ali Yousouf ambapo Wizara yangu imetoa ridhaa kwa Wizara ya Ardhi Makaazi, Maji na Nishati ya kukodishwa eneo la eka 25 mwekezaji huyu Hanyegwa Mchana;
- j) Juhudi za kushajiisha uundwaji wa jumuiya na vikundi vinavyojishughulisha na ufugaji umefanyika, kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi, Kiuchumi na Ushirika pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto ambapo katika hatua ya mwanzo jumla ya mikutano 13 ilifanyika Unguja na Pemba kushajiisha uundwaji wa jumuiya na vikundi vya ufugaji.
- k) Jumla ya wafugaji 48 na wafanyabiashara 18 wameshapatiwa mafunzo ya vitendo ya usindikaji wa samli, siagi, jibini na mtindi pamoja na mbinu za uzalishaji na uhifadhi wa maziwa;
- l) Jumla ya mitambo 5 ya *biogesi* (ya kidenish) imejengwa kwa wafugaji waliohitajia huduma hiyo na mengine 3 (ya kichina) iko katika ujenzi kwa kutumia teknolojia ya mahandaki. Aidha, vijana 4 wamepatiwa mafunzo ya ujenzi wa mitambo ya biogesi ya aina mpya ya mahandaki ambayo yana unafuu wa gharama ukilinganisha na aina nyengine; na
- m) Kituo cha mbegu za majani Kizimbani kimeanza kuwekewa uzio na kituo cha mifugo Magome na skuli ya wafugaji Ole kimefanyiwa ukarabati. Shamba la Kipange linae mwekezaji Mifugo-Care, na sehemu ya Shamba la Hanyegwamchana mwekezaji Al-Yousif *Charitable Organization*. Mashamba ya Pageni, Kitumba na Chamanangwe yatatumika kwa utafiti wa mifugo badala ya kuwapa wawekezaji.

Malengo ya Mwaka 2012/2013:

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Uzalishaji Mifugo inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Kuimarisha huduma za elimu kwa wafugaji kwa kuzingatia mahitaji ya jamii ya wafugaji;
- b) Kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao yake kwa kushirikiana na wafugaji na kufanya utafiti wa mifugo;
- c) Kuimarisha utoaji wa huduma za kupandisha ng'ombe kwa sindano;
- d) Kutoa nafasi za ajira kwa vijana kupitia shughuli za ufugaji;
- e) Kuimarisha mazingira ya utendaji wa kazi;
- f) Kuimarisha mashamba na vituo vya mifugo; na
- g) Kushajiisha utumiaji wa nishati mbadala (*biogesi*), ili kutunza mazingira.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, idara hii mapato yake yaliripotiwa na Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo. Kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 Idara hii inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 15,000,000/= (Unguja shilingi 9,000,000/= na Pemba shilingi 6,000,000/= yatakayotokana na ushuru wa huduma za uzalishaji wa mifugo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, idara ilipangiwa kupata shilingi 448,702,189/=. Kati ya hizo shilingi 359,504,189/= ni kwa matumizi ya mishahara na shilingi 89,198,000/= kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2012 jumla ya shilingi 60,012,000/= zimepatikana ambazo ni sawa na asilimia 67. Jumla ya shilingi 141,500,000/= zimepangwa kutumika kwa Mradi wa Kupandisha Ng'ombe kwa Sindano na hadi April mwaka 2012 mradi ulishapatiwa shilingi 141,500,000/= ambazo ni sawa na asilimia 100.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara inaombewa jumla ya shilingi 571,500,000/= kutoka serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 119,000,000/= zimetengwa kwa matumizi mengineyo na shilingi 452,500,000/= kwa ajili ya mishahara.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara itatekeleza Mradi mmoja wa Upandishaji Ng'ombe kwa Sindano ambao unaombewa shilingi 122,000,000/= ([Kiambatanisho nam 5](#)).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika itatekeleza mradi mmoja wa kuendeleza wafugaji wadogo wadogo katika programu ya pamoja ya Ajira kwa Vijana (*Youth Employment Programme*) ambapo itazalisha nafasi 240 za ajira kwa vijana (ajira 160 kupitia ufugaji wa kuku na ajira 80 kupitia ufugaji wa mbuzi wa maziwa na wa kienyeji). Mradi huu utapatiwa shilingi 150,000,000/= kutoka katika Programu ya Ajira kwa Vijana inayosimamiwa na Wizara ya Kazi, Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

IDARA YA HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO:

Mhe. Spika, Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo ina jukumu la kutoa huduma za kinga na tiba za maradhi ya mifugo. Aidha, kuhakikisha mifugo yetu haienezi maradhi kwa binadamu kwa kufanya ukaguzi wa wanyama. Vilevile, idara hii ina jukumu la kushajihisha jamii kuepuka

ukatili dhidi ya wanyama na kufanya uchunguzi wa mwenendo wa maradhi ya kuambukiza na yenye kuathiri mifugo yetu.

Malengo ya Mwaka 2011/2012:

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara iliwekewa malengo yafuatayo:-

- a) Kuendelea kutoa huduma za tiba, kinga na uchunguzi wa maradhi ya mifugo kwa nia ya kuboresha afya za mifugo yetu nchini;
- b) Kuendelea kuimarisha karantini na ukaguzi wa mifugo na mazao yake kwa lengo la kuikinga mifugo na binadamu dhidi ya maradhi yanayoweza kuletwa na mifugo au bidhaa zake kutoka nje ya nchi;
- c) Kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, kuziendeleza maabara za uchunguzi wa maradhi kwa kuzipatia zana na nyenzo nyengine za kufanyia uchunguzi wa maradhi;
- d) Kufanya ukarabati wa kliniki ya mifugo ya Dunga na ujenzi wa kliniki ya mifugo Unguja Ukuu;
- e) Ununuzi wa vifaa na vitendea kazi vya kliniki 5 za mifugo zilizofanyiwa ukarabati;
- f) Kuendelea na uimarishaji wa mazingira ya kituo cha karantini Kisakasaka;
- g) Kununua jumla ya dozi milioni moja za chanjo ya mahepe na kuchanja kuku wa kienyeji Unguja na Pemba;
- h) Kuendelea na utaratibu wa kupata hatimiliki ya eneo la Karantini Nziwengi Pemba pamoja na vituo vyengine vya mifugo, pia kuendelea kukamilisha hatua za uanzishaji wa eneo la Karantini huko Mkoa wa Kaskazini Unguja;
- i) Kutoa taaluma kwa wafugaji juu ya kuwakinga wanyama wao na maradhi ya kuambukiza kupitia vyombo vya habari, vijarida, vipeperushi pamoja na semina;
- j) Kuendelea kutoa taaluma kwa jamii juu ya kuepukana na tabia ya ukatili wa wanyama, na kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali kama ZALWEDA na ZAASO ya Mama Ana iliopo Kianga (na sio Dunga) ya kupiga vita ukatili wa wanyama; na
- k) Kutayarisha mpango wa tahadhari ya mapema juu ya magonjwa ya miripuko katika sekta ya mifugo kwa kushirikiana na FAO kupitia Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ilitekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Jumla ya wanyama 357,094 wametibiwa kutokana na maradhi ya mifugo, kati yao ng'ombe 16,157, mbuzi 9,971, kuku na jamii ya ndege 327,402, punda 1,239, mbwa 1,319 na paka 1,006. Wanyama waliofungwa uzazi ni Mbwa 431 na paka 721 kwa lengo la kupunguza wanyama wazururaji.
- b) Jumla ya wanyama 130,440 walikaguliwa na kuruhusiwa kuingia nchini. Kati ya hao, ng'ombe ni 5,366, mbuzi 669, kuku (vifaranga vya mayai na nyama) 124,305 na wanyama wengine 100. Aidha, bidhaa za mifugo zilizolingizwa nchini ni pamoja na mayai ya mbegu 19,000.
- c) Maabara ya Maruhubi kwa Unguja na Chakechake Pemba zimefanyiwa ukarabati na kupatiwa vifaa na madawa ya kufanyia kazi kama vile majokofu, darubini, madawa ya kufanyia uchunguzi (*reagents and chemicals*) n.k.

- d) Kuhusu ukarabati wa kliniki ya mifugo ya Dunga na ujenzi wa kiliniki mpya ya mifugo ya Unguja Ukuu, vifaa vya ujenzi tayari vimeshanunuliwa na ukarabati utaendelea ndani ya mwaka huu wa fedha baada ya kupitishwa bajeti yetu.
- e) Ununuzi wa vifaa na vitendea kazi vya kliniki za Maruhubi na Mangapwani kwa Unguja pamoja na Konde na Kengeja kwa Pemba umefanyika.
- f) Uimarishaji wa kituo cha Karantini ya Kisakasaka umeendelezwa kwa kufanya kazi ya usafishaji wa jumla ya ekari 60 kati ya 100 na vile vile uboreshaji wa jengo la Ofisi umefanyika ikiwa ni pamoja na kuanzisha utanuzi wa jengo hilo. Aidha ukarabati wa chinjio umefanyika.
- g) Kwa kushirikiana na Programu za ASSP/ASDP-L, Idara imechanja kuku wa kienyeji 428,035 dhidi ya ugonjwa wa mahepe/magwa. Kati ya hao 146,707 ni kutoka Unguja na 281,328 kutoka Pemba. Aidha jumla ya kuku wa kisasa 246,190 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa mahepe, kuku 39,689 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa gumboro na 4,514 dhidi ya ugonjwa wa ndui. Pia zoezi la majaribio la uchanjaji wa ugonjwa wa vibuma (ECF) ulifanywa kwa Wilaya mbili za Unguja na mbili za Pemba. Jumla ya ndama 320 wa Unguja na Pemba wameshapatiwa chanjo na tathmini ya ugonjwa huo inaendelea.
- h) Uanzishwaji wa eneo jipya la karantini ya mifugo kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja (Donge Muwanda) umeanza kwa mashirikiano ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" na juhudi za upatikanaji wa hati miliki kwa maeneo ya Nziwengi Pemba na Donge Muwanda Unguja zimeshaanza kwa kuyapima maeneo hayo.
- i) Idara ilitoa elimu, ushauri na maelekezo juu ya matunzo mazuri ya wanyama. Vile vile Idara inashirikiana na Jumuiya zisizo za Kiserikali kutoa ushauri wa kitaalamu wa kinga na tiba kwa wafugaji. Jumla ya vipeperushi 5,000 vilitayarishwa na kusambazwa kwa wafugaji, na vile vile vipindi vya taaluma ya kukinga maradhi ya mifugo vimeendelea kutolewa kwa kupitia vyombo vya habari.
- j) Idara inashirikiana na taasisi zisizo za kiserikali zikiwemo ZALWEDA na ZAASO katika kutoa huduma na taaluma dhidi ya ukatili wa wanyama kwa kuwatembelea wafugaji katika vituo vyao na kuwapa ushauri juu ya matunzo bora ya mifugo yao na kutoa zawadi kwa wanaotunza vizuri punda wao na
- k) Mpango wa tahadhari umeshatayarishwa, na wataalamu wa mifugo 100 kutoka Unguja na Pemba wamehudhuria mafunzo juu ya tahadhari ya kujilinda na maradhi mbali mbali ya kuambukiza na yasiyo na mipaka (*Transboundary Animal Diseases*) na tahadhari ya mapema ya magonjwa ya mifugo (*Early Warning System*) kwa kushirikiana na FAO.

Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo: -

- a) Kuendeleza udhibiti wa maradhi ya mifugo kwa kuimarisha vituo vya karantini, maabara na vituo vya mifugo;
- b) Kutoa taaluma kwa wafugaji juu ya kuwakinga wanyama na maradhi ya kuambukiza na kuzuia ukatili wa wanyama;

- c) Kuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi kwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi;

- d) Kuimarisha mazingira ya kazi; na

- e) Kuendeleza utaratibu wa ufuatiliaji, takwimu na tathmini ya maradhi ya mifugo. Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mapato yatokanayo na huduma ya utabibu wa mifugo yalikadiriwa kuwa shilingi 48,000,000. Hadi kufikia mwezi wa Aprili jumla ya shilingi 43,004,500 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 89.6 ya lengo. Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Idara hii inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 59,000,000 yatakayotokana na ushuru wa huduma za utabibu wa mifugo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara ilipangiwa kupata shilingi 446,819,710. Kati ya hizo shilingi 386,608,710 ni mishahara na shilingi 60,211,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa April, 2012 jumla ya shilingi 52,500,000 zimepatikana kwa matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 87.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ilitekeleza miradi miwili ya maendeleo; Mradi wa Kudhibiti Mafua ya Ndege ulioombewa shilingi 55,000,000 na Mradi wa Kudhibiti maradhi ya Kichaa cha Mbwa uliombewa shilingi 95,000,000. Mpaka kufikia mwezi wa Aprili 2012, miradi hii imepata asilimia 100 ya fedha zilizoombwa.

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka 2012/2013 Idara ya Utabibu wa Mifugo inaombewa jumla ya shilingi 628,630,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 508,630,000 ni mishahara na 120,000,000 kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara itaendelea kutekeleza Miradi miwili. Mradi wa Kudhibiti Mafua ya Ndege ambao umeombewa shilingi 80,000,000 (Kiambatisho nam 6) na Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa ambao pia umeombewa shilingi 80,000,000 (Kiambatisho nam 7).

IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI

Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ina majukumu ya kuendeleza uvuvi, kuhifadhi mazingira ya bahari na rasilimali zake na kuzingatia matumizi bora na endelevu ya rasilimali hizo kwa kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni zake kwa nia ya kuinua uchumi wa jamii na Taifa kwa ujumla.

Malengo ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Uvuvi ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Kufanya ukaguzi wa maeneo ya uvuvi kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu kwa kushirikiana na kamati za wavuvi za jamii;
- b) Kuendesha mafunzo kwa wanajamii juu ya umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira ya bahari na rasilimali zake. Jumla ya vijiji 60 na wavuvi 1,200 watafaidika na mafunzo hayo;
- c) Kuendesha mafunzo kwa wanajamii juu ya uelewa na kuwashirikisha katika uhifadhi wa wanyama wa baharini walio hatarini kutoweka kama pomboo, nyangumi na kasa;
- d) Kuainisha maeneo madogo maalum yenye umuhimu kwa uhifadhi wa rasilimali za bahari katika ngazi ya jamii;
- e) Kuendesha mafunzo kwa wadau mbalimbali wa utalii kwa lengo la kuhifadhi rasilimali za bahari na mazingira yake;
- f) Kununua vifaa kwa ajili ya ofisi zilizokamilika za “MENAP”, “MIMCA” NA “PECCA”, na pia kukamilisha ujenzi wa ofisi za Idara Unguja na Pemba pamoja na kununua vifaa vya ofisi hizo;
- g) Kusimamia ujenzi wa soko la kisasa Tumble; na
- h) Kuanzisha mafunzo kwa wavuvi wazalendo kuvua kwenye maji ya kina kirefu, na kutafuta boti za kisasa kwa ajili ya mafunzo hayo. Katika kufanikisha mafunzo haya ambayo ni muhimu katika kuanzisha “fleet” ya wavuvi wazalendo, Wizara yangu imepanga kufanya

mazungumzo na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuona namna ya kuanzisha mtaala wa uvuvi wa bahari kuu katika vyuo vyetu vya amali viliopo Mkokotoni na Vitongoji.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara ilitekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Doria 189 za ukaguzi wa maeneo ya hifadhi zimefanyika kwa kushirikiana na kamati za wavuvi kwa lengo la kuimarisha matumizi bora na endelevu kwa wavuvi na wavuvi 19 walikamatwa kwa uvuvi haramu na kufikishwa katika vyombo vya sheria. Doria tatu za anga zilifanyika katika bahari kuu;
- b) Jumla ya wavuvi 2,056 kupitia kamati tendaji za vijiji 88 katika maeneo yote ya hifadhi za baharini wamepatiwa mafunzo juu ya umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira na rasilimali zake;
- c) Mafunzo yalitolewa kwa wanavijiji 160 katika hifadhi za “MIMCA” na “MENAP” juu ya uelewa na ushiriki wa wanajamii katika suala la uhifadhi wa wanyama wa baharini walio hatarini kutoweka. Katika kupata taaria hizo, Idara imetoa fomu maalum ambazo zinazojazwa na wavuvi kwa kila wanyama hao wataponasa kwenye nyavu;
- d) Maeneo madogo madogo maalum yenye umuhimu wa hifadhi wa rasilimali katika bahari za Chwaka, Marumbi na Jambiani yaliainishwa kwa kushirikiana na wanajamii;
- e) Mafunzo kuhusu uhifadhi wa rasilimali za mazingira ya baharini yametolewa kwa watembezi wageni (watalii) kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii na Kamati tendaji za maeneo ya hifadhi;
- f) Ujenzi wa ofisi za Idara Unguja na Pemba umekamilika na vifaa kwa ajili ya ofisi za “MENAP”, “MIMCA” na “PECCA” tayari vimenunuliwa na kufungwa katika ofisi husika;
- g) Ujenzi wa soko la Tumbe unaendelea na umefikia hatua za mwisho za uezekaji;
- h) Kutokana na kukosekana kwa fedha katika mwaka uliopita, mafunzo kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu (*offshore fishing*) hayakuweza kufanyika. Hata hivyo, Wizara imepanga kufanya mafunzo hayo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 kwa mashirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za baharini;
- b) Kuimarisha shughuli za uvuvi wa kienyeji na bahari kuu;
- c) Kuimarisha shughuli za utafiti na uwekaji wa matumbawe ya kienyeji;
- d) Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi;
- e) Kuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi kwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi; na

- f) Kuendeleza utaratibu wa ufuatiliaji, takwimu na tathmini ya samaki na wanyama wanaohofiwa kutoweka.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara itasimamia utekelezaji wa miradi miwili ifuatayo:-

- i. Mradi wa Uhifadhi wa Mazingira ya Baharini na Ukanda wa Pwani (MACEMP) (Kiambatisho nam 8).
- ii. Mradi wa Uvuvi wa Bahari Kuu (Kina Kirefu cha Maji “*offshore fishing*”) (Kiambatisho nam 9).

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ilikadiriwa kukusanya mapato ya leseni za uvuvi wa kienyeji jumla ya shilingi 20,000,000. Hadi kufikia mwezi wa Aprili jumla ya shilingi 22,556,800 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 112.7 ya lengo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Idara hii inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 30,000,000 yatakayotokana na mauzo ya leseni za uvuvi wa kienyeji.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 jumla ya shilingi 333,297,545 zilipangwa kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 273,009,545 ni kwa mishahara na shilingi 60,288,000 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili shilingi 46,440,400 zimepatikana kwa matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 77.

Mhe. Spika, jumla ya shilingi 8,892,445,000 zilipangwa kutekeleza shughuli za mradi wa MACEMP. Kati ya hizo shilingi 216,000,000 zilipangwa kutoka Serikalini na shilingi 8,676,445,000 ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2012 shilingi 216,000,000 zilipatikana kutoka serikalini ambayo ni sawa na asilimia 100 na jumla ya shilingi 5,169,712,782 zilipatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 60. Baada ya uhaulishaji kukubaliwa na Benki ya Dunia, bakaa ya Dola za Kimarekani 200,000 (sawa na Tshs 296,400,000), zitatumika kumalizia matumizi yaliyokwishapitishwa katika bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka 2012/2013 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi inaombewa jumla ya shilingi 387,498,000 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo shilingi 297,026,000 kwa mishahara na shilingi 90,472,000 ni kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, jumla ya shilingi 400,000,000 zimeombwa kutoka serikalini ili kutekeleza kazi za maendeleo. Kati ya hizo shilingi 300,000,000 ni kwa ajili ya Mradi wa Kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu (Kina Kirefu cha Maji) na shilingi 100,000,000 ni kwa mradi wa MACEMP.

Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha Idara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika itatekeleza mradi mmoja wa kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu (kina kirefu cha maji) katika programu ya pamoja ya Ajira kwa Vijana (*Youth Employment Programme*) ambapo itazalisha nafasi 60 za ajira kwa vijana kwa kuwapatia boti mbili za uvuvi wa kina kirefu cha maji. Mradi huu utapatiwa shilingi 400,000,000 kutoka katika Programu ya Ajira kwa Vijana.

IDARA YA MAZAO YA BAHARINI

Mhe. Spika, Idara ya Mazao ya Baharini ina majukumu ya kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini, ukulima wa mwani, kuwaendeleza wafanyabiashara wa mazao ya baharini na udhibiti wa viwango vya mazao yao kwa ajili ya kuinua hali zao kiuchumi na kuongeza pato la taifa.

Malengo ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ilikuwa na malengo yafuatayo:-

- a) Kuhamasisha matumizi ya mwani ikiwemo kutengeneza sabuni na usarifu mwengine kwenye matumizi ya vyakula mbali mbali;
- b) Kutoa elimu kwa wakulima juu ya ukulima bora wa mwani utakaopelekea kuzalisha mwani bora na wa kiwango cha juu, na pia kutoa taaluma juu ya ujuzi wa ufugaji wa mazao ya baharini ndani na nje ya nchi;
- c) Kuhamasisha wakulima wa mazao ya baharini kuunda vikundi vya ushirika vya kuweka na kukopa ili kuwa na mitaji ambayo itawawezesha kuanzisha vyanzo vya ziada vya kujiongezea kipato na kuwainua kiuchumi;
- d) Kuhamasisha wanajamii kujihusisha na ufugaji wa samaki, chaza, uzalishaji wa lulu na kaa pamoja na kuimarisha usarifu na uuzaji wa mazao hayo katika masoko ya ndani na nje ya nchi; na
- e) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Sayansi ya Baharini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuendeleza utafiti wa mwani mnene ambao unastahamili hali ya hewa na wenye tija zaidi. Pia kufanya utafiti wa mazao ya kamba na majongoo bahari.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ilitekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Mafunzo ya uimarishaji wa ubora wa mwani (*Quality maintaining*), uhamasishaji wa mwani kwa ajili ya soko la ndani ikiwemo utengenezaji wa sabuni, vyakula (keki, vileja n.k.), utayarishaji wa juisi ya matunda na kiushio cha mwani yamefanyika Unguja na Pemba. Jumla ya wakulima wa mwani 118 walipatiwa mafunzo hayo;
- b) Elimu ya ukulima bora wa mwani na ukaushaji wa zao la mwani kwa wakulima wa vijiji 56 (26 Unguja na 30 Pemba) imetolewa. Wajasiriamali 38 wa mazao ya baharini wamepatiwa mafunzo juu ya njia bora ya ufugaji wa samaki, kaa na chaza. Jumla ya wazalishaji wa mazao ya baharini 30 wakiwemo wajasiriamali 18 na wataalamu 12 walipelekwa China kwa mafunzo ya ufugaji wa samaki, kamba na chaza. Pia, Idara imeanzisha ujenzi wa mabwawa mawili yatakayotumika kama ni shamba darasa kwa ajili ya ufugaji wa samaki;
- c) Kwa hatua za awali mafunzo ya uhamasishaji yamefanyika na yalihudhuriwa na washiriki 150 (40 Unguja na 110 Pemba) ili na wao waweze kujiunga na vikundi vya kuweka na kukopa (SACCOS), na kujiwezesha kupata mitaji ya kujiongezea kipato;
- d) Wanajamii 140 kutoka Unguja na 333 kutoka Pemba walihamasishwa na kupatiwa mafunzo ya njia bora za ufugaji wa samaki, kaa na chaza ambapo jumla ya vikundi 113 vimeundwa (72 Pemba na 41 Unguja).

- e) Utafiti wa mwani mnene “*cottonii*” ulifanyika kwa kushirikiana na Kampuni ya mwani ya BIRR, Taasisi ya Sayansi ya Baharini ya Chuo kikuu cha Dar es Salaam pamoja na wanajamii katika vijiji vya Fundo na Tumbe Kisiwani Pemba. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa upo uwezekano wa kulima mwani huo kwenye maji mengi kwa kutumia njia ya chanja za kueleza “raft”.

Pia, kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Taasisi ya Utafiti wa Baharini (*Institute of Marine Research*) ya Norway, Idara ilifanya tafiti za awali (*feasibility study*) za kuangalia maeneo ya mwambao yanayofaa kwa ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini. Ripoti ya tafiti hizo zimekamiliwa na maeneo yanayofaa kwa shughuli hizo yametambuliwa. Aidha, Idara kwa kushirikiana na “*Korea International Cooperation Agency*” (KOICA) inaendelea na utafiti wa ufugaji wa viumbe vya baharini (*feasibility study*) kwa kutumia vizimba (*sea cages*) kwa Unguja na Pemba.

Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara ya Mazao ya Baharini imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- a) Kuimarisha ukulima bora wa mwani na ufugaji wa mazao ya baharini.
- b) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya baharini.
- c) Kuhamasisha usarifu na matumizi ya mazao ya baharini na ukuzaji wa soko la ndani na nje.
- d) Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.
- e) Kuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi kwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi.
- f) Kuendeleza utaratibu wa ufuatiliaji takwimu na tathmini ya uzalishaji wa mazao ya baharini.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara itasimamia utekelezaji wa mradi mmoja ambao ni:-

Mradi wa Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini (Kiambatisho nam 10).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, mapato yatokanayo na ushuru wa usafirishaji wa mazao ya baharini nje ya Zanzibar yalikadiriwa kuwa shilingi 40,000,000. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2012, jumla ya shilingi 69,152,850 zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 173% ya lengo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Idara hii inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 70,000,000 yatakatokana na ushuru wa mazao ya baharini.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Mazao ya Baharini iliombewa jumla ya shilingi 143,838,784 kwa ajili ya kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 97,746,784 ni kwa mishahara na shilingi 46,092,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2012 jumla ya shilingi 46,000,000 zimepatikana ambazo ni sawa na asilimia 99.8.

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka 2012/2013 Idara ya Mazao ya Baharini inaombewa jumla ya shilingi 206,653,000 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo shilingi 112,405,000 ni kwa mishahara na shilingi 94,248,000 ni za kutekeleza matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara inaombewa jumla ya shilingi 78,000,000 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kushajiisha Ufugaji wa Viumbe vya Baharini.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kazi zote za Wizara kwa upande wa Pemba kwa kushirikiana na Idara zake zilizomo katika Wizara hii. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kazi zilizotekelezwa ni miongoni mwa kazi zilizokwisha elezwa chini ya Idara zote zilizomo katika Wizara.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi Kuu Pemba ililenga kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 12,000,000. Hadi kufikia mwezi wa Aprili jumla ya shilingi 22,504,750 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 188 ya lengo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Ofisi Kuu Pemba inakadiriwa kukusanya jumla ya mapato ya shilingi 45,000,000. Mapato haya yatatokana na Huduma za Utabibu wa Mifugo shilingi 12,000,000, Huduma za Uzalishaji wa Mifugo shilingi 6,000,000, Leseni za Uvuvi shilingi 6,000,000 na ushuru wa usafirishaji wa Mazao ya Baharini shilingi 21,000,000.

Mhe. Spika, kwa kutekeleza malengo yaliyoelezwa katika Idara mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi Kuu imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 910,306,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 520,500,000 kwa mishahara na shilingi 389,806,000 ni kwa matumizi mengineyo. Kwa matumizi mengineyo, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imekadiriwa kutumia shilingi 54,646,000, Idara ya Uendeshaji na Utumishi shilingi 61,200,000, Idara ya Mazao ya Baharini shilingi 77,112,000, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi shilingi 68,648,000, Idara ya Uzalishaji wa Mifugo shilingi 64,600,000 na Idara ya Utabibu wa Mifugo shilingi 63,600,000.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2011/2012

Ukusanyaji wa Mapato 2011/2012

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilijipangia kukusanya mapato ya shilingi 1,020,000,000. Kati ya mapato hayo, shilingi 120,000,000 zitatokana na mapato ya ndani ya Wizara (ikiwemo ada za leseni za uvuvi wa ndani, utibabu wa wanyama na ada ya mazao ya baharini), na shilingi 900,000,000 zitatokana na mapato ya leseni za uvuvi wa bahari kuu. Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2012 Wizara ilikusanya mapato ya ndani ya shilingi 157,218,900 ambayo ni sawa na asilimia 131 ya lengo lililowekwa na shilingi 133,770,234, sawa na asilimia 15 zilikusanywa kutokana na uvuvi wa bahari kuu (Kiambatisho nam 11).

Matumizi ya Fedha 2011/2012

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 12,411,153,120 ambapo shilingi 2,871,708,120 zilikuwa ni kwa kazi za kawaida na shilingi 9,539,445,000 ni kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za kawaida shilingi 800,000,000 zilitengwa kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2012, fedha zilizopatikana ni

shilingi 683,243,214 kwa matumizi mengineyo ambayo ni sawa na asilimia 85. Aidha, jumla ya shilingi 750,500,000 ziliombwa Serikalini kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2012 shilingi 615,753,750 zilipatikana kwa matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 82. Aidha jumla ya shilingi 8,788,945,000 ziliombwa kutoka kwa washirika wa maendeleo kutekeleza miradi miwili ya maendeleo (MACEMP) na Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa). Kati ya hizo, shilingi 5,233,525,770 zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia 60.

MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inakadiria kukusanya jumla ya shilingi 2,290,000,000 kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Sambamba na makusanyo hayo, Wizara yangu inatarajia kutumia jumla ya shilingi 1,763,160,000 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 803,160,000 ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa kutekeleza miradi miwili ya maendeleo (Mradi wa Kichaa cha Mbwa, na Mradi wa Kushajiisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini) na shilingi 960,000,000 ni kutoka SMZ. Pia, jumla ya shilingi 3,529,000,000 zimetengwa kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi 2,305,000,000 ni kwa mishahara na shilingi 1,224,000,000 ni za matumizi mengineyo.

HITIMISHO

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuzishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Watu wa Korea, Serikali ya India, Serikali ya Israel, Serikali ya Norway, Serikali ya Japan, Serikali ya Misri, Serikali ya Uholanzi, Serikali ya Marekani, Serikali ya Uingereza na Ufalme wa Oman kwa kushirikiana nasi katika kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi. Aidha, napenda kuyashukuru mashirika ya maendeleo yakiwemo “GEF”, “KOICA”, “SADC”, “UNICEF”, “USAID”, “WHO”, “WSPA”, Benki ya Dunia, Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika “AU”, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa “FAO”, Shirika la Maendeleo la Japan “JICA”, Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo “IFAD”, Jumuiya ya Afrika Mashariki, “EAC”, na Umoja wa nchi za Ulaya “EU” kwa kusaidia maendeleo ya sekta za uvuvi na mifugo.

Vile vile napenda kuzishukuru taasisi binafsi hapa nchini, Wizara za SMZ, taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali kama Taasisi ya Sayansi ya Baharini, *Indian Ocean Marine Affairs Society*, *Tanzania Domestic Biogas Programme (TDBP)*, *ZAASO*, *ZALWEDA* na *ZSPA* ambazo pia zimesaidia katika kuleta maendeleo katika sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati na kuwapongeza Katibu Mkuu wa Wizara Dk. Kassim Gharib Juma, Naibu Katibu Mkuu Dk. Omar Ali Amir, Afisa Mdhamini Pemba Nd. Mayasa Ali Hamad, Wakurugenzi, wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi walioko Unguja na Pemba kwa utendaji mzuri na kufanyakazi kwa juhudi, ushirikiano, ubunifu na ustahamilivu mkubwa.

Vile vile napenda kuwapongeza, wafugaji, wavuvi, wakulima na wafanyabiashara wa mwani, na wadau wengine wa sekta ya mifugo na uvuvi kwa jitihada na mashirikiano yao wanayotoa katika kuendeleza sekta hizi pamoja na changamoto zinazowakabili. Napenda kuwahakikishia kwamba mchango wao tunauthamini sana na tutaendelea kuyafanyia kazi mapungufu yanayojitokeza kulingana na vipaumbele na nyenzo zilizopo.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Wavuvi, Vikosi vya SMZ na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyotoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu. Vile vile tunawashukuru wananchi wote kwa kuitikia wito wa kutumia mazao ya mifugo

na uvuvi katika milo yao na tunawashajiisha wale bidhaa za ndani ili kuwainua wazalishaji wetu kimapato na kuimarisha afya zao. Hivyo basi, kwa niaba ya Wizara yangu napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwaomba wananchi kuongeza juhudi katika uzalishaji na matumizi ya bidhaa hizo ili kuchangia katika suala zima la kufikia uhakika wa chakula hapa nchini kwetu.

Mhe. Spika, naomba kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa wajumbe wote wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Habari na Uwezesaji kwa miongozo yake mizuri iliyotupa katika kufanikisha malengo yetu tuliyojiwekea katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi kwa manufaa ya nchi yetu. Miongozo tuliyoipata katika Kamati hiyo imeweza kutatua changamoto nyingi zinazokabili maendeleo ya sekta hizi. Tunakushukuruni sana.

Mhe. Spika, mwisho nawaomba Waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee, wajadili, watoe maoni, ushauri, mapendekezo na hatimae waikubali na waipitishie bajeti ya Wizara yangu kwa lengo la kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi kwa manufaa ya wafugaji, wavuvi, wakulima wa mwani na wananchi kwa jumla.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 5,292,160,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013. Kati ya fedha hizo shilingi 3,529,000,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 1,763,160,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kunisikiliza kwa umakini sana na naomba kutoa hoja. Wabillahi Tawfiq.

KIAMBATISHO NAM. 1: MRADI WA MACEMP

MALENGO YA MRADI WA MACEMP

Mradi wa Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (*The Marine and Coastal Environment Management Project – MACEMP*), ulianzishwa ukiwa na malengo makuu yafuatayo:

1. Kuhifadhi mazingira ya bahari na ukanda wa pwani.
2. Usimamizi bora wa ukanda wa uchumi wa Bahari Kuu.
3. Kujenga uwezo wa wanajamii katika matumizi bora ya maliasili kwa lengo la kupunguza uharibifu wa mazingira na maliasili na hatimae kupunguza umasikini.
4. Kuimarisha huduma za miundo mbinu na kuimarisha uwezo wa taasisi na jamii.

MAFANIKO YALIYOPATIKANA

1: USIMAMIZI WA UKANDA WA UCHUMI WA BAHARI KUU (EEZ)

- a. Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu
- b. Kuimarika kwa Doria za Bahari Kuu
- c. Ujenzi wa afisi za idara ya Uvuvi – Unguja na Pemba imekamilika.
- d. Ujenzi wa afisi za Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania umemalizika na mamlaka ipo katika harakati za kuhamia katika jengo jipya huko Fumba.
- e. Ujenzi wa soko la Tumbe umo katika hatua za mwisho. Kwa sasa wajenzi wapo katika hatua ya kuezeka na kumalizia baadhi ya sehemu za kuta.

- f. Akaunti ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu imefunguliwa ambayo inafanya kazi na ina bakaa ya dola za kimarekani 3,166,692 kwa sasa.
- g. Kuimarishwa kwa usimamizi wa bahari kuu kwa kuwekwa vifaa vya ufuatiliaji (*Vessel Monitoring System (VMS)*).
- h. Kumalizika kwa mpango wa biashara wa Mamlaka ya Uvuvi wa bahari kuu (*Preparation of DSFA business plan*).
- i. Kuwekwa kwa Matumbawe 4 ya asili baharini (*four artificial Fish Aggregating Devices (FADs)*).
- j. Mfuko wa kuimarisha uhifadhi wa bahari na rasilimali zake umeanzishwa (*establishment of the Marine Legacy Fund (MLF)*).

2: USIMAMIZI WA ENEO LA BAHARI NA UKANDA WA PWANI

- a. Wakulima wa mwani 7000 na wavuvi 8000 wa visiwa vya Unguja na Pemba wamepewa taaluma katika kutekeleza Uvuvi na Ukulima wa Mwani Bora wenye faida kubwa ilitolewa,
- b. Utafiti wa kusaidia na kufuatilia miradi na vikundi 317 umefanyika katika miradi ya jamii kwa Unguja na Pemba na imebainika kuwa 85% ya miradi hiyo inafanya vizuri katika utekelezaji wake.
- c. Jumla ya wafanyakazi 457 katika taasisi tafauti zinazohusiana na uhifadhi wa mazingira wamepatiwa udhamini wa masomo mbali mbali kama ni sehemu ya kujenga uwezo, jumla hiyo inajumuisha mafunzo ya muda mrefu, muda mfupi na ziara mbali mbali za ndani na nje ya nchi. Aidha, mradi umewezesha jumla ya wanajamii 12 kufanya ziara za kimafunzo nchini Indonesia, vile vile idara ya vyama vya ushirika Zanzibar kwa kushirikiana na *MACEMP* imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi 85 na wastani wa wanachama 190 wamepatiwa taaluma hizo Unguja na Pemba.
- d. Kazi ya tathmini ya kiwango na uwezo wa upeo wa kuhudumia watalii (*carrying capacity*) na watembezaji kwa kulinganisha na rasilimali za maeneo ya hifadhi za baharini za *MENAI*, *MBCA* and *PECCA* Kazi inaendelea.
- e. Kazi ya kuanza mpango wa utalii kwa Ukanda wa Pwani (*tourism management plan*). Kazi hii nayo Kazi inaendelea.
- f. Kuanzishwa kwa mpango shirikishi wa Uhifadhi wa usimamizi wa rasilimali za ukanda wa pwani (*the intergrated coastal zone management – ICZM*) ambapo mipango 10 (*plans*) imo katika majaribio katika wilaya 1o za Zanzibar.
- g. Kuimarishwa kwa maeneo ya Hifadhi za baharini (*Marine Managed Areas*) ya Tumbatu *Marine Conservation Area (TUMCA)*, na Changuu Bawe *Marine Conservation Area (CHABAMCA)*.
- h. Kuimarishwa kwa Uhifadhi wa miokoko
 - Kuimarishwa kwa ufugaji nyuki
 - Kumalizik wa tafiti za *Mangrove Inventory na social economic importance of mangrove*
 - Kuandikwa kwa *Mangrove Management Plan*
 - Kupandwa hekta 457 za mikoko (sawa ma miche 183,586)
 - Kuimarishwa kwa vikundi vya Uhifadhi 127.

- i. Kuimarishwa kwa Maeneo ya hifadhi za kihistoria (*Cultural heritage sites*)
- utafiti wa kuorodhesha maeneo ya hifadhi ukefanyika
 - Utafiti kuhusu ujuzi wa asilisili (*Indigenous Knowledge*) umefanyika,
 - Uwekaji wa mipaka ya ya maeneo ya hifadhi 25 umefanyika,
- o Maeneo ya hifadhi 13 yamefufuliwa na kukarabatiwa kwa kushirijiana na wananchi,
- Kazi ya ukarabati wa maeneo mawili ya kihistoria (*Palace Museum na Beit el Ajaib*) inaendelea.
 - Hati za uthibitisho (*title deeds*) kwa umiliki wa maeneo 7 ya kihistoria ya Kizimbani, Shakani, msikiti wa Kizimkazi, magofu ya Kizimkazi, magofu ya Fukuchani, Mvuleni na magofu ya Mwinyi Mkuu, Dunga zimepokelewa na kuhifadhiwa katika Idara ya Mambo ya Kale.
 - Kazi ya ikolijia kwa uchimbaji na kutathmini mambo ya kihistoria ya eneo la kihistoria la Chwaka – Tumbe Kaskazini Pemba imefanyika.
- j. Utafiti juu ya ukulima wa mwani wa *Cottonii* katika maji ya kina kirefu, umefanyika huko Gando Pemba. Utafiti huu umefanywa na Kampuni ya Birr.
- k. Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima imewezeshwa katika:
- Kushajiisha jamii katika kuendesha miradi midogo midogo.
 - Kutoa majarida ya biashara (*the Zanzibar Business News*)
- l. Ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi wa rasilimali za bahari na mazingira yake ambapo:
- Kamati za uvuvi 137 zimeanzishwa na kuendelezwa.
 - Kamati 66 za ukulima wa mwani pamoja na sheria ndogo ndogo (by-laws) zimeanzishwa.
- m. Kuimarishwa kwa ubora wa samaki na mazao ya baharini kwa ujenzi wa masoko ya samaki ya Tumbe na Kendwa.

TASAF

Mradi wa *MACEMP* umefanikiwa kuviwezesha vikundi vya jamii 322 hapa Zanzibar kupitia TASAF, ambapo jumla ya wanajamii 17,125 na familia zao wameweza kufaidika.

URATIBU WA MRADI NA KUJENGA UWEZO

Kufanikisha mafunzo katika fani na nyanja tofauti (*Capacity Building*) kama ifuatavyo:

Kiwango	Idadi
<i>Certificate</i>	127
<i>Diploma</i>	50
<i>Advanced Diploma</i>	7
<i>Post Graduate Diploma</i>	5
<i>Bachelor Degrees</i>	45
<i>Masters Degrees</i>	13
Mafunzo mafupi	86
Jumla	333

KIAMBATANISHO 2: MRADI WA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA MIFUGO

JINA LA MRADI	MRADI WA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA MIFUGO
MUDA WA MRADI	MIAKA MINNE (2011/12 - 2014/15)
JUMLA YA GHARAMA	7,200,000,000.
Lengo Kuu	Kuimarisha miundo mbinu inayohitajika kuleta ufanisi wa uzalishaji na masoko kwa mifugo na bidhaa za mifugo.
<p>Malengo ya Jumla:</p> <ul style="list-style-type: none"> i) Ujenzi wa machinjio mawili mapya ya kisasa ya ng'ombe Unguja na Pemba. ii) Ujenzi wa machinjio ya kisasa, mawili ya kuku, Unguja na Pemba. iii) Kuyafanyia ukarabati majosho makongwe na ujenzi wa majosho mepya Unguja na Pemba. iv) Kufanya ukarabati wa miundo mbinu wa karantini ya Kisakasaka na kuanzisha karantini nyengine huko Pemba. v) Kuzifanyia ukarabati maabara na vituo vya mifugo vilivyopo na kujenga maabara nyengine mpya Unguja na Pemba. vi) Kuimarisha miundo mbinu ya masoko na kuongeza thamani bidhaa zitokanazo na mifugo kwa soko la ndani na nje. vii) Kuanzisha na kuendeleza kituo cha utafiti na shughuli za utafiti zinazoendana na mazingira ya Zanzibar. viii) Kujenga uwezo kwa watafiti na wasaidizi watafiti. ix) Kueneza teknolojia mpya na rahisi za ufugaji kwa walengwa na wadau wa sekta ya mifugo. 	
Fedha iliyotengwa 2011/2012	Jumla ya shilingi 243,000,000 zilitengwa kwa kazi za mradi huu
<p>Malengo ya Mwaka 2011/2012:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Ujenzi wa chinjio jipya na la kisasa huko Kisakasaka 	
<p>Utekelezaji Halisi 2011/2012</p> <ul style="list-style-type: none"> • Ziara ya wataalamu kutembelea machinjio ya kisasa Tanzania bara (Sumbawanga, Dodoma na Arusha) kwa ajili ya kutayarisha Hududi Rejea za kutafuta mzabuni wa kuandaa michoro ilifanyika. Aidha, mchakato wa kumpata mzabuni wa kutayarisha michoro kwa ajili ya machinjio mapya na ya kisasa ulianza katika robo ya pili, lakini kutokana na idadi ndogo ya wazabuni waliojitokeza kufanya kazi hiyo, mchakato huo umeanzwa upya na unategemea kuendelea hadi mwaka ujao wa fedha. • Ujenzi wa kituo kimoja cha Unguja Ukuu umeanza kwa ununuzi wa vifaa vya ujenzi huo. Pia vifaa kwa ukarabati wa vituo vya Mahonda na Dunga pamoja na nyumba ya mfanyakazi wa kituo vimenunuliwa. 	
Gharama kwa mwaka 2012/2013	Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Mradi umetengewa jumla ya shilingi 200,000,000 kutoka serikalini.
<p>Malengo ya mwaka wa fedha 2012/2013</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Kuendelea na shughuli ya ujenzi wa chinjio la Kisakasaka 	

2. Kuandaa michoro ya ujenzi kwa kituo cha utafiti wa mifugo Chamanangwe
3. Kuandaa michoro ya ujenzi wa maabara ya mifugo Kizimbani.
4. Ujenzi wa kituo cha Unguja Ukuu na kuendeleza ukarabati wa vituo vya Mahonda na Dunga.

KIAMBATANISHO 3: Orodha ya Wafanyakazi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi

N o	IDARA	UNGUJA			PEMBA			JUML A
		W/UM E	W/WAK E	JUML A	W/UM E	W/WAK E	JUML A	
1	Utumishi na Uendeshaji	37	20	57	9	8	17	74
2	Mipango, Sera na utafiti	6	3	9	3	0	3	12
3	Uzalishaji Mifugo	116	52	168	50	10	60	228
4	Utabibu wa Mifugo	117	78	195	39	8	47	242
5	Maendeleo ya Uvuvi	83	25	108	32	4	36	144
6	Mazao ya Baharini	17	7	24	11	4	15	39
	JUMLA	376	185	561	144	34	178	739

KIAMBATANISHO 4: Orodha ya Wafanyakazi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Viwango vya elimu zao

No	Ngazi ya Utaalamu	Idadi ya Unguja	Idadi ya Pemba	Jumla	Asilimia
1	PhD	1	-	1	0.1%
2	MSc	13	-	13	1.8%
3	BSc	19	5	24	3.2%
4	PGD	3	-	3	0.4%
5	Adv. Diploma	4	1	5	0.7%
6	Diploma	140	40	180	24.4%
7	Certificate	94	37	131	17.7%
8	Form VI	6	2	8	1.1%
9	Form IV	80	14	94	12.7%

10	0-Form III	201	79	280	37.9%
	Jumla	561	178	739	100.0%

KIAMBATANISHO 5: MRADI WA KUPANDISHA NG'OMBE KWA SINDANO

JINA LA MRADI	MRADI WA KUPANDISHA NG'OMBE KWA SINDANO
MUDA WA MRADI	Umeanza 2010/11 unamaliza 2017/18
JUMLA YA GHARAMA	Shilingi 1,141,500,000
Lengo Kuu	Kupunguza umasikini kwa kuongeza kipato cha wafugaji wadogo wadogo kwa kuongeza uzalishaji wa ng'ombe wa kienyeji kwa kuwapandishia madume bora yenye sifa za uzalishaji wa maziwa na kuzalisha ng'ombe chotara.
Fedha zilizotengwa 2011/2012	141,500,000
<p>Malengo ya Mwaka 2011/2012: Mradi ulikuwa na malengo yafuatayo:-</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Kuendelea kuyahudumia madume yalioko kituoni. 2. Kukusanya, kutengeneza na kuhifadhi mbegu kutoka katika madume bora ya ng'ombe wa maziwa. 3. Kuendelea kuutunza mtambo wa "Liquid Nitrogen". 4. Kusambaza "Liquid Nitrogen" na mirija ya mbegu bora kwa ajili ya upandishaji. 5. Kukamilisha ukarabati wa jengo na kulizungushia uzio eneo la Kituo. 6. Kufanya matayarisho ya upandaji majani ya malisho kwa ajili ya madume yaliyopo kituoni. 7. Kuendelea kutoa mafunzo kwa wapandishaji waliopo kazini. 	
<p>Utekelezaji Halisi 2011/2012:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Madume yalipatiwa matibabu na chakula 2. Jumla ya mirija 1,008 ya mbegu bora za ng'ombe wa maziwa zilitengenezwa na kutumika. 3. Mtambo umepatiwa matengenezo ya kawaida mara mbili kutoka kwa fundi wa Kampuni uliyonunuliwa. 4. Jumla lita 3,500 za "Liquid Nitrogen" na mirija 3,109 za mirija ya mbegu bora za ng'ombe imesambazwa kwa ajili ya shughuli za upandishaji. 5. Ukarabati wa jengo haukufanyika na badala yake kumefanyika marekebisho ya mwendo wa umeme kwa kuweka transfoma mpya ili shughuli za uzalishaji wa "Liquid nitrogen" ziendeleo. Aidha, shughuli ya kuweka uzio imeanza. 6. Upandaji wa majani haukufanyika kutokana na kutokamilika kwa shughuli ya uzungushaji wa uzio kituoni. 7. Jumla ya wapandishaji 25 walipatiwa mafunzo kazini, vile vile pikipiki 2 pamoja na mitungi midogo 8 ya kuhifadhia mbegu imenunuliwa ili kuimarisha huduma za upandishaji. 	
Fedha zilizotengwa 2012/2013	122,000,000

Malengo ya Mwaka 2012/2013 ya mradi ni kama yafuatayo:

1. Kukamilisha ujenzi wa uzio kituoni.
2. Kuimarisha huduma za upandishaji kwa kuzalisha lita 3,000 za “Liquid Nitrogen” na kupandisha ng’ombe 4,000 kwa njia ya sindano
3. Kuimarisha huduma za afya kwa vidume vya mbegu (ununuzi wa madawa ya kinga na tiba).
4. Kuimarisha lishe ya vidume vya mbegu (Ununuzi wa chakula cha ziada).
5. Kuanzisha shamba la malisho kwa vidume vya mbegu.

KIAMBATISHO 6: MRADI WA KUDHIBITI MAFUA YA NDEGE

Jina la mradi	MRADI WA KUDHIBITI MAFUA YA NDEGE
Muda wa mradi	2006/2007 – 2014/2015
Jumla ya gharama	TZS 1,200,000,000.
Lengo Kuu	Kudhibiti mafua ya ndege na magonjwa yasiyo na mipaka kuingia Zanzibar
Fedha zilizotengwa 2011/2012	TZS 55,000,000 kutoka SMZ
Malengo ya Mwaka 2011/2012: Kununua vifaa vya maabara (<i>Reagents/equipments</i>)	
Utekelezaji Halisi 2011/2012 Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2012 kazi zifuatazo zlikuwa zimekamili:- <ol style="list-style-type: none"> 1. Vifaa na vitendea kazi mbalimbali vya maabara vimenunuliwa. 2. Utoaji wa mafunzo kwa maofisa 42 kutoka Unguja na Pemba juu ya utumiaji wa vifaa vya ufatiliaji wa mwenendo wa maradhi. 	
Fedha zilizotengwa 2012/2013	TZS 80,000,000
Malengo ya Mwaka 2012/2013: <ol style="list-style-type: none"> 1. Kufuatilia mwenendo wa mafua makali ya ndege pamoja na maradhi ya mifugo yasiyokuwa na mipaka. 2. Kutoa mafunzo kwa madaktari wasaidizi wa mifugo Wilayani juu ya upashanaji habari za magonjwa ya mifugo. 3. Ununuzi wa vifaa na madawa ya maabara za mifugo. 4. Kufuatilia mienendo ya maradhi mbali mbali yanayosambazwa na kupe. 5. Kutoa chanjo ya maradhi ya mahepe kwa kuku na vibuma kwa n’gombe. 6. Uchunguzi wa maradhi ya kiwele na usafi wa maziwa. 	

KIAMBATISHO 7: MRADI WA KUDHIBITI KICHAA CHA MBWA

JINA LA MRADI	MRADI WA KUDHIBITI KICHAA CHA MBWA
MUDA WA MRADI	2005/2006 – 2014/2015
JUMLA YA GHARAMA	Gharama za mradi huu hupangwa kila mwaka na kuidhinishwa na mfadhili (WSPA) na Serikali.
Lengo Kuu	<ol style="list-style-type: none"> i. Kudhibiti na hatimae kutokomeza kichaa cha mbwa ili kutokomeza maambukizi ya kichaa kwa binaadamu. ii. Kuongeza muamko kwa wafugaji na raia juu ya haki za wanyama na kudhibiti ukatili dhidi yao
Fedha zilizotengwa 2011/2012	Jumla ya shilingi 95,000,000 kutoka SMZ na dola za kimarekani 75,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo zilitengwa kutekeleza Mradi kwa mwaka wa fedha 2011/2012
<p>Malengo ya Mwaka 2011/2012: Mradi ulikuwa na malengo yafuatayo: -</p> <ol style="list-style-type: none"> 1) Kuendelea na zoezi la kutoa chanjo kwa paka na mbwa. 2) Kufanya mapitio ya sheria ya haki za wanyama. 3) Kutoa mafunzo ya umuhimu na hatari za mbwa. 4) Kuwaelimisha wamiliki wa mbwa kuhusu umuhimu wa kuchanja mbwa. 5) Kusaidiana na wafugaji mbwa kuboresha afya za mbwa. 	
<p>Utekelezaji Halisi 2011/2012:</p> <p>Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa ulifanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Jumla ya mbwa 7,887 na paka 1,019 walipata chanjo dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa. 2. Kwa kushirikiana na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, sheria ya haki za wanyama imepitwa. 3. Semina 10 juu ya umuhimu na hatari za mbwa na umuhimu wa kuchanja mbwa zilifanywa; moja kwa kila Wilaya Unguja na Pemba. 4. Kwa kushirikiana na wafugaji, mbwa 262 walifungwa uzazi, mbwa 7,375 walipatiwa dawa za minyoo, mbwa 2,520 waliogeshwa kwa ajili ya kuwakinga na maradhi yanayotokana na kupe na paka 435 wamefungwa uzazi. 	
Fedha zilizotengwa 2012/2013	Jumla ya shilingi 80,000,000 kutoka SMZ na dola za kimarekani 44,000 (TZS 69,960,000) kutoka kwa washirika wa maendeleo zimetengwa kutekeleza Mradi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.
<p>Malengo ya Mwaka 2012/2013 ya mradi ni kama yafuatayo:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Kuendeleza kampeni ya uchanjaji mbwa 14,000 na paka 1,500. 2. Kufunga uzazi mbwa 300 na paka 500 kwa lengo la kupunguza kuenea kwa mbwa na paka wazuzuraji. 	

3. Kufanya matibabu ya maradhi mbali mbali ya mbwa na paka.
4. Kutoa taaluma kwa jamii juu ya utunzaji bora wa mbwa na paka.
5. Kuiboresha maabara ya uchunguzi wa maradhi ya mifugo ya Maruhubi – Unguja na Wete – Pemba.
6. Kuelimisha jamii juu ya maradhi ya kichaa cha mbwa kupitia vyombo vya habari.
7. Kusaidia maendeleo ya uchunguzi kuhusu maradhi ya kichaa cha mbwa.

KIAMBATISHO 8: MRADI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI (MACEMP)

JINA LA MRADI	MRADI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI (MACEMP)
MUDA WA MRADI	Umeanza: Februari 2006 Hatua za ukamilishaji wa Mradi zitaanza 31 Agosti 2012 hadi Disemba 2012.
JUMLA YA GHARAMA:	
US DOLA MILLION 61	
ZANZIBAR (40%): 25,906,737.31	
BARA (60%):	
Lengo Kuu la Mradi wa MACEMP	Kuimairisha matumizi endelevu ya bahari kuu na bahari ya maji madogo, kuimarisha ukusanyaji mapato yatokanayo na uvuvi, kupuguza hatari za uharibifu wa mazingira, kuinua hali ya maisha ya wanajamii wanaoishi katika wilaya zilizo katika ukanda wa pwani. Pia mradi umelenga kuimarisha miundo mbinu na utendaji wa taasisi zinazotekeleza maradi
Fedha iliyotengwa 2011/2012	5,784,297.00
Malengo ya Mwaka 2011/2012:	
<ol style="list-style-type: none"> 1. Kuendelea na ziara za ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya jamii kwa Unguja na Pemba. 2. Kukamilisha ujenzi wa afisi za Idara ya Uvuvi kwa Unguja na Pemba. 3. Kukamilisha ujenzi wa afisi za Mamlaka ya Uvuvi wa bahari kuu Tanzania zinazojengwa Fumba – Unguja. 4. Kuanza kwa ujenzi wa soko la Tumbe kisiwani Pemba. 5. Kuendelea na ukarabati wa maeneo mawili ya Kihistoria (<i>Palace Museum, Beit el ajab na Mtoni Palace</i>). Aidha, maeneo mengine 25 kwa Unguja na Pemba yatapimwa na taarifa zake kuhifadhiwa kwa matumizi ya vizazi vya hivi sasa na vizazi vijavyo. 6. Kuendelea kugharamia masomo kwa wataalam na watendaji mbali mbali wa mradi na idara ndani na nje ya nchi. 7. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yanayohusu mamlaka ya Uvuvi wa Bahari kuu Tanzania. 8. Kukamilisha mchakato wa uanzishwaji wa maeneo mapya ya Hifadhi ya Tumbatu (TUMCA) na visiwa vya Mji Mkongwe (Bawe, Chumbe na Prison) - CHABAMCA. 9. Kukamilisha utafiti wa uwezo wa maeneo ya hifadhi na kiwango cha watalii ambao wanaweza kutembelea bila kuathiri mazingira. 10. Kutangaza mafanikio ya Mradi wa MACEMP ndani na nje ya Nchi pamoja na kuanza utaratibu wa kuanzishwa kwa MACEMP II ili kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa. MACEMP II itaelekeza jitihada zake kwenye maendeleo zaidi. 11. Kuendelea kuwawezesha wadau wa mradi kutekeleza majukumu yao kwa kuwapatia vifaa, 	

nyenzo na huduma nyenginezo zinazohusu kazi za mradi.

12. Kuendelea na usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa matumizi endelevu ya ardhi (**Land use plans**).
13. Mapitio ya sera ya mazingira ya 1992 na sheria ya mazingira ya mwaka 1996.

Utekelezaji Halisi 2011/2012

1. Ufuatiliaji mradi kwa vikundi 322 umefanyika katika miradi ya jamii kwa Unguja na Pemba. Aidha tathmini iliofanywa imebainika kuwa asilimia 85 ya miradi ya uvuvi, ufugaji wa kuku, ufugaji nyuki, uhifadhi na utunzaji mikoko na miradi ya mbuzi wa maziwa inafanya vizuri. (Hata hivyo kwa baadhi ya miradi ya uvuvi bado haijafikia malengo yaliyokusudiwa kwa sababu ya upungufu wa samaki unaotokana na uvuvi haramu).
2. Ujenzi wa afisi za idara ya Uvuvi – Majengo ya Idara ya Uvuvi kwa Unguja na Pemba yamekamilika na hivi sasa Wizara ya Mifugo na Uvuvi imo katika harakati za kuhamia.
3. Ujenzi wa afisi za Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania umemalizika na mamlaka ipo katika harakati za kuhamia katika jengo jipya huko Fumba.
4. Ujenzi wa soko la Tumbe umo katika hatua za mwisho. Kwa sasa wajenzi wapo katika hatua ya kuezeka na kumalizia baadhi ya sehemu za ndani ikiwa ni pamoja na vifaa vya umeme, maji n.k.
5. Jengo la Palace Museum liliopo Mnazimmoja ujenzi wa ukarabati umekamilika na sasa liko katika hatua za mwisho za kupakwa rangi kwa mujibu wa mkataba. Jengo la Beit el Ajaib kazi za uwekaji umeme zimekamilika na ziko katika hatua za mwisho kukamilisha uwezekaji wa mabati kwa mujibu wa mkataba. Pia maeneo ya hifadhi za kimaumbile 25 yamepimwa na tayari maeneo 7 yameshapatiwa hati miliki na taarifa zake zimehifadhiwa kupitia Idara ya Mambo ya Kale.
6. Mradi wa MACEMP umegharamia masomo kwa wataalamu 100 ndani na nje ya nchi. Aidha jumla ya wafanyakazi 457 katika taasisi tafauti zinazohusiana na uhifadhi wa mazingira wamepatiwa udhamini wa masomo mbali mbali kama ni sehemu ya kujenga uwezo, jumla hiyo inajumuisha mafunzo ya muda mrefu, muda mfupi na ziara mbali mbali za ndani na nje ya nchi. Mradi pia umewezesha jumla ya wanajamii 12 kufanya ziara za kimafunzo nchini Indonesia, vile vile idara ya vyama vya ushirika Zanzibar kwa kushirikiana na MACEMP imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi 85 na wastani wa wanachama 190 wamepatiwa taaluma hizo Unguja na Pemba. Idadi hiyo ni mafanikio makubwa kwa upande wa mradi na serikali kwa ujumla kwani hii ni zaidi ya asilimia mia ya lengo katika kujenga uwezo kwa watendaji kulingana na ripoti ya tathmini ya mahitaji juu ya mafunzo kwa watendaji wa mradi (*Training need assessment*).
7. Mradi umeendelea kusimamia utekelezaji na majukumu ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (*Interim arrangement*) katika kazi zake muhimu zikiwa pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la ofisi huko Fumba, kufanya kazi za dori na ufuatiliaji wa meli za uvuvi wa bahari kuu kwa kutumia vyombo maalum (VMS), na pia kufanya ziara ya kujifunza na mikutano ya kimataifa ndani na nje ya nchi.
8. Mradi umegharamia uanzishwaji wa maeneo mapya ya Hifadhi ya Tumbatu (TUMCA) na visiwa vya Mji Mkongwe (CHABAMCA) ikiwa pamoja na kuanzisha kitengo cha hifadhi za bahari “*Marine Conservation Unit – MCU*”, kiliyopo chini ya Idara ya Mandeleo ya Uvuvi.
9. Utafiti wa uwezo wa maeneo ya hifadhi na kiwango chaa watalii bado unaendelea kwa utaratibu wa kujazwa fomu maalumu zinazotumiwa na wavuvi pamoja na wadau wanaotembeza wageni katika maeneo ya hifadhi za baharini za MIMCA, MBCA and PECCA.

10. Mafanikio ya mradi wa MACEMP yametangazwa kupitia magazeti, na tovuti ambayo bado inaendelea kuimarishwa kwa kuongezewa taarifa zake.
11. Kuhusu MACEMP II bado serikali inaendelea na mazungumzo na wadau mbalimbali ikiwemo Benki ya dunia ili tuweze kuwawezesha wadau kwa kuwapatia vifaa, nyenzo na huduma nyenginezo.
12. Kwa upande wa usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa matumizi endelevu ya ardhi (*Land use plans*), ramani 10 za matumizi ya ardhi pamoja na mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji vya Paje-Jambiani na Makangale-Tondooni zimekamilika.
13. Mapitio ya Sera ya Idara ya Mazingira yamefanyika na hatua za mapitio ya sheria ya mwaka 1996 zinaendelea.

Gharama kwa mwaka 2012/2013	Mchango wa Serikali TZS 100,000,000
Malengo ya mwaka wa fedha 2012/2013	
<ol style="list-style-type: none"> 1. Kuendelea kutangaza mafanikio ya mradi ndani na nje ya nchi. 2. Kuandaa ripoti ya ukamilishaji wa mradi (<i>Implementation completion report</i>) 3. Kukamilisha malipo ya mafunzo kwa wanafunzi wa mwaka wa mwisho waliopo ndani na nje ya nchi 4. Kuratibu na kufuatilia miradi midogo midogo iliyobuniwa na wananchi wenyewe pamoja na kuweka matumbawe ya kienyeji. 5. Kufanya malipo ya mwisho ya washauri elekezi pamoja na zabuni zilizokuwa hazijalipwa. 6. Kuendelea na kuimarisha maeneo mapya ya hifadhi. 7. Kuendelea kusafisha matumbawe ya baharini 8. Kuendelea na vikao mbalimbali vya wadau wa mradi. 9. Kuendeleza mchakato wa kuanzishwa mfuko wa bahari (MLF) 10. Kuendelea na mazungumzo na wadau mbalimbali kuhusiana na upatikanaji wa miradi mbadala 	

KIAMBATISHO 9: MRADI WA UVUVI WA BAHARI KUU

JINA LA MRADI	Mradi wa Uvuvi wa Bahari Kuu
MUDA WA MRADI	Miaka minne
JUMLA YA GHARAMA	USD 22,323,529
LENGO KUU LA MRADI	Kuwawezesha vijana kuvua katika maji ya kina kirefu
MALENGO YA JUMLA YA MRADI 2011/2012	Hakukuwa na malengo mradi unaanza mwaka huu

UTEKELEZAJI 2011/2012	HALISI	Hakukuwa na utekelezaji (mradi bado ni mpya)
FEDHA 2012/2013	ILİYOTENGWA	Tshs 300,000,000
MALENGO YA MWAKA 2012/2013: <ol style="list-style-type: none"> 1. Kuendesha mafunzo kwa vijana 60 kuvua katika bahari kuu 2. Kufanya doria ndani na nje ya maeneo ya hifadhi 3. Kutoa taaluma juu ya uvuvi haramu 4. Kuvunja jengo la ZAFICO Malindi 		

KIAMBATISHO 10: MRADI WA KUIMARISHA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI

Jina la mradi	Mradi wa Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini
Muda wa mradi	2012/2013 – 2013/2014
Jumla ya gharama	USD 470,000 (Tshs 733,200,000) kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Korea (KOICA) Tshs 78,000,000 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
Lengo Kuu	Mradi huu ni mpya ambao una lengo la kufanya utafiti wa kutambua maeneo yanayofaa kufuga samaki kwa kutumia vizimba katika bahari ya Zanzibar
Fedha zilizotengwa 2012/2013	USD 470,000 (Tshs 733,200,000) kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Korea Tshs 78,000,000 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
Malengo ya Mwaka 2012/2013 ya mradi ni kama yafuatayo: <ol style="list-style-type: none"> 1. Kuainisha maeneo ya baharini yanayofaa kwa ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba. 2. Kukusanya taarifa za kimazingira za maeneo husika na aina za samaki wanaofaa kufugwa katika maeneo hayo. 3. Kujenga uwezo wa wafanyakazi katika kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini. 	

KIAMBATISHO 11: MAPATO YALIYOKUSANYWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2011 HADI MACHI 2012 NA MAPATO YANAYOTARAJIWA KUKUSANYWA KWA MWAKA 2012/2013

KASMA	MAELEZO	MAKADIRIO 2011/2012	MAPATO HALISI JULAI 2011 HADI APRIL 2012	ASILIMIA MAPATO MAKADI
	<i>AFISI KUU PEMBA</i>			
142259	ADA YA UTIBABU WA VINYAMA	7,000,000	7,084,750	101
142228	LESENI ZA UVUVI	3,000,000	4,977,500	166
142229	ADA ZA MAZAO YA BAHARINI	2,000,000	10,442,500	522
	JUMLA NDOGO	12,000,000	22,504,750	188
	<i>IDARA YA HUDUMA ZA MIFUGO</i>			
142259	ADA YA UTIBABU WA VINYAMA	48,000,000	43,004,500	90
	<i>IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI</i>			
142228	LESENI ZA UVUVI	20,000,000	22,556,800	113
	<i>IDARA YA MAZAO YA BAHARINI</i>			
142229	ADA ZA MAZAO YA BAHARINI	40,000,000	69,152,850	173
	<i>IDARA YA UZALISHAJI MIFUGO</i>			
142290	MAPATO YA MIFUGO			
	JUMLA NDOGO	108,000,000	134,714,150	125
	JUMLA WIZARA	120,000,000	157,218,900	131
	LESENI ZA UVUVI WA BAHARI KUU	900,000,000	133,770,234	15
	JUMLA KUU	1,020,000,000	290,989,134	29

MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO KUANZIA JULAI 2011 HADI APRIL 2012

IDARA / MRADI	SMZ		WASHIRIKA WA MAENDELEO		JUMLA MAKADIRIO 2011 / (A+C)
	MAKADIRIO 2011/2012 (A)	FEDHA ZILIZOPATIKA ANA July - April 2012 (B)	MAKADIRIO 2011/2012 (C)	FEDHA ZILIZOPATIKA NA July - April 2012 (D)	
HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO					
MRADI WA KUDHIBITI KUCHAA CHA MBWA	95,000,000.00	95,000,000.00	112,500,000.00	63,812,988.00	207,500,000.00
MRADI WA MAFUA YA NDEGE	55,000,000.00	55,000,000.00			55,000,000.00
UZALISHAJI WA WANYAMA					
MRADI WA UPANDISHAJI NG'OMBE KWA SINDANO	141,500,000.00	141,500,000.00			141,500,000.00
MIPANGO, SERA NA UTAFTI					
MRADI KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA MIFUGO	243,000,000.00	108,253,750.00			243,000,000.00
MAENDELEO YA UVUVI					
MRADI WA HIFADHI YA MAZINGIRA ZA BAHARI NA UKANDA WA PWANI (MACEMP)	216,000,000.00	216,000,000.00	8,676,445,000.00	4,845,940,676.43	8,892,445,000.00

JUMLA KUU	750,500,000.00	615,753,750.00	8,788,945,000.00	4,909,753,664.43	9,539,445,000.00
------------------	-----------------------	-----------------------	-------------------------	-------------------------	-------------------------

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA KAZI ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2012/2013

IDARA	MRADI	MAKADIRIO YA KAZI ZA MAENDELEO YA MWAKA 2012 / 2013	
		SMZ	WASHIRIKIJI WA MAENDELEO
MIPANGO SERA NA UTAFITI	Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo	200,000,000	
HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO	Kudhibiti Mafua ya Ndege	80,000,000	
	Kudhibiti Kichaa cha Mbwa	80,000,000	69,960,000
UZALISHAJI WA MIFUGO	Kupandisha Ng'ombe kwa Sindano	122,000,000	
MAZAO YA BAHARINI	Kuimarisha Ufugaji wa Samaki	78,000,000	733,200,000
MAENDELEO YA UVUVI	Kusimamia mazingira ya bahari na Ukanda wa Pwani (MACEMP)	100,000,000	
	Kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu	300,000,000	
JUMLA	-	960,000,000	803,160,000

MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA 2011/2012, FEDHA ZA KAZI ZA KAWAIDA KUANZIA JULAI 2011 HADI APRILI 2012

KASMA	IDARA	MAKADIRIO 2011/2012			FEDHA ZILIZOPATIKA	
		MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA YA MAKADIRIO	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO
03	<i>AFISI KUU PEMBA</i>	440,543,207	328,458,000	769,001,207	361,863,307	281,373,000
02	MIPANGO, SERA NA UTAFITI	221,453,000	111,132,000	332,585,000	49,102,233	99,454,000
04	UENDESHAJI NA UTUMISHI	292,842,685	104,621,000	397,463,685	212,200,709	97,463,810
06	HUDUMA ZA UTABIBU WA WANYAMA	386,608,710	60,211,000	446,819,710	368,503,289	52,500,000
08	UZALISHAJI WA WANYAMA	359,504,189	89,198,000	448,702,189	331,325,960	60,012,000
07	MAZAO YA BAHARINI	97,746,784	46,092,000	143,838,784	79,768,284	46,000,000
016	MAENDELEO YA UVUVI	273,009,545	60,288,000	333,297,545	223,664,585	46,440,400
	JUMLA KUU	2,071,708,120	800,000,000	2,871,708,120	1,626,428,367	683,243,200

MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2012/2013

IDARA	MAKADIRIO YA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2012 / 2013		
	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA
MIPANGO SERA NA UTAFITI	73,327,000	165,674,000	239,001,000
UENDESHAJI NA UTUMISHI	340,612,000	244,800,000	585,412,000
HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO	508,630,000	120,000,000	628,630,000
UZALISHAJI WA MIFUGO	452,500,000	119,000,000	571,500,000
MAZAO YA BAHARINI	112,405,000	94,248,000	206,653,000
MAENDELEO YA UVUVI	297,026,000	90,472,000	387,498,000
AFISI KUU PEMBA:			-
MIPANGO SERA NA UTAFITI	-	54,646,000	54,646,000
UENDESHAJI NA UTUMISHI	520,500,000	61,200,000	581,700,000
HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO	-	63,600,000	63,600,000
UZALISHAJI WA MIFUGO	-	64,600,000	64,600,000
MAZAO YA BAHARINI	-	77,112,000	77,112,000
MAENDELEO YA UVUVI	-	68,648,000	68,648,000
JUMLA	2,305,000,000	1,224,000,000	3,529,000,000

HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA MIFUGO, UTALII, UWEZESHAJI NA HABARI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Viwe Khamis Abdalla Kny/ Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nisome hotuba kwa niaba ya Mwenyekiti ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii muhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema na mwingi wa utukufu ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezeshwa kukutana leo hii ndani ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kuijadili Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, nachukuwa fursa hii kuwapa pole wafiwa na waathirika wote wa janga lililolikumba Taifa la kuzama kwa meli ya

Mv. Skagit, ajali ambayo ilitokea tarehe 18/7/2012 na kusababisha kupotea kwa ndugu zetu kadhaa pamoja na mali zao. Tunamuomba Mola mtukufu aziweke roha zao mahala pema peponi, Amin.

Mhe. Spika, kamati yetu inatoa pongezi maalumu kwa Mhe. Hamad Masoud, aliyekuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa uamuzi wake wa busara wa kujiuzulu nafasi hiyo. Kitendo hiki ni kutimiza uungwana wake kwa Taifa hili kwani kama tujuavyo kuwa *uungwana ni vitendo*. Hii ni dalili ya kupevuka kisiasa na kuweka mbele maslahi ya umma. Aidha, tunampongeza Mhe. Rashid Seif kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Miundo mbinu na Mawasiliano. Tunamtakia kheri na mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yake ya Kitaifa.

Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii kukushukuru kwa dhati kabisa wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati yetu kwa kutekeleza majukumu yao ya kikamati kikamilifu pamoja na kunituwa mimi kuja kuwasilisha maoni ya Kamati yetu mbele ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, tunatoa pongezi zetu za dhati kabisa kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi tukianza na Waziri Mhe. Abillah Jihad Hassan pamoja na watendaji wake wote ambao tumekuwa tukishirikiana nao bega kwa bega wakati wote Kamati inapohitaji msaada wao. Tunaamini kuendelea kwa mashirikiano haya kutaleta ufanisi mkubwa kwa utendaji wa Wizara hii.

Mhe. Spika, Kutokana na uzito wa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii, naomba uniruhusu kuwataja kwa majina ili waheshimiwa Wajumbe waweze kuwatambua kama ifuatavyo:

1. Mhe. Asha Bakari Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Mohammed Said Mohamed - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Assaa Othman Hamad - Mjumbe
4. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
5. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Abdi Mosi Kombo - Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
8. Mhe. Kazija Khamis Kona - Mjumbe
9. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu
10. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

Mhe. Spika, Kamati yetu imefarajika sana kwa kuongezeka kwa mchango wa sekta ya uvuvi kwenye pato la Taifa. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, tunayo furaha ya dhati kwamba sekta ya

uvuvi nchini imefikia asilimia 6.7 ya pato la Taifa. Haya ni mafanikio makubwa ambayo yanahitaji kuendelezwa ili wananchi waondokane na dhana ya kwamba uvuvi ni shughuli ya uchumi kwa wale ambao hawana kazi ya kufanya. Aidha, kukuwa kwa mchango wa sekta hii kitaifa kwende sambamba na kukuwa kwa pato la wavuvi ili nao wajivunie thamani ya kazi yao. Vilevile Wizara inapaswa kuongeza nguvu zaidi katika suala zima la utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya uvuvi haramu kwani wavuvi wengi bado hawana elimu ya kutosha juu ya uvuvi haramu na wala hawazijui kwa kina athari za uvuvi haramu.

Mhe. Spika, kukamilika kwa Sera ya mifugo nchini ni hatua muhimu ya kuelekea kwenye maendeleo endelevu ya sekta ya mifugo. Sera hii inalenga kuziba mapengo yaliyojitokeza katika sera ya kilimo ya mwaka 2002, ambayo kwa bahati mbaya haikuzingatia ustawi wa wanyama, hali ya upatikanaji wa masoko ya bidhaa za mifugo, utengenezaji na uuzaji wa nishati inayotokana na kinyesi cha wanyama pamoja na uongezaji wa thamani kwa bidhaa zetu za mifugo tunazozialisha. Ni matarajio ya Kamati yetu kwamba, utekelezaji wa sera hii utatusaidia kuimarisha huduma kwa jamii, kuimarisha ushauri wa jinsi ya kutekeleza sera hii kwa ufanisi, kuimarisha upatikanaji wa habari zinazohusu mifugo nchini na hatimaye kuchangia vyema kwenye pato la Taifa.

Mhe. Spika, miongoni mwa malengo yaliyopangwa kutekelezwa na Wizara hii katika mwaka wa fedha 2011/2012 ni kuanzisha mpango mkuu wa sekta ya uvuvi (*Fisheries Master Plan*). Hata hivyo lengo hilo halikutekelezwa kutokana na sababu za kiutendaji. Kutokana na hayo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa katika bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2012/2013 mpango huo unaanzishwa ili kutoa miongozo mizuri itakayoleta mafanikio zaidi katika sekta hii muhimu ya uvuvi.

Mhe. Spika, kuanzishwa kwa mabwawa ya kufugia samaki katika maeneo ya Kiungoni na Pujini Pemba kama ni mashamba darasa kwa wafugaji wa samaki pamoja na kupatiwa mafunzo ya ndani na nje kwa wafugaji wa mazao ya baharini ni hatua muhimu inayotarajiwa kuendelea kuchukuliwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kamati inashauri Wizara kuwaendeleza zaidi wafugaji hao kwa kuwatengea fedha maalumu kwa ajili ya kuwasaidia kwani wengi kati yao bado wanakabiliwa na uchache wa fedha na utaalumu wa kuyaendeleza mabwawa waliyoyaanzisha na hivyo kusababisha malengo ya Serikali ya kuwakwamua kutokana na umasikini uliokithiri kutofikiwa.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kutilia nguvu ufugaji wa samaki badala ya kutegemea samaki wanaovuliwa. Hii itaongeza uzalishaji na uvunaji wa samaki na hivyo kuongeza mapato nchini.

Mhe. Spika, Kamati ina furaha ya dhati kwa kuanzishwa programu ya kuendeleza miundombinu ya ufugaji ambayo itatekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 na kugharimu jumla ya shilingi milioni 200. Ni wajibu wetu kuelewa kuwa wafugaji na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla wanaisubiri kwa hamu programu hiyo ili hatimaye waweze kufanya kazi zao kwa mafanikio zaidi. Kwa mantiki hiyo basi, ni vyema kuitekeleza programu hiyo kama ilivyopangwa ili wafugaji wetu wazidishe bidii ya kufanya kazi na kuunga mkono juhudi za Serikali za kupunguza umasikini nchini.

Mhe. Spika, Kutokana na kupatikana kwa mtambo wa uhakika wa kupandishia ng'ombe pamoja na '*liquid Nitrogen*' jumla ya ng'ombe 2,867 wamepandishwa kwa njia ya sindano, ambapo ni

sawa na asilimia 125 ya uzalishaji kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Haya ni mafanikio makubwa ya kupigiwa mfano Mhe. Spika, kwani mradi huo unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yenyewe ulitengewa jumla ya shilingi 141,500,000/= na kupatiwa fedha zote ulizotengwa kwa asilimia mia moja. Aidha, tunatoa wito kwa Serikali kuendelea kuulea mradi huu kwa kuupatia fedha zote zilizoombwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ambazo ni shilingi za Kitanzania 122,000,000/= kwa kadri inavyowezekana. Halkadhalika tunawaomba wafugaji waendeleo kukitumia kitengo chetu hichi cha upandishaji wa ng'ombe kwa sindano kwa nia ya kupata mbegu bora zenye kutoa maziwa mengi na zenye kustahamili maradhi.

Aidha, Wizara ilijipangia mpango mzuri wa kuanzisha utoaji wa taaluma ya upandishaji mbuzi kwa njia ya sindano ambao kwa mwaka wa fedha 2011/2012 haukuweza kutekelezwa kutokana na kukosekana fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kuunusuru mradi huu kwa kutafuta mfadhili mwengine au kuutekeleza kwa kutumia fedha za ndani, kwani tumebaini kuwa mradi wa ufugaji wa mbuzi hususan mbuzi wa maziwa ni wenye tija kubwa.

Mhe. Spika, Kamati yetu imesikitishwa sana na hali za vituo vya utibabu wa mifugo Unguja na Pemba. Pamoja na matengenezo yaliyofanywa kwa baadhi ya vituo hivyo, bado vinakabiliwa na changamoto ya upungufu mkubwa wa samani za ofisini na wafanyakazi hali ambayo imewafanya watendaji wachache waliopo vituoni humo kuwa na hali duni. Hivyo, kupitia mkutano huu wa Bajeti, naomba kufikiriwa kwa yale maombi ya Wizara ya kuongezwa wafanyakazi hususan wataalamu ili kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi na kutazamwa watendaji wa sekta hii ya Utibabu wa mifugo kwa jicho la huruma ili kuwatia moyo wa kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, Kamati imefarajika sana kuona kuwa Wizara hii ina mashirikiano mazuri na jumuiya zinazoshughulikia kulinda haki za wanyama na matibabu ya wanyama. Kamati yetu inaisihi Wizara hii kuendeleza mashirikiano zaidi na jumuiya hizo na pia kusimamia vyema suala zima la haki za wanyama kwani wanyama wengi na hasa wanyama kazi (wakiwemo punda na ng'ombe) huwa hawatendewi haki na wafugaji wao kwa kubebeshwa mizigo mizito ikiambatana na kipigo kizito.

Mhe. Spika, Kilio cha wananchi wengi na hasa akina mama wanaojishughulisha na ukulima wa mwani nacho kimekuwa ni cha muda mrefu ambacho kinahitaji kunyamazishwa. Hivyo, Kamati inapendekeza kufanyiwa kazi kwa utafiti uliofanywa kupitia mradi wa *MACEMP* katika vijiji vya Fundo na Tumbe kisiwani Pemba, ambao unaonesha kuwa upo uwezekano wa kulima mwani wenye kuleta tija nzuri wa cottonii kwenye maji mengi kwa kutumia njia ya chanja za kueleza.

Aidha, Kamati yetu inapendekeza Wizara kufanya ziara za kuwakagua wakulima wa mwani mara kwa mara. Hatua hii ni muhimu ili kuweza kuelewa matatizo yanayowakabili ili kuyatafutia ufumbuzi muwafaka. Kadhalika, tunaikumbusha Serikali ule wajibu wa kuwatafutia mustakbali mwema wananchi wake wanaojishughulisha na ukulima wa mwani kwa kuwajengea viwanda vya kusarifu mwani na kuweza kupata soko la uhakika la mwani tena kwa bei nzuri. Vilevile Wizara iendeleo kufanya jitihada kubwa zitakazowawezesha wakulima wa mwani

kupata maeneo maalum ya kukaushia mwani hususan wakati wa mvua hasa kwa vile mwani unaponyeshewa na mvua huharibika.

Mhe. Spika, Mradi wa uvuvi wa bahari kuu unatarajiwa kutekelezwa katika mwaka 2012/2013 na kugharimu jumla ya dola za Kimarekani 22,323,529 ni mradi muhimu sana ulioibuliwa katika wakati mwafaka kabisa. Pamoja na malengo mazuri yaliyopangwa kwenye mradi huu, Kamati inapendekeza suala zima la kuwawezesha wavuvi wetu ili kumudu gharama za kuvua bahari kuu lizingatiwe kwa kiasi kikubwa kwani wengi wao hawamudu gharama za ununuzi wa nyenzo zinazohitajika. Kwa kuzingatia maslahi yanayopatikana kutokana na uvuvi wa bahari kuu, ni dhahiri kuwa kutowasaidia wavuvi wetu katika kufikia malengo tuliyojiwekea kutasababisha vijana kutoka nchi za jirani kuitumia fursa na nyenzo za Zanzibar bila ya kuinufaisha nchi yetu.

Mhe. Spika, Kamati yetu inatoa shukurani za dhati kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kwa kufanikiwa kukusanya mapato zaidi ya kiwango kilichokadiriwa kwa mwaka 2011/2012. Hadi kufikia mwezi Aprili 2012, jumla ya shilingi 22,556,800 zimekusanywa ambazo ni asilimia 112.7 ya malengo. Tunaishauri Wizara kukaza kamba katika suala zima la ukusanyaji wa mapato kwa mwaka huu wa fedha ili hatimaye matumizi mazuri yafanyike kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa uvumilivu wao na kuweza kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii. Aidha, napenda kuwaomba Wajumbe wako waichangie bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na hatimaye kuipitisha.

Kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari na vijana wenzangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, naunga mkono hotuba hii na naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Viwe tunakushukuru sana kwa uwasilishaji bora kabisa wa hotuba kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Waheshimiwa tunakwaza na muda kuhusiana kumaliza shughuli zetu. Tumejaribu kutoa ratiba mpya hapa inaonesha kwamba shughuli zetu tumalize tarehe 10/08/2012 na hii baada ya kutumia na muda wa nyongeza. Hii maana yake nini maana yake ni kwamba hotuba inawasilishwa kama leo, uchangiaji umalizike leo, kesho tufanye majumuisho baada ya hapo tuiite Wizara nyengine isome, ndivyo tunaweza tukenda na ratiba hii vyenginevyo tujituzishe muda zaidi ya ule muda tulioruhusiwa na kanuni ambayo hiyo itamaliza mfuko wa bajeti na hatimae tusiweze kufanya shughuli zetu huko usoni.

Sasa ili tumudu kufanya hivyo kuna mambo mawili ambayo waheshimiwa wajumbe nyinyi ndio mtaamua ili kusaidia shughuli zetu ili zende sawasawa. Moja ni kukubaliana kuzidisha muda mpaka saa tisa. Au kupunguza muda wa kuchangia uwe dakika 15 sasa hayo ni maamzi ambayo nawaomba mtoe nyinyi ilimradi shughuli zetu zimalizike kwa muda uliopangwa hapa. Kwenda zaidi ya tarehe itamaliza bajeti yetu na itakuwa matumizi yetu yamekwenda zaidi ya ambavyo zimekasimiwa na Baraza hili.

Sasa niliposema tuongeze muda mpaka saa tisa nimeona kuna wengine wamefurahi, lakini kuna wengine kidogo hawakufurahia. Kupunguza muda tukachangia kwa dakika 15 wengine wana

mengi ya kuzungumza, sasa inaonekana twende mpaka saa tisa. Nimuobe basi Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoa hoja ili Baraza likubali hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lilipanga shughuli zake kwa ratiba ya awali na kufuatia fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya mkutano huu ilikuwa tunaishia kati ya tarehe 3 au 4, na kwa kuwa shughuli za Wizara zilizobakia bado hazijamaliza, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako litenge kando kanuni ya muda wa kuzungumza, ili tuweze wajumbe wachangie wengi lakini tupunguze muda mpaka kufikia dakika kumi na tano. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Amekosea kidogo dalili zimeonekana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Samahani nimekosea kutoka saa nane na nusu tuunganisha mpaka saa tisa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Nikushukuruni waheshimiwa wajumbe kwa kusaidia kiti kumaliza shughuli zetu sawa sawa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri lakini kidogo naomba sana Mheshimiwa mtu sifa yake tumpe. Mhe. Spika, kwa kuwa sasa hivi kuna tatizo kubwa sana hasa kule Marumbi na nina imani hiyo Mheshimiwa Rais wetu, kipendwa chetu atafanya kwa jitihada zote kwa kwenda kuwaona wananchi wetu wa Marumbi na kuweza kuwasaidia lile tatizo lao la kila siku kila linakuwa ni kero. Sasa hiyo nimeona Mheshimiwa niilete massage ili kulitatua kuwa sera yetu ya Chama cha Mapinduzi ni kuweza kutatua matatizo kwa wananchi wetu. Sasa nimeona nilete hiyo ili Mhe. Rais aende haraka sana kwenda kuwasaidia.

Lakini vile vile Mhe. Spika, ukurasa wa pili nimsifu sana Mheshimiwa wangu Waziri kazi anazozifanya ni nzuri, anapita katika mkondo ule ule wa sera wa Chama cha Mapinduzi kwa kuwasaidia wananchi wake katika kuleta neema katika nchi hii. Mheshimiwa ninakushukuru sana kwa jitihada hizo na inshaalla Mungu akujalie uendeleo nazo ili wananchi waondokane na kero hizi ndogo ndogo za uvuvi pamoja na mifugo.

Lakini naingia ukurasa wa 6 sekta ya uvuvi. Mheshimiwa katika sekta ni muhimu sana, sekta hii inalingana na sekta tunosema kilimo ni uti wa mgongo na hii haina tofauti yoyote. Lakini hasa sekta hii inatakiwa tuiwezeshe, tatizo letu kubwa sisi tunashindwa kuwawezesha hawa wenzetu wahusika na wakaweza kufanyakazi zao nzuri na hasa kutokana na bajeti zao zinakuwa ni finyu sana na ndio maana yale malengo ambayo wanakusudia kuyaweka wanashindwa kuyafatilia kwa ukamilifu na hatimae tunakuja kuwasakama. Kwa hivyo Mheshimiwa naomba sana sekta hii ni muhimu sana mambo mengi wanakuwa wanaomba lakini hatimae hawakamilishi vile inavyotakiwa.

Nikiendelea na ukurasa huo huo wa saba ambamo katika masuala haya ya minai Mheshimiwa vijiji vyengine wanalalamika kutokana na mradi huu hawaoni faida zao. Sasa sijui kama ni kweli na kama ni kweli tuoneshwe jinsi gani faida au neema wanayoipata katika vijiji hivi vyenye minai, kwa sababu wengi, kwa mfano watu Kizimkazi, watu wa sehemu nyengine wanalalamika sana kuhusu mradi huu Mheshimiwa wanaambiwa kuna mradi huo lakini tija yao inakuwa ni ndogo sana kuipata kwa wao.

Hebu mimi naomba Mhe. Waziri ikiwa wewe ni Mheshimiwa ambaye uko karibu sana na Mkurugenzi husika naomba sana hili suala lifatiliwe ili tuweze kujua tatizo liko wapi kweli hawa watu hawafaidiki na mradi huu. Kwa sababu kuna mambo wanaambiwa wasifanye kwa mujibu wa sheria na wao wako tayari kusalenda yale masuala. Lakini kinyume chake tunaendeleza kuwatia umaskini badala ya kuwasaidia kwa lile jambo ambalo tumeshaliamua kwamba wasilifanye. Kwa hivyo mimi naomba Mheshimiwa hizi kero ambazo za hapa na pale hebu tujaribu Wizara tuziondoshe ili wananchi wetu tunaleta sera nzuri za mategemeo mazuri lakini hatimae inakuwa hakuna ufatiliaji inakuwa finishing yake haieleweki.

Mhe. Spika, nije katika suala hili la changamoto la sekta ya uvuvi. Mheshimiwa mimi nakubaliana kifungu cha (b) ni kweli ukurasa huo wa 9 kuwa uharibifu bado upo hatujaweza kuumiliki hili suala na wananchi wetu wanapokuwa wanalalamika wanasema, sisi kama hatujafanya biashara hii ya uharibifu hatuna biashara nyengine kwa sababu hawana nyenzo. Na ndio maana nikasema Wizara hii nayo tuipe power kama tunavyoipa wizara nyengine ya Kilimo kwa sababu wana mambo mengi sana wana activities nyingi sana za kuweza kuwasaidia wananchi na kuweza kuwaondolea umaskini wanajitahidi kiasi chao hapa na pale lakini meno ya kuwawezesha ndio maana nikasema tukiweza watu hawa wanaoleta uharibifu baharini wanoua matumbawe wanaofanya mambo mengine yoyote yaliyokuwa si mazuri kinyume na utaratibu, wenye kutumia mabomu, wenye kutumia mishipi iliyokuwa haitakiwi, wenye kutumia madema yaliyokuwa hatakiwi kwa mujibu wa sheria ninaomba sana Mheshimiwa hawa watu tuwawezeshe, tunawakataza lakini hapo hapo *to take action* ya kuwawezesha. Hilo ni suala ambalo la msingi sana Mheshimiwa lakini tutakuwa tunasema tu haufai haufai lakini hatimae wanarudi hakuna kuwezesha kuona ile hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa ukurasa wa 19 mambo ya ufugaji Idara ya Uzalishaji Mifugo. Mheshimiwa nimsifu sana Mhe. Waziri na nilikuwa ndio kilio changu na nilisema leo nipambane nae lakini ameeleza jambo zuri sana nimerudisha nyuma majeshi yangu amesema kuwa eneo la Pangei hatopewa mukezaji watakuwa nalo wenyewe kwa utafiti. Mimi ninakubaliana nalo asilimia mia kwa mia, kwa nini jamani tuwe tunatoa. Twende Bambi, Bambi mpaka leo hakuna jibu wa shamba lile la ufugaji wa ng'ombe Mheshimiwa hili nakuomba sana kwa msimamo wako na kuitekeleza sera yetu hebu wape watu wa Bambi lile shamba mifugo sasa hivi imeshakuwa late down hebu tuwape. Kwa sababu tukisema ukweli katika jimbo langu la Kitope tuna asilimia ziro kwenye ufugaji tumefeli ng'ombe tuliopelakwa si wazuri na nilitoa hadhari mapema kutokana na mradi ule sharti tuangalie jamani tuwape watu ng'ombe ambao waliokuwa wenye kwenda na hali halisi ya nchi yetu. Kitope ng'ombe wengi wamekufa, fedha za wavuja jasho zimepotea nyingi.

Sasa mara nyengine ninakuomba sana Mhe. Waziri tuwe serious na jambo lile, tusifanye utashi wa kutaka kukimbilia kunyan'ganya fedha tukaleta ng'ombe kama wale waliokuwa vibovu kabisa wamefeli sana wananchi wangu. Nataka jibu rasmi nipewe sababu gani ambao ng'ombe

waliokuwa wakipewa wale ni wabovu na wengine wamekufa na nimekwenda kuwaangalia mimi mwenyewe vibovu havifai ng'o. Sasa naomba sana Mheshimiwa wangu hili suala tukubaliane pamoja na jitihada zako lakini hapa sikubaliani napo nipewe sababu za kuridhisha kabisa wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa nini ng'ombe wamepelekewa wabovu.

Mheshimiwa niende kwenye mazao ya baharini, suala la mwani. Mhe. Spika, mara nyingi sana mimi nasema hebu tuwe wazi katika miradi hii, maana ya kuwa tuwe wazi tuwatafutie na wale wenyewe waweze kusafirisha kupeleka nje, ndio solution ya kuweza kuondoa umaskini nimesema wapewe zana ya kukaushia ile mimea ya mwani. Lakini tunazungumza hapa tunaonekana wawakilishi ndio wamezungumza tu. Mheshimiwa suala hili mimi nitakuwa mkali sana, kila siku tunawaachia hawa wawekezaji wanawadidimiza hawa, hakuna biashara ya kupeleka nje ukala hasara hata siku moja. Mimi nakataa kitu hicho na sisi tulikuwa wafanyabiashara hivyo hivyo tunajua. Nje huko huu mwani ukiipeleka kuna pesa chungunzima, yale mapezi ya papa yale ya samaki ukipeleka nje unapata biashara kubwa sana, kitu kidogo tu unafanyiwa supu basi unalipa dola. Kwa nini na hawa wasiruhusika, naomba sana Mheshimiwa waruhusike ili kwa kujiondolea umaskini waondoshe lile kero kila siku mtakuwa mnagombana wananchi kutokana na nini tusione tabu, lazima wapewe mashine za kuweza wao wenyewe ndio hapa imeandikwa wanaweza kutengeneza sabuni, usarifu mwengine kwenye matumizi ya vyakula.

Sasa watafanya vipi Mhe. Spika, pengine hata elimu hawana tunazungumza kwenye kitabu tunadanganya humu, hebu tuwe serious na hili jambo mara nyengine Mheshimiwa bajeti zinazokuja waje na activities zao watuoneshe jinsi ule muelekeo ulivyo. Lakini hapa sijui kama kweli wameshapewa matatizo hayo wameshasomeshwa sijui siwezi kujua. Sasa hiyo hali halisi naomba sana Mheshimiwa wananchi wa mwani ili waione kazi yao nzuri waweze kuwezesha kupewa vimashine vidogo vidogo vilivyokuwa cost yake sio kubwa sana. Mhe. Spika, kama nilivyosema leo Wizara hii sitaki niende sana.

Halafu la pili uvuvi wa juu wa ufugaji wa samaki. Mheshimiwa waziri nikusifu sana suala hiili nimeona jinsi gani unavyolipenda suala lile, maana yake kila siku bahari kuu samaki wenyewe leo mawimbi, hatuna vyombo vya kuendea huko. Mimi naomba sana ukazishe huu uvuvi wa juu wa kufuga samaki, tutainuka sana Mheshimiwa. Tena uwe serious sana suala hili ninakuomba bajeti nyengine unambie kuwa umeshaekeza zaidi ya miradi mitano sita katika mabwawa ya ufugaji hapo nitakuwa pamoja na wewe wala sikutabanishi. Lakini nataka hapo Mheshimiwa uwe serious na ninakuamini hivyo.

Kwa kumalizia nimshukuru sana amefanya kitendo kizuri sana Mhe. Waziri kwenda kusuluhisha mgogoro kati ya Chwaka na Marumbi ameingia mwenyewe kwenye boti, akawa survey mwenyewe akahahakikisha kuwa mipaka imewekwa kwa mujibu wa sheria zilizokubaliana baina ya pande mbili nalo hilo ninampa hongera hivyo ndivyo Waziri tunavyotaka. Mawaziri sio wakae katika ofisi tu tunataka wawajali wananchi na hizi kelele zetu kwa mujibu wa taratibu wa kanuni zetu za Baraza wazikubali katika utekelezaji. Mheshimiwa tunamshukuru sana sana Mhe. Waziri na hivyo ndivyo tunavyotaka Mhe. Waziri lazima uwe active ukiondoka katika Wizara ile umeonesha. Nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na Katibu Mkuu wake na Mkurugenzi wa Uvuvi pamoja na wakurugenzi wengine.

Sina zaidi Mheshimiwa ninaiunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kupata fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu subhanallahu wataala aliyenijaalia katika hali ya uzima na afya njema katika Baraza lako tukufu hili kuchangia mambo yetu ya nchi yetu pamoja na taifa letu kwa ujumla.

Mhe. Spika, leo tupo katika Wizara ya Uvuvi mimi nianze hapo sekta ya uvuvi. Sekta ya uvuvi kama tunavyojua nchi yetu ya Zanzibar ni visiwa na imezungukwa na bahari ina wavuvi wengi. Idara ya Uvuvi katika takwimu zake mwaka 2010 inatwambia ina wavuvi wasiopungua 34571 lakini mpaka kufikia mwaka 2013 wavuvi wanaweza kufikia hata laki moja. Mhe. Spika, wavuvi wetu wa Zanzibar yetu ni wavuvi wadogo wadogo, pamja na dhamira nzuri ya Serikali ya Mapinduzi yenye sura ya Umoja wa Kitaifa kuelekea kwenye uvuvi wa Bahari Kuu lakini hatujafika huko tunakusudia tu. Kama wavuvi wetu ni wadogo wadogo Mhe. Spika, tunataka kwanza tuwajue wavuvi wadogo wadogo ni wepi, tukeshajua tunaweza kuwatendea haki zote zinazostaili za uvuvi na bila ya kuwajua hatuwezi kuwatendea haki.

Mhe. Spika, wavuvi wadogo wadogo mmoja niseme ni wavuvi wanaovulia nyavu za macho madogo, samaki wake ni dagaa la tonge kwa tonge, kwa usemi wa mjini la kuosha, kuvua saladini, vibua na samaki wengine watakaolingia hata samaki wakubwa wanawapata. Ring net au kwa jina jengine mtando ndizo nyavu zinavua uvuvi huo lakingi ukilinganisha ring net na nyavu nyengine wanazomurika kwa taa ni sawa sawa, tofauti yake ring net aina ya mtando unavua mchana na nyavu za kumulika kwa taa zinavua usiku. Ukitaka ushahidi huo nenda soko la Malindi utajifunza mengi hilo moja.

Mhe. Spika, samaki aina ya pweza anavuliwa kwa mchokonoo au mangu kwa jina jengine ndoana. Sasa wewe unapokataza zana hizo kufanyia kazi pweza tutamvua kwa jambo gani. Ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwa majumuisho atueleze tuwache njia hiyo na tumvua pweza kwa jambo gani.

Mhe. Spika, tukiendelea na zana ambazo kuwa sheria hii namba 7 ya 2010 inakataza kuvulia ambayo ndio wavuvi wadogo wadogo wanazotumia bila ya zana hizo hakuna mvuvi mdogo mdogo hata mmoja atakaeingia baharini. Afadhali ya kutwambia uvuvi Zanzibar ni marufuku.

Mhe. Spika, tukiangalia kuna kitu kinaitwa bunduki sio bunduki hizi za askari wetu polisi bunduki za kuvulia baharini, hizi unavulia samaki mmoja mmoja, umevaa kioo chako, viatu vyako vya kuogelea na pengine hata chupa ya oxygen ya kuongezea hewa unatembea katika bahari na kifaa chako hicho samaki anatembea unachagua samaki unaemtaka na unamchoma hivi ndivyo inavyotumika bunduki ya kuvulia.

Haitoshi Mhe. Spika, katika zana wanazovulia wavuvi wetu wadogo wadogo ni mshipi na mshipi vile vile unavulia samaki mmoja mmoja kadiri ya Mwenyezi Mungu atakavyokuwezesha. Vile vile haitoshi viatu vya kuogelea vinamsaidia mvuvi katika kupata nguvu ya kuogelea pamoja na kujitafautisha na samaki hatarishi walioko ndani ya bahari. Kwa sababu unayo huu kama huna viatu basi inakuwa kama chambo cha samaki. Sasa leo hii kiatu cha kuogelea kinapigwa marufuku, je, tunawapeleka wapi wavuvi wetu.

Nitoe mfano ulio hai juzi tu tarehe 18 meli ya MV Skyget imezama, tunamshukuru Mwenyezi Mungu zana hizi hizi zinazokatazwa ikiwemo chupa ya oxygen na vioo ndizo zilizotumika kuokolea wale wenzetu waliofika mbele ya haki, tena walibebwa na vyombo vya serikali ikiwemo magari mpaka kwa ma-diver wetu waliopo Mtoni kule Unguja na wakasaidia zoezi hili. Sasa Mhe. Spika, atakapokuja waziri hapa atueleze zana hizo zina uharamu gani wa kuvua.

Mhe. Spika, nyavu za macho makubwa jarife halivui, jarife ni aina ya mtego unaotega na kuvua masamaki makubwa wakiwemo papa, mbawasi au ndoar na samaki wengine. Lakini wavuvi wetu wadogo wadogo hawewezi kwenda mbali, ndio sasa serikali inaanza kuvua bahari kuu na bado mipango haijakamilika. Sasa tuwajue wavuvi wadogo wadogo ndio hao.

Mhe. Spika, tando, tando ni uvuvi wa asilia na huu unavuliwa samaki waliochelewa katika mawindo lazima tufaham hivyo kila kitu kisifanywe haramu, lakini yote haya yamefanywa haramu. Lakini unapokataza mambo haya yote uvuvi Zanzibar upo mimi nasema uvuvi haupo na ni bora waziri anayehusika na mambo haya kutangaza moja kwa moja uvuvi hakuna. Lakini kama wavuvi wadogo wadogo wanaruhusiwa kuvua basi zana zote hizi nilizozitaja basi zitatumika. Na ninamuomba Mhe. Waziri pamoja na Idara ya Uvuvi isijenge uhasana na wavuvi, yeye amepata kazi kwa sababu kuwepo uvuvi na bila ya uvuvi yeye angekuwa hayupo katika sekta ile. Sekta ya uvuvi ni sekta binafsi ambayo imeajiri watu wengi ukiachana na wavuvi hata walaji na wafanyabiashara walio wengi.

Mhe. Spika, boti zinazotumika kwa wavuvi wetu wadogo wadogo ni boti aina ya Ngwanda, madau ya mti mmoja, Mitumbwi ya madau ya Kitumbatu, hizi ndio zana wanazotumia wavuvi wetu wadogo wadogo. Sasa shughuli zote hizi ukizuia uvuvi upo mimi nasema jibu uvuvi hapana. Sasa Mhe. Waziri akija hapa atupe maelezo ya kina ili tufaham laa atumie njia mbadala kwamba hizi tunazuia tukupeni hizi, tutashkuru wavuvi si wakaidi wakipata maelekezo yaliyo mazuri na wakapata zana watakwenda kiasi cha umbali mkubwa sana kuvua samaki.

Na mimi ninamuhakikishia Mhe. Waziri kwamba wavuvi aina ya mtando wanavua baharini, na siku moja ya jumamosi au jumapili twende mimi na wewe field moja kwa moja wewe usiteremke mimi nitakwenda tuangalie wanavua vipi uvuvi huu tutapata picha halisi. Lakini sio kwamba kila kitu tunakifanya ni haramu tutakuwa hatuwezi kufanyakazi zetu za kivuvi.

Mhe. Spika, nikija katika maeneo tengefu yaliyowekwa kwa jili ya ustawishaji. Lakini tukiangalia ghuba ya Minka, ghuba ya Minka imekusanya maeneo Lemba, Chwaka Bay, Matemwe, Pwani Mchangani, Kiwengwa, Pongewe, Uroa, Ukongoroni Michamvi na Marumbi. Hiyo ni ghuba ya Minka sasa ukiangalia sehemu zote hizo ni eneo tengefu ambazo zimewekwa wavuvi hawathubutu kufanya shughuli za kivuvi.

Tukija katika ghuba ya Tunka, ghuba ya Tunka imekusanya Tumbatu, Mkokotoni, Kidimni, Kendwa, Bumbwini, Tazari, Mwambale, Mangapwani na Mto wa Pwani zote ni sehemu ambazo wavuvi hawezi kufanya shughughuli zao za kivuvi. Sasa tuangalie je huyu mvuvi tumempa fursa kufanya shughuli zake kwa ufanisi. Kweli tumetangaza utalii kwa wote ni sawa tunapata pato la kitaifa ambalo kubwa lakini huyu mzalendo tumuuwe moja kwa moja awe hana haki ya kuitumia raslimali yake ya bahari. Mimi naona si vyema ningemuomba Mhe. Waziri ili mambo yake

yende sawia basi sheria hii kuileta Barazani kuifanyia marekebisho kama sheria nyengine zinazofanyiwa marekebisho si jambo la aibu ni sheria nyingi hapa tunazifanyia marekebisho.

Na hii sheria imekwenda mbali hii kazi yake ni kumdhibiti mvuvi tu, jambo la kusikitisha wavuvi wanavyopata shida na Mheshimiwa natoa kama mwakilishi wa wananchi sitetei Kojani narejea Zanzibar nzima. Marumbi na Chwaka sio Kojani lakini kuna mgogoro wa kutosha haitoishia hapo utakwenda utasambaa kote. Ninamuomba Mhe. Waziri pamoja na Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi asiwaone maadui wavuvi akae nao awape elimu na atafute njia mbadala ya kuweza kufanya kazi.

Mhe. Spika, ghuba ya Minai, ghuba ya Minai imekusanya Bweleo, Kizimkazi, Jambiani, Makunduchi, Unguja Ukuu, Bwefum, Mtende, Fumba na Kibondeni, angalieni sehemu zote hizo mvuvi hawezi kufanya kazi ukiangalia Unguja nzima imemaliza. Je tunajiuliza huyu mvuvi ana nafasi gani wakati wavuvi wetu ni wadogo wadogo hawana vyombo vya kufikia bahari kuu. Mhe. Spika, ninamuomba Waziri aje atueleze ni sehemu zipi wanazowapa wavuvi kufanya kazi zao. Ninafikiri hata mnaposafiri mnavikuta vitumbwi vyetu ni vidogo vidogo haviwezi kufika bahari kuu. Kwa hivyo waziri akija hapa atueleze kwa kina kabisa.

Mhe. Spika, wavuvi wetu hawa ambao ni wavuvi wetu wadogo wadogo wanapata shida sana kunakuwa na matatizo makubwa sana wakati mwengine anaporudi baharini anakwenda kuuza samaki anakamatwa na akifika nyavu zake na mitego yake inazuiliwa, ambao kuna mashine na mitumbwi yao halafu kuchomwa moto bila kufikishwa mahkamani, hili ni tatizo nguvu inatumika nyingi kuliko busara. Sasa kama nilivyosema sheria yetu hii kama ina mapungufu iletwe hapa tufanye marekebisho lakini zaidi ya hivi hatuna mvuvi.

Mhe. Spika: unazo dakika tano.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika. Jambo jengine Mhe. Spika, wavuvi ni watu wanaoranda katika bahari katika mawindo yao ya kutafuta samaki, mtu anaweza kuwa karibu na Kisiwa cha Chumbe hapo sehemu za Manyuni ilipozama meli juzi, wavuvi wetu kote huko wanafika. Mimi navijua vipwa vyote Manyuni iko pale, lakini inaweza kutokea dhoruba mtu akashindwa kwenda kujizuia upepo mpaka ukapita katika Kisiwa cha Chumbe kwa sababu kina papi, hili ni tatizo hatupati hata fursa wavuvi kufika.

Mhe. Spika, nikija katika Idara ya Mazao ya Baharini tunashukuru na tuipongeze serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuweza kubuni ufugaji wa samaki. Hii ni njia moja mbadala angalau kupunguza wavuvi wa bahari, lakini katika ufugaji wa samaki aliyekuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Said Ali Mbarouk tulitembelea tarehe 17/02/2012 sehemu za wafugaji wa samaki lakini bado hakujawa na utaalumu wa kutosha. Kama mimi mvuvi niliyekwenda kuona samaki wale wanaofugwa na kusema kuwa utamuondoshea mtu umasikini bado kabisa, tunamuomba Mhe. Waziri wetu mpya ajitahidi pamoja na Idara ya Uvuvi kuelimisha zaidi wafugaji wa samaki. Mtu huwa anakadiria na kukwambia nina samaki elfu moja humu kumbe hawapo magengeu matatu hayazidi, lazima tuangalie.

Halafu Mhe. Spika, pametajwa hapa Mradi wa *MACEMP*. Mradi huu umekusudiwa kuwanyanyua wavuvi, lakini wavuvi hasa hauwafikii msaada huo, kuna vikundi vichache tu vya

ujanjaujanja ndio wanaopewa wavuvi hasa hauwafikii. Tunaiomba wizara kupitia Waziri wetu aliangalie hilo na walengwa wapate haki zao.

Mhe. Spika, Waziri aliyepita alitoa ahadi katika kikundi cha wafugaji samaki Kuungoni kuwa atawasaidia bwawa moja, lakini mpaka nazungumza hapa leo na ndio bajeti ilipita hakuna chochote kilichofanikishwa. Mhe. Waziri tunataka utapokuja hapa utueleze.

Vile vile ndani ya Jimbo hilo la Kojani alitoa ahadi kwa mfugaji Kisiwani Kojani kumsaidia shilingi lako saba kwa kujiendeleza anafuga samaki sehemu ya Kipaata Kijiwebanda kisiwani Kojani. Mhe. Waziri utueleze kwa sababu mambo yote yako ofisini kwako.

Vile vile katika ufugaji wa wanyama alitoa ahadi katika ufugaji wa mbuzi Kijekani kuwasaidia dume wa mbuzi mpaka leo watu wale hawajapata. Mhe. Waziri tunakusubiri hapa utueleze. Naona Mhe. Spika, unaangalia muda wako na mimi sitaki kukuudhi. Kwa haya machache nakushukuru sana na mimi sitounga mkono hoja mpaka nitakapopata maelezo mazuri ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kupata fursa hii kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mhe. Spika, mimi nianze na suala la mifugo na nianze kwa masikitiko kabisa. Kwa sababu ninachokifahamu mimi Mhe. Spika, ili ufuge maana yake uwe na shamba la kufugia, sasa masikitiko yangu yanayokuja ni katika suala zima la mashamba ya kufugia kutokana na mambo yaliyojitokeza, sasa nabakia kujiuliza hii mifugo hatima yake tutaifuga wapi, tutaifuga barabarani. Ndio maana naumiza kichwa na napata tabu katika hili na kuanza kupiga kelele sana kuwa mifugo inazagaa mjini barabarani, jibu lake nafikiri linajitokeza kutokana na hali hii. Inaonekana kwamba labda hayo mashamba yenyewe hayapo, na ndio maana watu wanaamua kufuga mifugo mjini.

Mhe. Spika, sababu ya kusema hivyo mimi nataka Mhe. Waziri atapokuja anieleze tuna mashamba yetu ya mifugo ambayo yako rasmi likiwemo shamba la Tunguu na Kitumba; ambalo lina wafugaji wa mbuzi na kondoo. Shamba la Tunguu la Mifugo ambalo lilikuwa lina ukubwa usiopungua hekta 10,500. Inasemekana kwamba kuna wajanga walio wachache shamba hili wamelichukua, sasa sijui kama washapimiwa naomba Mhe. Waziri atapokuja anisaidie hizi hekta karibu elfu moja za Tunguu zimechukuliwa na nani, na anieleze aliyepewa amepewa kwa misingi gani.

Mhe. Spika, baada ya hilo pia nataka Mhe. Waziri atapokuja anisaidie shamba la Kitumba la ufugaji wa mbuzi na kondoo. Mhe. Spika, shamba hili nalo linaonekana tayari limeanza kuvamiwa na wananchi kwa kujenga makaazi ya kudumu na kuanza kupanda miti ya kudumu. Nataka Mhe. Waziri atapokuja hapa anielezee hasa jitihada za serikali au wizara zilizochukuliwa katika kunusuru shamba lile, na ni nani hasa aliyechukua hatua ya kuvamia, na wizara ina mikakati gani ya kurejesha ile ardhi ambayo tuliikusudia kwa lengo la kuweka mifugo yetu.

Mhe. Spika, naomba niendeleo na leo kwa upande wangu ni masikitiko tu katika wizara hii. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri tulikuwa na kiwanda chetu cha Chakula cha Mifugo pale Maruhubi, kiwanda kile serikali yetu kwa nia njema tu iliamua kumpa mwekezaji, lakini cha kusikitisha ni kwamba kinachoonekana lengo na dhamira ya serikali kutoka kwa mwekezaji

haijafikiwa, kiwanda kile sasa hivi kimekuwa ni *go down* la kuweka bidhaa mbali mbali. Ukiachilia na kiwanda cheneyewe lakini pia serikali ilikuwa na kiwanda cha kutotoa vifaranga kwa bahati nzuri Mhe. Waziri wa Elimu hili analifahamu vizuri sana, kwa sababu alikuwa mtetezi mkubwa wa kukianzisha kiwanda hiki, na kiwanda hiki cha kutotoa vifaranga pale Kizimbani kimetumia gharama kubwa sana, pesa nyingi za walipa kodi nacho pia kiwanda kile kimepewa mwekezaji.

Athari yake Mhe. Spika, kwamba sasa hivi wananchi wetu wanategemea kupata vifaranga kutoka Tanzania Bara vifaranga ambavyo vilikuwa vina gharama kubwa lakini pia vilikuwa havipati chanjo muhimu zikiwemo za gumboro, chanjo ambazo zinaathiri vifaranga na kupelekea wafugaji wetu walio wanyonge vifaranga vyao vingi kufariki na kuwarejesha nyuma baada ya kuendelea mbele. Hapa mimi nilikuwa na maombi kwa Mhe. Waziri, nimuombe Mhe. Waziri ashirikiane na Mhe. Waziri wa Fedha kujaribu kuipitia mikataba ya yule mwekezaji kuangalia hali halisi kama kuna njia za kufanya mbadala kuweza kuinusuru ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu; waweze kujiendeleza katika suala zima la mifugo ya kuku.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba nichangie katika ukurasa wa 20 Kituo cha Uzalishaji Ng'ombe kwa Sindano Maruhubi. Mhe. Spika, hapa nimuombe Mhe. Waziri hebu ajaribu kutathmini upya katika kuendeleza kituo hiki. Kwa sababu kuna malalamiko Mhe. Spika, kwamba ng'ombe wanaotumika kutoa mbegu hawana ubora, sasa na hili linapelekea kwamba mbegu zinazotumika kupandishia mifugo kwa wafugaji wetu zinakuwa hazina maendeleo yoyote. Sasa nimuombe Mhe. Waziri hapa ajaribu kufanya tathmini kwa zile mbegu wanazozitumia kwa ajili ya kutaka kupandishia hii mifugo ya wananchi wetu.

Lakini Mhe. Spika, hapa hapa napo pana masikitiko, kwamba hili eneo nalo limeanza kuvamiwa na wananchi kwa ujenzi, na wananchi hawa wanafikia pahala wanajihisi wao ndio wenye eneo lile na wao wanafikia kutaka kuchukua hatua za kuishitaki hiyo Wizara yenyewe. Sasa nataka Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kadhia ya mgogoro huu wa ardhi katika kituo cha kupandishia mbegu kwa sindano Maruhubi; hatua zilizofikiwa kwa ajili ya kunusuru eneo lile.

Mhe. Spika, nimalizie kwa Mradi wa *Kopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe*. Mhe. Spika, bado nirejee tena kwamba serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, ina nia njema sana na wananchi wetu katika kuwaondoshea umasikini. Mradi huu Mheshimiwa ulianzishwa kwa gharama kubwa sana, lakini hivi sasa mradi huu umekuwa hausikiki na hatujui maendeleo yake yamefikia wapi. Mimi Mhe. Waziri atapokuja naomba anisaidie tu, mradi huu ulianzishwa kwa gharama za kiasi gani na hivi sasa tumepata mafanikio ya aina gani katika mradi huu.

Mhe. Spika, baada ya kuchangia hayo kwa sababu najua kuna wenzangu wengi wanataka kuchangia na muda kama ulivyozungumza unakuwa ni mchache lazima tugawane baadhi ya maeneo hakuna haja ya kurejea hayo kwa hayo. Mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani nitaunga mkono hoja baada ya kupata maelezo ya kutosha kwa Mhe. Waziri. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikazungumza machache katika wizara hii ya wanyonge. Mhe. Spika, mimi kabla sijaaza kuchangia hii wizara nataka niwatoe hofu na wasiwasi wananchi wangu wa Jimbo la

Kwamtipura. Mimi bado ni Mwakilishi wao na nitaendelea kuwa Mwakilishi wao kwa kuwa wamenileta hapa kuja kuwatumikia wasiwe na wasiwasi, nitaifanya kazi hiyo kwa uadilifu mkubwa sana.

Mhe. Spika, nimeamua kusema hayo kwanza kwa sababu huko nje kuna maneno mengi, magazeti, vipeperushi na mambo mbali mbali; Hamza kafukuzwa, sijui Mshimba kafukuzwa, sasa wananchi wetu wa Chama cha Mapinduzi wasibabaike wala wasishituke. Sisi tupo na tunafanya kazi tuliyoletewa hapa na wananchi kupitia hiyo hiyo tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, hili wala lisiwatie wasi wasi.

Mhe. Spika, nimeamua niyaseme hayo kwa makusudi kwa sababu leo nimekuja na kitabu chetu hiki kinachosema Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2010 hadi mwaka 2020. Haya sio maneno yangu, haya ni maneno ya mwelekeo wa sera ya CCM.

Mhe. Spika, nataka nianze katika kitabu hiki kuna ukurasa wa 63 mpaka 72. Katika kitabu hiki chetu kinasema kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mwelekeo wa ilani yake mwaka 2010 mpaka 2020 kina mambo kimeyataja humu naomba niyanukuu kidogo kwa ruhusa yako.

Kwanza, uwezeshaji wananchi kiuchumi. Tunamshukuru Dr. Ali Mohammed Shein ameanzisha wizara hiyo na tunaendelea nayo. Lakini vile vile kumeandikwa kuna mafunzo ya uwezeshaji wa wananchi, kwa hivyo hili Mhe. Waziri baadae nitakuja kutaka ulisimamie.

Lakini jengine ni kwamba, “Ushirika kama chombo cha wananchi katika kupelekea kujitegemea”. Haya yote yamo katika mwelekeo wa CCM. Lakini vile vile vyombo vya fedha na benki za wananchi, Mhe. Waziri wa Fedha sasa hivi hayupo lakini bado ujumbe huu nitampa Mhe. Waziri ili baadae ampelekee.

Jengine linasema, “Upendeleo kwa wananchi katika ajira”. Sasa katika mwelekeo huu hii ni ya Tanzania nzima lakini kwa upande wa Zanzibar unaposema upendeleo kwa ajira ina maana kwa wananchi wanaoishi katika eneo hilo. Kwa hivyo, haya sio maneno yangu mimi, haya ni maneno ya hii sera yetu na mwelekeo wetu.

Lakini katika kitabu hiki vile vile kimeeleza changamoto, ukiangalia ukurasa wa 34, 35 na 36 kinasemaje, kwamba “Kuna haja ya kukuza matumizi ya sayansi na teknolojia katika sekta ya uvuvi na ufugaji”. Kwa hivyo, hii Mhe. Waziri baadae nitakuja kukueleza kwa vizuri kwa sababu huu bado ni muongozo wa Chama cha Mapinduzi.

Jengine katika changamoto huu mwelekeo wetu umesema kwamba, “Ukosefu wa mitaji kwa wajasiri amali kutokana na masharti magumu ya mabenki”. Hili narejea pale pale kwa Mhe. Waziri wa Fedha. Lakini vile vile katika changamoto huu mwelekeo wetu pia umesema, “Usimamizi usioridhisha wa fedha za umma”. Kwa hivyo, hii changamoto tayari imeonekana na hili kama sisi ni Waheshimiwa tena Wawakilishi tulioletwa hapa na chama chetu, hili tunatakiwa lazima tulisimamie.

Mwisho kabisa wa kunukuu nataka niseme kwamba inasema, “Udhaifu wa uongozi na ubadhirifu wa mali za umma na fedha katika vyama vya ushirika”. Mhe. Spika, nilitaka niinukuu hii ili wale ambao wana wasiwasi tunapokuwa wakali hapa Barazani katika kusimamia matumizi ya fedha za umma, kwa hivyo wasiseme labda Mhe. Hamza mkali, Mhe. Makame Mshimba mkali, Mhe. Mtando mkali, Mhe. Ali Salum mkali na wengine, huu ndio mwelekeo wetu wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, nimeamua niyasema hayo kwa makusudi ili niweze kujenga hoja zangu katika misingi hiyo iliyowekwa na Chama cha Mapinduzi. Mhe. Spika, nataka lakini samahani katika kitabu hiki hiki ukurasa wa 87 kinasema kwamba, “Vita dhidi ya rushwa ni mkakati endelevu wa utekelezaji wa kiapo cha mwanachama wa CCM, kwamba rushwa ni adui wa haki na kwamba mwana CCM hatapokea wala kutoa rushwa”. Kwa hiyo huo ndio mwelekeo wa sera za CCM katika mwaka 2010 mpaka 2020. Sasa atakaekuwa na wasiwasi na maneno ya kitabu hiki, ina maana yeye huyo ndio ana matatizo, sio sisi ambao tunaosimamia.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nataka kwanza nimpongeze Mhe. Waziri lakini vile vile nimpe pole kwa kazi ngumu aliyopewa ya kuwasimamia walala hoi. Mhe. Spika, wizara hii ya walalahoi, mifugo wenyewe walala hoi, uvuvi walalahoi. Mhe. Spika, nataka nianze mwenzangu mvuvi kutoka Kojani na hii ndio faida, Mhe. Spika, siku zote anasema Baraza la Wawakilishi halitakiwi liwe na watu wenye *PhD* watupu humu mnatakiwa watu wenye fani tofauti, ukiacha maneno aliyoyazungumza Mheshimiwa wa Kojani, sijui nani atakaeweza kuzungumza zaidi ya yale katika suala la uvuvi. Hayo aliyoyazungumza yeye mimi nadhani ushauri wangu Mhe. Waziri atuandalie semina, mimi nimeshawahi kuhudhuria semina za Idara ya Uvuvi. Kwa hivyo awaandalie Waheshimiwa wengine wala asione tabu ili kuja kutupa taaluma ni namna gani ya kuweza kuwaendeleza wavuvi wetu hapa Zanzibar, lakini vile vile tusiharibu mazingira.

Mhe. Spika, tukitaka tusitake kisiwa chetu hakiongezeki lakini Wazanzibari tunaongezeka kila siku, Wazanzibari wazaliwa na wageni na sote tunahitaji matumizi ya kutumia kitweo kutoka baharini. Sasa Mhe. Spika, ndio maana pale niliposema kwamba Mhe. Waziri wa Fedha alikuwa awepo ili atusikie, hapa ndipo inapoonekana kwamba sasa hivi ipo haja ya kuanzisha benki ya maendeleo; aidha kama itaitwa ya ushirika au ya nini. Katika miradi hii ya uvuvi tumeshakuwa na miradi mingi, kuna miradi ya *PADEP* imeanza muda mrefu sana, lakini hebu tuangalie faida inayopatikana katika miradi ya *PADEP* je, ndio ile iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, wapo wananchi wetu wamepewa ng’ombe lakini huyo ng’ombe anaemfuga anaweza kumuondolea umasikini, mwananchi anafuga ng’ombe wawili sasa sisi tunavyotaka ule ufugaji umfanye mtu ajitegemee, ng’ombe wawili atajitegemea nini, si rahisi. Kwa hivyo, hapa ndio maana tukasema kwamba lazima kiwepo chombo cha fedha ambapo hata huu mwelekeo wetu wa sera za CCM umeeleza, kuwe na vyombo vya fedha kwa sababu masharti ya benki yanakuwa ni magumu.

Mhe. Spika, ukianzisha benki kwanza hii benki wanafanya kama *revolving fund*, lakini leo utakuta wananchi wetu wanapewa misaada kupitia *SACCOS*, sijui *PADEP*, kupitia Mfuko wa AK na JK, lakini bado fedha hizi zinakuwa haziwasaidii sana. Kwa sababu mfano umeshampa shilingi milioni moja au mbili ile anabakia nayo kwake, lakini kama kutakuwa kuna benki ina

maana fedha ile anakwenda anachukua benki anafanya shughuli zake kile anachozalisha anarejesha. Kwa hivyo, inakuwa ile pesa anaizungusha ili akiirejesha kuna wengine wanakuja kuchukua.

Mhe. Spika, bila ya hivyo itakuwa siku zote hapa tunakuja kupiga stori, bado wananchi wetu hatujaweza kuwakomboa. Sasa hapa katika suala zima la uvuvi mimi nimeshaona mpaka *film* ambazo tulioneshwa jinsi matumbawe yanavyoharibika baharini, kama mwenzangu hapa kazungumza wale wanaokwenda na umangu, miwani ile ya baharini, sasa pweza anapokuwepo mbali au samaki inabidi sasa upangue lile pango ili uweze kumvuta. Lakini vile vile wao wenyewe watu wa pwani kwa sababu na mimi nimeshawahi kuchokoa pweza na mimi mtu wa pwani vile vile. Mhe. Spika, mimi nina asili nyingi, Mhe. Spika, mimi asili yangu *original* nimetokea Makunduchi, wazee wangu wamehamia Chaani na Pwani Mchangani. Sasa mimi nishawahi kuchokoa pweza kwa umangu Pwani Mchangani na wala nilikuwa sijui kama ninaharibu matumbawe au vipi, mimi samaki nishapiga kwa mshare chini ya bahari hivi unavyoniona.

Mhe. Spika, iko haja kutokana na matumizi makubwa na mahitaji makubwa ya samaki na pweza lazima serikali yetu sasa hivi tuhakikishe kwamba tunaleta boti ambazo zina uwezo wa kwenda nje zaidi kama alivyosema Mheshimiwa. Ukiangalia haya maeneo yaliyokuwa maeneo tengefu yanawekwa kwa dhamira nzuri ili wale samaki wakue halafu baadae wafunguliwe wananchi wakavue. Lakini je, wananchi wetu watasubiri mpaka samaki weshakua ndio wende baharini? Mimi nadhani Mhe. Spika, tulipokwenda China na namuomba sana Mhe. Waziri afanye ziara rasmi kwenda China. China walivyotwambia hii sekta ya uvuvi kama mtaweza kujitahidi yaani itakuwa baada ya hiyo karafuu mnayoitegemea itakuwa sekta ya pili ni uvuvi. Mhe. Waziri naomba chukua muda nenda zako China piga wiki nzima wala usiwe na haraka ya kurudi. Wewe ikisha bajeti hapa hii bajeti tutakupitishia kwanza pesa zenyewe huna humu, hii bajeti yako tupu huna kitu, nenda zako China kaangalie ufundishwe ni namna gani vya kuweza kufanya.

Wenzetu China Mhe. Spika, kila taasisi ina benki yake, kuna benki ya kilimo, benki ya uvuvi, benki ya ushirika, kuna benki ya ufugaji, kila taasisi na benki yake. Sisi mpaka leo hatuna hata benki moja ya kuwashughulikia hawa wajasiriamali. Kwa maana hiyo ndio mimi bado narejea tena, kwa upande wetu serikali na mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha bajeti ya mwakani nitalisimamia ili tuhakikishe serikali inaanzisha mtaji wa kuanzisha benki ya maendeleo mbayo hawa wavuvi na wawekezaji wengine wataweza kujikomboa.

Jengine Mhe. Spika, samaki hivi sasa huko baharini Zanzibar kuna samaki washaota mvi ndio, hawajavuliwa, samaki Zanzibar washaota mvi hawajavuliwa mwisho hapo mtu anakwenda keshona wimbi kubwa anarudi na kingarawa chake, kapigwa makofi na wimbi anarudi, ukivuka tu pale mimi hapo kwetu Pwani Mchangani pale sehemu ya kwenye wimbi pale ukivuka tu pale unamkuta samaki anaandea mkongojo. Kwa sababu wananchi wetu hawana zana, sasa Mhe. Spika hebu tulettee mambo, naamini ukienda China sasa hivi China wana mikutano, na sijui kwa nini hujenda katika Mkutano wa Viongozi wa Kiafrika kule China.

Juzi wenzako walikuweco kule wanapanga mipango namna gani China kuisaidia Afrika kujikomboa kiuchumi, Mheshimiwa mikutano kama hii uwe anakwenda wale wenzetu wako rahisi sasa hivi kuweza kutusaidia sisi Afrika.

Mhe. Spika, tukiweza kupata vyombo ambavyo vinakwenda bahari kuu samaki hawatoibiwa tena, leo samaki wetu wanafika mpaka kuja kuibiwa, ile meli ya Magufuli wale samaki hawakuibiwa Bara bwana wale samaki wameibiwa Zanzibar. Kwa sababu sisi tunaogopa kwenda, Mheshimiwa samaki mmoja mvuvi akimvua samaki huyo mmoja tu kwa siku basi tayari keshaweza kujitegemea kwa mwezi mzima, lakini nani ana uwezo wa kwenda kule. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri ili samaki hawa vizee kule baharini wapate kuondoka lazima tupate zana za kwenda bahari kuu.

Lakini jengine Mhe. Spika, nataka nije katika mgogoro wa Marumbi, naomba sana Mheshimiwa mgogoro wa Marumbi mdogo tena mdogo sana, ndio yale aliyozungumza mwenzangu kwamba wamechukuliwa vifaa vyao kwa bahati mbaya vikachomwa moto wao wenyewe mpaka sasa hivi hawana zana za kufanyia kazi, mtu ataishi vipi. Mhe. Waziri naomba andaa mazingira kawatafutie boti kama tatu tu na nyavu zao, wale vijana weshatulua wananchi wetu. Mhe. Spika pahala pakiwa na matatizo ya njaa hakuna lugha yoyote itayoweza kusikilizwa, naomba wenzangu wameshauzungumza mgogoro huo naomba na wewe ufuatilie ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu na wao tunawawezesha kiuchumi vile vile.

Jengine pameelezwa hapa kwamba kuna mashamba ambayo amepewa ndugu yetu Al-youssouf. Mimi nakubaliana lakini Mhe. Spika, bado naomba, serikali yetu lazima ihakikishe inawawezesha wananchi na itoe elimu kwa wananchi ili kuwawezesha kufuga katika ufugaji unaotakiwa, wafugaji wetu wanafuga bila ya taaluma ya kutosha, kuku wanaofuga wao kwa sababu wenzetu mahoteli wanataka kuku kuanzia kilo moja na nusu kwenda kilo mbili, sasa kwa sababu wafugaji wetu hawana taaluma ya kutosha wanakuwa hawawezi kutimiza hizo kilo. Lakini soko la kuku hapa Mhe. Spika, lipo kubwa.

Mhe. Waziri kaeleza hapa, Sekta ya Mifugo anasema ukurasa wa nne kuwa hivi sasa imeweza kutoa ajira kwa kaya 34,000 na inachangia asilimia 4.2. Mhe. Spika, hii kwanza hizi kaya 34,000 kama wangelikuwa wanajiwezesha kweli kweli hawa mimi nafikiri wananchi wetu wengi wangukuwa wameondokana na umasikini. Na hii kusema kwamba inachangia asilimia 4.2 bado tuna uwezo wa kuchangia hata asilimia 15 kama tutawawezesha vizuri zaidi hawa wananchi wetu.

Sasa mimi kitu ambacho nakiomba kwamba huyu ndugu yetu Al-youssouf sisi tungelimuomba yeye akawa anazalisha zaidi vifaranga. Kwa sababu wananchi wetu wengi hawana uwezo wa kuzalisha vifaranga, yeye azalishe vifaranga ili awauzie wananchi wetu, na serikali iwawezeshe ili waweze kujipunguzia umasikini, lakini leo Al-youssouf akija akifuga kuku akiuza haya hawa watu wetu watafuga nini. Mhe. Spika, haya mambo lazima twende na hali kila mmoja na uwezo wake, lakini katika kuwawezesha wananchi wa ndani basi lazima tuwajengee mazingira yaliyokuwa mazuri.

Lakini vile vile jengine Mhe. Spika, mimi sifurahi sana kuona kuku wanaletwa kwenye makontena. Mhe. Spika, tunapoleta kuku kwenye makontena kuku yule anauzwa tuseme shilingi elfu nne na mia tano, lakini mwananchi wetu mfugaji wa Zanzibar yule kuku tangu kumchukua kifaranga akamlea mpaka akakua mpaka akenda kumuza basi hiyo shilingi elfu nne na mia tano ndio ile gharama ya kumlea atauza shilingi ngapi. Sasa mimi nadhani ifike pahala katika

kuwalinda wafugaji wetu, basi ni lazima na sisi tuhakikishe kwamba tunawalinda lakini vile vile na uingizaji wa bidhaa nyengine kama hao kuku kutoka nje. Mimi nafikiri serikali iandae utaratibu kwa sababu hiyo ni sawa sawa na kulinda soko la ndani, hivyo wajaribu kuangalia kodi ambayo itawafanya na hawa wananchi wetu kuweza kuuza kuku wao vile vile.

Lakini pia naona Mhe. Waziri taaluma zaidi inahitajika kwa wafugaji wetu hasa wanaofuga kuku.

Mhe. Spika, kuna miradi mingi ya TASAF. Wananchi wetu wamepeva miradi ya ufugaji wa kuku lakini mingi ya miradi ile ukenda imekufa. Kuna watu wengine, ninajua Mhe. Spika, unataka kuniambia bado dakika 5 sawa nishasikia.

Kwa hivyo kitu nilichokuwa ninakiomba kwamba inaonesha kuwa bado taaluma kwa watu wetu inakuwa ndogo. Unakuta kuna akina mama mfano, akina mama 20 wanafuga kuku 200. Kweli tutaondoa umaskini hapo. Bado hatujaondoa umaskini. Kwa hivyo bado tunahitaji mitaji zaidi ili kila mmoja aweze kukopa benki ili aweze kujitegemea kuanzisha ule mradi ambao unaoutaka.

Lakini jengine Mhe. Spika, Mhe. Waziri andaa safari nyengine ya kwenda Botswana. Mhe. Spika, kule Botswana uchumi wao unategemea zaidi madini, karibu asilimia 70 yanategemea madini. Lakini vile vile wanategemea na Utalii kama asilimia 25, na vile vile na kuna asilimia ndogo wanategemea na ufugaji wa ng'ombe.

Mhe. Spika, Botswana kule ng'ombe hakitupwi kitu mpaka kwato zile. Sasa mimi ninadhani Mhe. Waziri kama atakwenda Botswana akaangalie sekta ya mifugo wenzetu wanafanya vipi, ninaamini Mhe. Waziri mwakani atakuja na kitu ambacho kitakuwa ni kitu kipya.

Wenzetu kule nyama ya ng'ombe inakaushwa. Mhe. Spika, nyama hiyo inatiwa katika vipaketi. Kama utapewa Mhe. Spika, utatafuna kutwa nzima. Maana yake ule utamu hawishi. Kwa hivyo, ina maana ile akiweza Mhe. Waziri kujifunza akenda na wataalamu wake, wakija wakiwafunza wananchi wetu hapa kuweza kumsarifu ng'ombe Mhe. Spika, ng'ombe mwananchi anaweza kumuza, anaweza akamchinja mwenyewe akamuza, akamkatakata akapata faida kubwa na akanunua ng'ombe mwengine. Kwa hivyo hii itawawezesha wakulima wetu vile vile kujifundisha namna kuweza kusarifu nyama ya ng'ombe vile vile.

Lakini jengine Mhe. Spika, namuomba tena akenda China akajifundishe wenzetu wa China walivyowafundisha wananchi wao kula kila kitu. Mhe. Spika, China samaki wote wanaliwa, wanyama wote wanaliwa. Sasa hivi hapa Zanzibar tunachagua ndio maana mtu analalamika. Sasa Mhe. Waziri ninataka ukenda China, ninashukuru hivi karibuni Wachina wameanza kutufundisha ninafikiri kula mwani. Sasa ile ndio hatua ya mwanzo. Njaa hapa hapana, pale Mhe. Ali Juma Shamuhuna anacheka, Donge kule yale majani yote yanaliwa. Sasa Mhe. Waziri ukenda China huko, naomba uchukue ile taaluma, wenzetu walichukua vipi hatua ya kuondoa njaa katika nchi yao.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kitu ambacho nilichokuwa ninataka kukisema, ninashukuru sana sera ya mifugo imeshapatikana anasema Mhe. Waziri, lakini sisi hatujaiona. Hili Mhe. Spika, katika

kosa moja ambalo tumelifanya ndani ya Baraza la Wawakilishi kuiruhusu serikali kuitengeneza sera yao, halafu sisi tusizione.

Mhe. Spika, sera ndio inayoongoza kutunga sheria. Sasa nilikuwa naomba pamoja na kwamba tumewaruhusu serikali sera wanaweza wakapitisha wenyewe, lakini basi angalau wakatufanyia semina hivi, alau kujua ile sera inazungumzaje ili haya aliyozungumza Mheshimiwa wa Jimbo la Kojani, kama kuna sera ya uvuvi, ina maana mule ndio tungepata kuona kuna hili linaumiza wananchi, hili tufanye hivi. Hayo ninafikiri yangeweza kuja kutusaidia zaidi huko mbele.

Lakini vile vile ninamshukuru Mhe. Waziri kwa kusema kwamba wanazifanyia marekebisha kanuni ndogo ndogo. Ni kweli kuna matatizo mengi. Kama ulivyozungumza katika kitabu chako nitakuwa sina muda wa kukisoma, lakini umesema kuna upungufu wa vifaa vya kudhibiti maradhi, uvamizi wa maeneo ya wizara yanayofanywa na wananchi. Sasa hili nilikuwa kidogo Mhe. Waziri ninataka nikuombe.

Wananchi wetu wamekosea katika eneo lako pale Maruhubi, walijenga na kwa kuwa eneo lilikuwa halitumiki wananchi wakaona wana haki ya kujenga wamejenga. Lakini utaratibu munaotaka kujenga ukuta hivi sasa, munatumia nguvu kubwa wananchi wetu mutawaumiza.

Mimi naomba kutoka katika zile nyumba zao mungeweka alau mita sita mukaweka ule ukuta, lakini leo unapokwenda kujenga kuta mita moja kutoka kwenye zile nyumba Mhe. Spika, hata upepo itakuwa hawapati na halafu hili litatuletea mgororo baina yetu sisi, wizara na wananchi. Kwa hivyo hili nilikuwa naomba Mhe. Waziri kwa heshima kubwa wananchi wamelia, wameleta barua na mimi mwenyewe nikenda. Lakini nikasema sasa Mhe. Waziri msikivu atakusikieni kilio chenu, na ninaamini atakapokuja kufanya majumuisho atatolea jawabu ambayo itakayokuwa ni nzuri.

Mhe. Spika: Muda umemalizika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa kuwa muda umemalizika baada ya hayo machache ninataka niunge mkono, na ninaunga mkono zaidi kwa sababu hii Wizara imo ndani ya mwelekeo wa sera za CCM katika miaka 2010 – 2020. Ninakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi kuweza kuchangia bajeti hii ya Mifugo na Uvuvi.

Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuniwezesha kufika hapa kuweza kuchangia bajeti hii, pamoja na kumshukuru Mhe. Spika, pamoja na Mhe. Waziri kwa shughuli kubwa walizopewa ili kuongoza shughuli hizi za uvuvi pamoja na wakulima.

Zaidi ya hayo nizungumzie kuhusu masuala ya mwani. Uvuvi wa mwani kwa kweli hivi sasa Mhe. Spika, Mhe. Waziri hajaupa uzito zaidi hasa kuwashughulikia wakulima wetu ili kuwapatia nyenzo za kuweza kulima mwani mwingi ili kuwapatia faraja na fedha nyingi za kigeni na uwezo huu ulikuwepo. Lakini Mhe. Waziri bado hajalichangamkia suala hili hasa kuwatafutia masoko ya kisasa; ambapo hivi sasa nchi nyingi zinapendelea kupata mwani kwa shughuli zake za matibabu, chakula pamoja na supu na vilaji vyengine.

Nchi nyingi duniani hivi sasa zinahitaji mwani lakini utashangaa kwamba bado mwani haujapata soko zuri wala bei nzuri. Hakuna hata sehemu moja ukisikia kinafikia shilingi mia tatu. Kitu cha mwanzo kilichokuwa na bei mbaya ni mwani. Hakuna kilo ya kitu chochote duniani inayoanzia shilingi mia tatu isipokuwa mwani peke yake. Sijui Mhe. Waziri hili amelifikisha wapi na atanieleza nini atakapokuja; kwamba suala hili hajalipatia ufumbuzi kuweza kupata bei nzuri ya mwani.

Kama yeye mwenyewe Mhe. Waziri Mhe. Spika, imeshindikana sisi Wawakilishi wa majimbo tunao uwezo wa kutafuta hii nafasi, basi atupe nafasi. Amepangiwa kwenda China, Japan na wapi lakini kama hajapata nafasi hii ya kwenda katika sehemu hizo, atoe uwezo kwa Wawakilishi wa majimbo tunaweza kutafuta nafasi hizi na uwezo huu upo, hizo nafasi za kwenda yeye wacha twende sisi Wawakilishi wa majimbo.

Hapa Mhe. Waziri naomba anisaidie kuhusu mambo ya uvuvi. Hivi sasa tunazo sehemu nyingi za uvuvi lakini utakuta sehemu zetu hazina vioti vya kuvulia sehemu zinazohitajika na huko ndiko kwenye samaki wengi. Kwa kweli Mhe. Spika, ingelifaa utuhakikishie au utwambie kwa nini katika majimbo yetu hatujapata boti za kisasa kwa ajili ya kuwasaidia wajasiri amali wetu kuweza kwenda kufanya uvuvi sehemu hizi husika, na bado wanapata matatizo ya kukamatwa na nyavu ndogo kwa sababu hawana uwezo wa kwenda katika sehemu kubwa za kuweza kufika kuweza kuvua.

Hiyo kusema kweli wanakamatwa, mimi ninasema wao hawana makosa, makosa ni wewe Mhe. Waziri kwamba huwapatii vifaa vya kisasa kuweza kufika sehemu waliko samaki. Utakuta kila siku wavuvi wetu wanapata matatizo ya kutiwa ndani na kupata hatia ya kushtakiwa kwa sababu wanakwenda katika sehemu ndogo, na sehemu hizo hazizuii zile nyavu kubwa, inabidi uende na nyavu zenye macho madogo na hapo ndipo wanapopata matatizo.

Kwa hivyo ukweli Mhe. Waziri unieleze sababu kwamba wavuvi wetu wanapata matatizo, ninahisi hapa Mhe. Waziri wizara yako ndio inayosababisha hasa wakulima wetu au wavuvi wetu kuweza kupata matatizo. Ipo haja ukifika unieleze ni lini utaweza kutupatia boti za kisasa hasa katika majimbo yetu, hasa kwenye Jimbo langu la Koani ambalo lina bahari kubwa sana katika sehemu ya Ghuba.

Mhe. Spika, kuhusu masuala ya kufanyiwa *repair* majosho yetu ya ng'ombe. Hivi sasa majosho mengi ya ng'ombe yamekufa hasa ukitazama Hanyegwamchana ilikuwa ni sehemu kubwa sana ya kuoshea ng'ombe, au Tunguu ilikuwa vile vile ni sehemu kubwa ya kuoshea ng'ombe au sehemu za Dunga hadi Binguni. Hivi sasa sehemu hizi zimekufa zimesababishwa ukitazama ni wewe Mhe. Waziri kuttoa kipaumbele suala hili ili kuhakikisha kwamba wafugaji unawahudumia vizuri. Kwa hivyo Mhe. Waziri ipo haja kuhakikisha katika sehemu kutuhakikishia ni lini majosho ya ng'ombe yatafanyiwa *repair* safi na kurudi kama hadhi yake yalivyokuwa.

Mhe. Spika, hapo hapo ipo haja kuhakikisha katika mifugo hiyo tunajitahidi sana kufuga kuku. Lakini utakuta tulikuwa na viwanda vya vyakula cha kuku na hadi leo hatujui kiwanda kile kimeishia vipi. Wafugaji wengi wanapata matatizo. Utakuta kila mfugaji mpaka ahakikishe

kwamba anaagiza chakula kutoka Bara. Hajui chakula kile kinatengenezwa vizuri au kinatengenezwa vipi, lakini tungekuwa na viwanda vyetu vya kuhakikisha vinatengeneza chakula cha kuku, ni wazi kwamba mfugaji angelikwenda mwenyewe kuhakikisha chakula kile kinafanya vipi, kinatiwa madini yale yanayotakiwa, kinatiwa dawa zinazotakiwa au vitu vyengine.

Lakini utakuta mfugaji anafuga kuku lakini chakula kile hakijui kinavyotengenezwa. Suala hili naona Mhe. Waziri ulipe kipaumbele kwamba wafugaji wetu wanapata hasara. Utakuta kuku wengi mtu anafuga lakini mwisho wake ni kufa au kudumaa hawazalishi vizuri. Hili ninafikiri Mhe. Waziri ulipe kipaumbele kwamba wafugaji wetu wanapata matatizo sana katika ufugaji hawafiki katika kupata ufugaji wa kileo. Ndio utakuta hata kuku naye anashindwa kuzalishwa Zanzibar mpaka atoke nchi za nje kabisa, na uwezo huo tunao hata tusingelikula kuku ambao hawaeleweki wanatoka wapi, kuku wale pengine wamekufa wamechinjwa sijui upimaji wake uko vipi. Hata Wizara ya Afya haituhakikishii kwamba kuku wale wanapimwa vipi, sisi tunakula tu.

Lakini wangelikuwa wanafugwa hapa Zanzibar tungelikuwa tunakuta kuku ambapo tungekuta kuku yule *original* kachinjwa leo na kaliwa leo, lakini unakuta kuku amechinjwa zaidi ya mwaka mmoja ndio mlaji anakula, ndio matatizo yake tunapata matatizo ya figo na kila aina katika matumbo yetu kwa sababu wazi tunakula chakula hatuelewi kimekaa muda gani.

Mhe. Spika, zaidi ya hayo ninaweza kusema kwamba uzalishaji wa samaki kuweza kwamba tuwe na viwanda vya kuweka barafu, tuhakikishe viwanda vile viwepo katika maeneo ya majimbo. Kwa sababu utakuta mvuvi anavua samaki inabidi amuuze kwa bei ya hasara kwa sababu samaki yule ikifika kesho hajui amuweke wapi, matatizo yale utajua kwamba samaki wale ikifika masaa matano au sita wanaharibika kabisa ni hasara kwa wavuvi wetu.

Utakuta Mhe. Spika, tunakopa vitu vingi vya uvuvi kwa ajili tuvua na halafu tupate faida. Lakini utakuta kwamba mtu akishapata samaki ikifika saa moja samaki yule amuuze kwa bei yoyote hata kilo moja kwa shilingi mia tatu, au amkate kipande kwa shilingi mia mbili. Wakati samaki yule alikuwa na uwezo wa kumuuzwa kwa shilingi elfu kumi, utakuta mvuvi anapata shilingi elfu tatu.

Hilo naona Mhe. Waziri uhakikishe kwamba kila jimbo au kila mkoa tuhakikishe tuwe na kiwanda cha barafu ili wavuvi wetu wapate kuvua uvuvi bora, na wanauza samaki kwa wakati na kupata faida, angalau kupata chakula kinachostahili kwa milo ya siku zote.

Vile vile wafugaji wetu wana matatizo, utakuta mfugaji ana ng'ombe zaidi ya ishirini. Katika ng'ombe ishirini kwa siku haiwezekani ng'ombe wale kwa siku asipate maradhi angalau ng'ombe hata mmoja. Lakini hajui ampeleke kitu cha wapi. Anakwenda umbali wa meli kutafuta kituo cha hospitali cha kuweza kutibu wanyama, na ukenda kule utakuta kwamba kituo hicho hakina dawa na daktari. Kwa hivyo ipo haja wapatiwe vijana wetu masomo wazalishaji mali, ili waweze kuwemo katika majimbo kuweza kuweka vituo vidogo vidogo vya matibabu ya wanyama. Mpaka utakuta katika jimbo langu ukitoka zako Tunguu hupati tena kituo chengine cha ufugaji wa ng'ombe hadi unafika Uzi Ng'ambwa. Mtu atoke na ng'ombe wake hadi Uzi Ng'ambwa ende Tunguu kufuatilia daktari, au aombe daktari kutoka mjini. Kwa hivyo tuna

matatizo ya kupata vituo vya ufugaji ili kupata matibabu kwa wakati hasa kwa wafugaji ng'ombe.

Mhe. Spika, kwa haya yote ninataka Mhe. Waziri aje aniambie ni lini katika jimbo langu kutajengwa kituo cha kisasa cha ufugaji wa ng'ombe; hasa sehemu za Tunguu hadi kufikia Uzi Ng'ambwa.

Kwa hayo machache sina zaidi, ninaunga mkono hoja asilimia mia. Ahsante sana.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kumshukuru Allah kutuwezesha tukawa wazima, na pia ninatoa shukurani zangu kwako mchana huu kuweza kunipatia na mimi nafasi ya kutoa mawazo yangu katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, mimi ninapenda nianze ukurasa wa 27 ibara ya 6 pale, Idara ya Huduma za Utibabu wa Wanyama. Mhe. Spika, nianze kwa kuuliza swali. Ninadhani kwamba sheria hii ya kuwalinda wanyama ipo muda mrefu si chini ya miaka 10 hivi. Jee, ni wafugaji wangapi wanaowatesa wanyama mateso makali wakafikishwa mahakamani na wakaweza kuhukumiwa.

Mhe. Spika, wanyama wanaopata mateso zaidi hapa Zanzibar ni ng'ombe na punda. Mhe. Spika, nikisema hivyo ninataka nitoe visa viwili vitatu katika wanyama hao. Kimoja nimekishuhudia kwa macho yangu, na viwili vimetokea na vimetokea vya kweli katika kuvipokea kwangu.

Kwanza ni mzee mmoja wa shamba huku alikuwa anafuga punda wake na alikuwa anampenda sana. Lakini huyu punda alimuasi kiasi fulani bwana wake akaanza kutafunatafuna, kwa hivyo akaamuru kumuua. Kwa bahati eneo alilomuuzia ni hapa Mwembe Makumbi. Katika Zanzibar eneo linalotesa wanyama hili ni namba moja.

Punda yule baada ya kuuzwa pale Mhe. Spika, kwa muda wa siku tatu alipata kipigo cha mbwa mgeni. Akashindwa hata kufanya safari ya kutembea. Mabwana walipompa kisago kile wakamuachia usiku ili ajitafutie huduma za maisha. Lakini punda huyu Mhe. Spika, usiku ule alifanya safari ya kurudi shamba kwa bwana wake.

Alifika kwao asubuhi saa mbili. Bahati njema bwana aliyekuwa anayemiliki huyu punda alikuwa yupo barazani pake amekaa. Kufika pale punda yule alikwenda kuweka kichwa chake kwenye mapaja ya bwana wake, akalia sana punda yule, akatoka machozi sana. Lakini bwana mkubwa kumuungalia punda jinsi alivyo hata ule unyoya hana, amebabuka mwili mzima kwa kupigwa marungu.

Kilio cha punda na bwana muuza punda naye akalia Mhe. Spika. Ikawa ni jambo la kusikitisha sana na akasema watakapokuja hawa wanunuzi basi ninawarejeshea pesa zao, yametosha. Kwa hivyo, hiki kilikuwa ni kipigo kikubwa sana cha huyu punda na haya mambo bado yanaendelea.

La pili mimi binafsi nililoliona, nilikuwa maeneo ya Bububu akapita punda na vijana wanne wamepanda kwenye ile gari ya punda. Lakini punda yule anaendelea na kisago na kipigo. Kufika Mshelishelini pale yule punda alilala, akashindwa kutembea. Kufika kwake kutembea yupo kati

kati ya barabara, na njia ya Bububu tunaifahamu kwamba mapishano ya gari ni mengi lakini wakafanya jambo moja la busara kweli kweli.

Yule punda baada ya kulala, sasa ikabidi wakambeba wakampachika ndani ya ile gari, sasa wakawa wao wanamvuta yule punda. Kidogo akapata huduma hapo kwa sababu watu walikuwa wengi na wakaona tutakalofanya lolote hapa, hawa hawatokubali tutakalolifanya. Kwa hivyo punda na yeye akapakiwa kwenye gari sasa, sasa wale wakaanza kumburura punda wakampeleka walikomtoa.

Kwa kweli Mhe. Spika, haya ni matatizo. Hawa ni viumbe tunatakiwa wawe ni wasaidizi wetu. Lakini na kisa kimoja kilichotokea Pemba pale Chake-Chake. Kulikuwa kuna bwana anachunga ng'ombe, sasa sijui huyu ng'ombe walikosana nini, akaamuru achinjwe yule ng'ombe. Sasa ng'ombe huyu alipoyaona yale alikata ile kamba akapiga mbio mpaka Makao Makuu ya Polisi Madungu. Alifikiri atakapofika pale huenda akapata usalama. Mabwana wa ng'ombe wakamtafuta wakaambiwa bwana ng'ombe wenu yupo Polisi kenda kushtaki.

Lakini bahati mbaya Mhe. Spika, huruma kwa wanyama hapana. Walipokuja wenyewe wakapewa ng'ombe wao wakamchukua huyo wakenda kumfanya walivyokwenda kumfanya. Lakini kama ingekuwa idara inafanya kazi, huyu alikuwa si ng'ombe tena wa kuchinjwa. Ni ng'ombe wa kufanyiwa utafiti ikajulikana kuna kosa gani walifanya hawa watu mpaka huyu mnyama akaja hapa Makao Makuu ya Polisi kuleta mashtaka yake.

Kwa hivyo Mhe. Spika, idara hii ina mpango wa kutaka kupitishiwa pesa ili iweze kufanya kazi zake vizuri. Lakini la kusikitisha Mhe. Spika, kuna matokeo kama hayo na ninadhani kuna wenzangu wanajua matokeo mengine mbali mbali hapa. Kwa hivyo ningelimumba sana Mhe. Waziri aje atupe jawabu au anipe idadi ya kesi ngapi walizopandishwa watu mahakamani na kuweza kuhukumiwa, kwa sababu Zanzibar tunaendelea kuwatesa wanyama vibaya.

Mhe. Spika, ukimuona ng'ombe jinsi alivyopakiwa, siku hizi wajenzi ni wengi, punda au ng'ombe anapachikwa matofali karibu hamsini na sitini, na tofali tunalijua uzito wake ulionao. Kutokana na hali ya maisha mtu anataka gari yake moja ile ya ng'ombe anayochukua aweze kukimu maisha yake. Lakini jee, huyu mnyama akiteseka akipata kuumwa, ule msaada unaotafuta utaupata. Kwa kweli hili ni tatizo. Namuomba sana Mhe. Waziri Mhe. Spika, aje anielimishe hapa kwa kiasi fulani.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika ibara ya 7 kwenye Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ukurasa wa 34 pale. Mhe. Spika, hapa naomba ninukuu kifungu 71 (g), kinasema kwamba kusimamia soko la kisasa Tumbe.

Mhe. Spika, kwanza sina budi kuipongeza serikali kuweza kutujengea soko la kisasa katika eneo letu la Tumbe. Waheshimiwa kutokana na kauli hiyo ya kujengewa soko la kisasa, ni neema moja kubwa ambayo wananchi wa Tumbe na maeneo mengine ya Pemba wanaweza wakapata ajira mbali mbali kutokana na fani za watu walizonazo.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo lakini kuna mambo kiasi fulani yanaweza kulifanya lile soko lisiwe la kisasa. Kwa sababu unapotangaza kuwa una soko la kisasa, ina maana umekamilisha

huduma za soko na unaweza kuwavutia watu wa maeneo mbali mbali na nchi mbali mbali kuja kuwekeza pale katika soko lako.

Lakini la kusikitisha Mhe. Spika, kuna mambo mengi katika soko hili la kisasa, tayari serikali wameshayatengua na ni mambo muhimu ninavyoona mimi. Moja majengo mawili ya dago. Wewe unatangaza soko la kisasa kuwavutia watu waje wawekeze, waje dago lakini wapi utamuweka dago. Ukiondosha majengo mawili. Huyu dago unakwenda kumuweka wapi.

Kwa hivyo alipokuwa hana pa kukaa dago, unataka kumfanya sasa ahamie katika kijiji. Akihamia katika kijiji hakuna usalama kwa dago. Kwa hivyo kuondosha mabanda mawili haya ya dago hili soko unalivunjia hadhi yake. Pia jengo la choo na jiko, wakija dago pale wanahitaji kujisaidia, wanahitaji kupika, lakini mambo hayo ukiondosha itakuwaje. Hizi huduma za dago atazifanya wapi.

Lakini pia ilikuwa soko lile lijengwe sehemu ya kuanikia mwani. Kama tunavyojua kwamba Tumbe kwa Zanzibar nzima inaongoza kwa suala zima la mwani. Sasa hapa sisi watu wa Tumbe tulikuwa tumeshaleta shukurani kubwa kwa serikali yetu ya awamu ya saba, kwamba na wale watu wanaofanya mwani watapata maeneo mazuri ya kuweza kuanikia mwani wao. Lakini hatimaye sehemu hii pia serikali wameifuta.

Mhe. Spika, lakini jengine ni jiko la kukaangia samaki. Mhe. Spika, unapokusanya watu wanapokwenda baharini, wakirudi wana njaa kubwa. Katika njaa mbaya wenyewe wanavyosema ni njaa mtu anayetoka baharini. Akirudi akifika juu pale anahitaji kupata huduma. Sasa wakati wamekwenda baharini bila shaka watakuwa wamepata samaki, majiko haya pia serikali imeyaondosha.

Jengine ambalo lilikuwa liwepo pale Mhe. Spika, ni *work shop* ya vyombo. Tunajua kwamba vyombo vyote vya baharini vinanunuliwa vikiwa ni vipya, baadae vinakua vikukuu halafu vinapata kuharibika. Walikuwa wavuvi wetu wakitoka pale huduma hizi za kupata vyombo viwepo pale pale kwenye hili soko. Lakini pia hili serikali wamelifuta.

Jambo jengine Mhe. Spika, ni Msikiti. Soko hili ilikuwa liwe na Msikiti ili waliopo pale na wavuvi wanaporudi kuvua waweze kutekeleza ibada. Lakini leo unaondosha ibada, na ibada ndio sehemu moja ya mwanadamu kuweza kumkumbuka Mwenyezi Mungu wake. Sasa ukiwaondoshea, unavyotaka kufanya arudi baharini, akifika pale haoni pa kusali aweze kumsahau Mungu. Kwenda kumuomba kwake Mwenyezi Mungu ampe riziki lakini akirudi asahau kumuabudu, ninadhani hata riziki pia zitakuwa zina matatizo.

Lakini jengine Mhe. Spika, ilikuwa soko lile pia iwe na kituo cha mafuta kwa wavuvi kwa sababu kutoka Tumbe hadi Konde au Tumbe hadi Wete au Chake-Chake ni mbali. Kwa hivyo ikaonekana pale pawe na kituo cha mafuta. Sasa wakati ni soko la kisasa, wavuvi wamekuja kuangalia wanataka kwenda baharini lakini mafuta hapana ni tatizo. Kumpeleka mtu Konde ni kilomita saba. Kwa hivyo kiasi fulani ni mbali. Hivyo pia hili serikali wamelifuta.

La mwisho Mhe. Spika, ni banda la mama ntilie. Hapa akina mama wa Tumbe na maeneo mengine walikuwa wapate ajira. Serikali ilikuwa na mpango wa kuwajengea akina mama hawa

ili aweze kupika pale, wavuvi wanaporudi baharini waweze kupata chochote. Kwa hivyo yote haya Mhe. Spika, yameondoshwa.

Mimi ningemuomba Mhe. Waziri aje anifahamishe kwa kina kabisa Mhe. Spika, ni lipi lililopelekea mradi huu. Ninadhani mkataba wa mwanzo ulipokuja yote haya mambo yamo. Ni lipi lililopelekea kuondoshewa kwa mambo haya ambayo ndio soko la kisasa.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije kifungu cha 8.2 (e) kwenye ukurasa wa 42. Hapa ninapenda kuipongeza kampuni ya mwani ya Bill, taasisi ya sayansi baharini ya Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam pamoja na wanajamii kwa utafiti wao walioufanya katika vijiji viwili. Ikiwa ni kijiji kimoja kwenye eneo la Tumbe na kijiji cha Fundo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba mwani huu wa *cottonii* bahari yetu hii ya Tumbe unastawi. Unakua na ni mwani ambao wananchi wanapata faida haraka. Mhe. Spika, mwani huu ndio mwani wenye tija duniani.

Lakini Mhe. Spika, tatizo kubwa la mwani huu. Huu mwani ndio chakula kikuu cha samaki wote wale wenye uwezo wa kula baharini. Mfano ni sawa sawa na Wazanzibari na wali. Hasa hapa nikitaka Mhe. Waziri katika huo utafiti uliofanyika ni utafiti wa kupanda tu na kustawi au ni utafiti mpaka wa kuunusuru mwani huu kutoliwa na samaki. Ningeliomba hapa nije nipate jawabu rasmi.

Mhe. Spika, nikiendelea na huduma hii ya mwani, wananchi wengi wa Zanzibar hasa akina mama ni wakulima wa mwani huu wa kawaida. Huu mwani umekuwa na muda mrefu, maana kama kwamba serikali haina habari na wakulima hawa. Biashara hii walipoanza walianza na shilingi mia moja mpaka wakafikia mia mbili bei kwa kilo moja.

Lakini bei hii ya shilingi mia mbili iliganda muda mrefu sana. Mhe. Spika, katika kazi moja ambayo ngumu ni kazi hii ya mwani, kwa sababu mwani ni maji. Kuuvua kule na ukaupandisha juu kwenda kuutayarisha Mhe. Spika, lile polo la kilo 50 basi unaweza kuzitia kilo 100 za mwani mbichi.

Mwani huu unahitaji kubebwa. Kwa hivyo akina mama wanashajihika sana. Mwani wa kilo 100 zile ulio mbichi hata ukishakauka basi ni kilo 10 au kilo 5 tu. Kwa hivyo akusanye kilo 5 hizo, kilo ni shilingi mia mbili kwa siku hizo za nyuma lakini kutoka hapo tumeganda na mia nne, Mhe. Mussa alisema hapa hakuna kitu chochote cha mia tatu lakini mimi ninasema mwani unanunuliwa mia nne, hakuna bei yoyote unayopata kitu ukaweza kupata maisha.

Hii bei kwa nini serikali isikae pamoja na hizi kampuni zinazonunua mwani wakaangalia faida wanayoipata ili mwananchi wetu na yeye aweze kuimarika kwa zao hili ambalo wananchi wengi hasa akina mama wanalizalisha zao hili. Kuna tatizo gani.

Mhe. Spika, mimi naona ipo faida ya mwani. Mhe. Spika, naona unatizama ninamalizia tu hapa.

Mhe. Spika: Unazo dakika 3.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante.

Alipokuja huyu mfanyabiashara akapandisha hii bei ya shilingi mia nne baadhi ya wafanyabiashara wengine walianza kulalamika. Lakini la msingi nililoliona kwamba baada ya kupandishwa haukushushwa. Kama haukushushwa ni kwamba faida ipo kubwa. Kwa hivyo kwa nini tuendeleo kubakia na shilingi mia minne hii, wananchi wetu hawa na wafanyabiashara hawa wasikae pamoja ili kumnusuru huyu mkulima. Kwa hivyo ningeliomba sana Mhe. Spika, serikali kwamba wakulima wetu wa mwani wawajali.

Mwani hivi sasa Mhe. Spika, una faida nyingi; ni chakula, sabuni na mambo mbali mbali. Kwa nini Mhe. Waziri huchukui jitihada za makusudi elimu hii ukaifikisha kwa wakulima wote wa mwani ili na wao atakapona kuwa bei niliyopewa si nzuri, basi akatafuta *swarfa* ile ya chakula, mwenyewe akawa na chakula chake akala na watoto au akafanya kitoweo akala na watoto, akafanya sabuni akaweza kufulia nguo zake na watoto. Kwa hivyo ningeleomba sana Mhe. Waziri hizi jitihada uzichukue na uzifanyie kama ni tija kwa wakulima wetu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nikapopata jawabu zangu kuhusu hili soko na mambo mengine basi sina uchoyo wa kumpa asilimia mia katika hotuba yake. Ahsante sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi alau niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, Wizara hii kwa kweli ni moja kati ya wizara muhimu sana. Ni wizara ambayo kama itafanya kazi vizuri basi ni tegemeo la uchumi wa nchi yetu na vile vile ni utekelezaji wa ile sera ya kupunguza umaskini Zanzibar; pamoja ni wizara tegemeo katika kuleta lishe kwa wananchi wa Zanzibar.

Sasa kwa umuhimu wa wizara hiyo, kwanza nitakwenda na wafanyakazi. Wizara hii ina wafanyakazi 739 ambapo kwa kweli ninathubutu kusema ni nguvu kazi ya kutosha ya kuweza kutekeleza majukumu yake.

Idadi hii ya wafanyakazi Mhe. Spika, inatakiwa ilete mafanikio na tija katika utendaji kwa sababu hawa ni wafanyakazi wengi, na tija vile vile inatakiwa ionekane kwa macho yaliyo wazi.

Kwanza Mhe. Spika, naomba nianze na umuhimu wa takwimu. Suala linalohusiana na mifugo na suala linalohusiana na uvuvi, linawahusu wavuvi na linawahusu wafugaji pamoja na vinavyofugwa kwa upande wa uvuvi. Kwa msingi huo suala la takwimu katika wizara hii ni kitu cha msingi sana, kwa sababu takwimu ndio itakayopelekea ile *allocation of fund*, hizi fedha na mipango mingi, kama tunapata wahisani na tunapata misaada mbali mbali, tutakapokuwa na takwimu, ndio itatuwezesha kuelekeza mambo haya katika sehemu zinazohusika. Bila ya takwimu tutakuwa tunafanya mambo bila ya kujua tunafanya nini na mwisho wa siku hatuwezi kupata tija ya aina yoyote. Kwa hivyo, hili amelizungumzia Mhe. Waziri katika ukurasa wa 12, kwenye kipengele kidogo cha 3(3) kwamba ukusanyaji wa takwimu unakwenda vizuri. Lakini namuomba Mhe. Waziri katika suala hili la takwimu basi asiishie kuzifanyia kazi yeye tu katika ofisi yake. Ikiwezekana wawakilishi wa wananchi na sisi tuzipate takwimu hizi, ili tuweze kushirikiana naye katika kuendeleza masuala ya uvuvi pamoja na mifugo katika nchi yetu.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala la takwimu lisiishie katika ofisi yake, bali lienee kwa wawakilishi wote ili tuweze kujua tunafanya nini, tunapanga nini na kwa wakati gani.

La pili Mhe. Spika, naomba nizungumzie suala la uvuvi wa bahari kuu. Nchi yetu Zanzibar ni visiwa na kwa kuwa ni visiwa vilivyozungukwa na bahari, rasilimali yetu kubwa ni bahari iliyotuzunguka. Zanzibar hatuna ardhi ya kutosha, bahari ndio ardhi yetu, bahari ndio rasilimali yetu na bahari ndio mgodi wetu. Kwa hivyo, ni vyema tukaitumia vizuri bahari na tuwe na mipango madhubuti na endelevu juu ya suala zima la matumizi ya bahari.

Mhe. Spika, katika kitu ambacho kinaweza kunyanyuwa uchumi wa nchi yetu kwa kipindi kifupi ni suala zima la uvuvi wa bahari kuu. Hizi kelele ambazo tunapiga Mhe. Spika, kama tungekuwa na mipango mizuri, mipango inayotabirika, mipango inayowezekana pamoja na utekelezaji juu ya uvuvi wa bahari kuu. Mimi nasema Zanzibar ndani ya kipindi kifupi hali yetu ya uchumi inaweza ikabadika kwa kipindi kifupi sana. Kadhalika kipato cha wananchi wetu kinaweza kukua katika kasi ya ajabu, lakini ninasikituika kwamba bado hatujawa na mipango ya uhakika na mipango ya ukweli juu ya matumizi bahari kuu.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma pale kaeleza, katuonesha ilani ya CCM ambapo ule ni mkataba wa chama hiki katika kipindi cha miaka mitano. Vyovyote vile suala la uvuvi wa bahari kuu litakuwa limegusiwa, kwa sababu kila mmoja anakubaliana na kwamba bahari kuu ndio suluhisho la uchumi wa nchi yetu. Kwa hivyo, tulitegemea kati ya mwaka 2010/2015 kwa vyovyote vile ilikuwa tayari ionekane kwamba sasa hivi tumeingia katika eneo hilo, sasa hivi ni mwaka 2012, keshokutwa tukijaaliwa ni mwaka 2013 na mwaka 2014/2015 itawadia Mwenyezi Mungu akipenda. Lakini haionekana kwamba kuna mipango sahihi na mipango ya ukweli na mipango madhubuti ya kuelekea kwenye uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Spika, ilielezwa katika bajeti ya mwaka jana kwamba kulikuwa na mipango kama hiyo, lakini hakukutendeka chochote. Bajeti ya mwaka huu ndio imetenga milioni 300, maana yake ni 2012/2013 Juni matumizi tutakayotumia katika uvuvi wa bahari kuu ni milioni 300, kama zitapatikana zote. Ingawa kwa kawaida haionekani kama zitapatikana zote, tuombe Mungu zipatikane zote. Hiyo imeelezewa kwamba ni ufundishaji tu wa vijana 60, sijui ni uvunjaji wa jengo la Malindi pale jengo gani sijui, sijui Tafiko pamoja na mambo mengine, bado Mhe. Spika, hatujawa *serious* katika suala hili na kama wawakilishi wa wananchi ambapo sasa hivi tunatimiza nusu ya kipindi cha miaka mitano, haturidhiki na kasi inayochukuliwa na serikali kuelekea katika uvuvi wa bahari kuu haturidhiki, kwa sababu uvuvi wa bahari kuu kwanza unahitaji miundombinu ya uvuvi wa bahari kuu, na miundombinu ya bahari kuu kwanza ni lazima tuwe na vyombo vyenye uwezo wa kwenda bahari kuu, ukiachia mbali mafunzo ni kitu cha msingi.

Lakini la pili, ni vyema tuwe na bandari, kwa sababu uvuvi wa bahari kuu hauusiani na bandari ile ya Malindi pale, abiria hapo hapo vyombo vya uvuvi hapo hapo ni vitu tofauti. Ujengaji wa masoko pamoja na maghala na vitu vyengine. Sasa hiyo ndio inayoweza kupelekea tukakamilisha suala zima la uvuvi wa bahari kuu. Nasema kwamba uvuvi wa bahari kuu unahitaji miundombinu ya uhakika ambayo ndio hiyo niliyoitaja. Kwa hivyo, inavyoonekana Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha wa 2012/2013 ku-*allocate* shilingi milioni 300 kwa ajili

ya kufundisha tu vijana hao pasi na kufikiria mambo mengine ya msingi, bado nasema serikali haijawa *serious* na suala hili, tukiwa kama wawakilishi wa wananchi, tunahitaji tuzio juhudi za serikali za dharura ili kuona kwamba tunakamilisha kipindi cha mwaka 2010/2015 tayari Zanzibar ikiwa imeingia katika uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Spika, katika hilo basi, watu wanasema ‘chuvi la vivyo latoelewa vivyo’. Basi hao vijana 60 ambao watapewa mafunzo, naomba sana watoke katika sehemu zinazohusiana na uvuvi, naomba sana. Haitofurahisha hata kidogo majimbo ambayo hayana uvuvi tukaambiwa kwamba ndio sehemu kubwa ya vijana hao walikotoka. Kila jimbo lina uchumi wa aina yake. Kwa hivyo, vijana hao 60 itafurahisha sana na itapendeza sana kwamba wanatoka katika majimbo ambayo yana uvuvi, likiwemo la Chake Chake maeneo ya Weshi, Ndagoni, Misooni na sehemu nyengine.

Suala la tatu Mhe. Spika, ni sekta ya mifugo. Kitu chengine ambacho kinaweza kikatusaidia Zanzibar katika suala la maendeleo ya uchumi na kuwaondoshea umaskini wa wananchi ni suala zima la sekta ya mifugo.

Mhe. Spika, inavyoonekana kwamba Zanzibar badala ya kwenda mbele, basi tunarudi nyuma katika suala zima la sekta ya mifugo. Tunakumbuka hapa katika miaka ile ya 1980 mpaka miaka ya 1970, tulikuwa tuna mashamba ya mifugo. Kuna shamba kama la Mtakata, kuna shamba la Chamanangwe na kuna shamba la Pageni Kipange. Mhe. Spika, mashamba haya serikali ilikuwa imewekeza mifugo, lakini leo ukenda Chamanangwe hakuna kitu, ukenda Mtakata hapana kitu na ukenda sehemu nyengine hapana kitu. Tuisahau suala la Makurunge ambalo hii ni mada ya muda mrefu sana. Tulipewa shamba tukalidharau watu wameanza kulichukua.

Mwelekeo au matumaini ya wananchi ni kwamba tuwe na mifugo, serikali iandae utaratibu wa kuwa mifugo ambayo tutaweza kupata mifugo hiyo na mazao yatokanayo na mifugo kukidhi katika soko la ndani. Leo ni aibu kwamba tunaagizia mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi yetu, kanakwamba Zanzibar hakuna wafugaji. Tunaagiza kuku kutoka Mabara ya mbali, kuku ambao hata ukiwatia mdomoni hawana ladha yoyote. Ramadhan hii na skukuu mayai tunaagizia nchi jirani, kitu ambacho wafugaji wa hapa kuna uwezekano kabisa, ni aibu kwa kweli, Zanzibar leo kuagiza mayai kutoka Kenya au kuagiza mayai kutoka Bara kama hapa hakuna watu wanaoweza kufuga.

Mhe. Spika, naomba katika hili serikali ikae kitako ijirudi kwenye suala hili na lazima tufike pahala masuala haya tuone kwamba tuna uwezo Wazanzibari wenyewe kuzalisha na kulikidhi soko la ndani na ikiwezekana kuuza nje ya nchi. Wazanzibari wapo wafugaji wazuri tu. Lakini kwa kweli tumekosa baadhi ya mambo kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan. Mhe. Spika, huwezi kuwa na mfugaji kama hujamuelimisha, huwezi kuwa na mfugaji kama hujamuezesha ili afuge. Hili linawezekana, tatizo letu ni nini.

Mhe. Spika, naomba serikali ikae kitako. Kwa sababu tunasema sasa tunataka kuondosha maneno haya, wakati wa kupiga maneno mengi umekwisha, sasa ni wakati wa vitendo, twende kwenye vitendo, ‘linalowezekana leo lifanywe leo’. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje atueleze hatima ya mashamba ya Mtakata hatima yake ni nini na mpango wa serikali kwa mashamba yale ni nini, Chamanangwe, Pageni, Kipange, Hanyegwa Mchana,

lakini zaidi atuelezee hatima ya shamba la Makurunge tulilopewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati yetu ya PAC ilikwenda kule, tukaonana na viongozi wa wilaya na wakatuambia bwana tatizo ni nyinyi tu. Tulipokuja hapa kweli tulikwenda katika Ofisi ya Kilimo na wakatuambia kwamba kile chuo cha Kizimbani wale ndio watakaoandaa hati, kwa sababu ndio makubaliano kwamba wao waombe, na hati itatolewa kwao. Kwa hivyo, atakapokuja hapa Mhe. Waziri kufanya majumuisho atueleze tumefikia hatua gani katika hili, tuisahau kwamba Makurunge Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewekeza kule. Kwa hivyo, hatuwezi tukawacha mambo yakenda kama yanavyokwenda.

Katika suala hili la mifugo Mhe. Spika, naomba atakapokuja Mhe. Waziri vile vile atuelezee ukubwa wa tatizo la maradhi haya ya kichaa cha mbwa. Maana katika kila bajeti zinatengwa fedha nyingi sana na wafadhili nao wanatia fedha nyingi sana katika hili. Hebu Mhe. Waziri utakaokuja tueleze, hili tatizo hasa la kichaa cha mbwa hasa liko katika kiwango gani, ili tushawishike nalo, maana fedha ndogo tulizonazo hatuwezi tukazipeleka mwahala ambamo hakuna matumizi, tukaamini kwamba sasa hivi kuna binadamu, achilia mbali mbwa. Binadamu wana mtatizo ambayo wanahitaji kupatiwa fedha. Sasa ikiwa hakuna kichaa cha mbwa, leo tukatenga fedha kwa ajili ya kichaa cha mbwa, kwanza tuangalie binadamu kwanza hilo ndio la msingi. Binadamu hivi sasa wana maradhi ambayo hayana tiba kwa sababu ya kukosa fedha, kwa hivyo ukija Mhe. Waziri hebu tuelimishe, hiki kichaa cha mbwa kiko katika kiwango gani ili Baraza lishawishike kukuingizia fedha hizi, kulikoni kuzichukua fedha hizi kwanza tukaziingiza huko, ni bora tukazitumia katika mambo ya kibinadamu ambayo yanayohitaji kupata ufumbuzi wa haraka.

Jengine Mhe. Spika, ambalo ni la nne hilo ni kuhusu wizi wa mifugo. Kadiri wakulima wetu wanavyofuga, lakini wanarudishwa sana nyuma na wizi wa mifugo na hili linawarusidha sana nyuma Mhe. Spika. Mtu anafuga ng'ombe wake au anafuga kuku wake, lakini kwa muda wa usiku mmoja tu mtu mjanga anakuja kuchukua kibanda kizima au anachukua mifugo yote, kwa kweli hali hiyo inamfanya mkulima yule au mfugaji yule kukata tamaa na suala la mifugo kulichukua katika maisha yake.

Mhe. Spika, kwa sababu tunajua kuwa dawa kubwa ni suala zima la sheria, tuambieni watu wa wizara mmejiandaaje kuona kwamba mnazikazia sheria ili kuona kwamba tunalitokomeza suala zima linalohusiana na mifugo ya wakulima.

Mhe. Spika, suala la utawala bora katika nchi yetu ni suala la msingi sana na limepewa kipaumbele kikubwa sana na serikali yetu. Kuna kesi hii nambari 430 ya mwaka 2011 ya mshitakiwa Abdalla Makame Mweliza na wenzake 23, ambao hawa walishtakiwa kwa ajili ya uvuvi haramu, lakini walipokwenda kwenye mahakama, mahakama ikaamua kwamba watu hawa hawana kesi ya kujibu, na la msingi ni kwamba vifaa vyao vyote warudishiwe. Kulikuwa na nyavu 47, vioo vya kuzamia 16, kuna samaki. Hao samaki ndio wameshaoza na kuna madau 6. Mahakama iliamrisha kwamba watu hawa warudishiwe vitu vyao, lakini utekelezaji wa hili haujatokea. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja tuelimishe. Kwa nini mambo kama haya watu hukimbilia mahakamani na wanapokwenda mahakamani, mahakama inapotoa maamuzi, serikali haitaki kutekeleza maagizo ya mahakama, tatizo nini. Pengine utakapokuja Mhe. Waziri unaweza kutuelimisha zaidi na sisi tukaelimika. Kwa hivyo, naomba utakapokuja Mhe. Waziri naomba na hili unisaidie.

Lakini la mwisho Mhe. Spika, kwa kuzingatia muda wako, kwanza naomba nitowe pongezi kwa wizara kwa kujenga majengo mawili ya kisasa ya wizara hii kwa Pemba na Unguja. Majengo ambayo hayajazidi hata mwaka mmoja tangu kuzinduliwa kwake, naipongeza sana wizara. Pia nimpongeze waziri aliyepita Mhe. Saidi Ali Mbarouk, naamini kwamba alifanya kazi kwa juhudi kubwa katika hili.

Mhe. Spika, katika bajeti hii tumeombwa tuidhinishhe fedha za matengenezo ya ofisi. Kwa hivyo, naomba utakapokuja Mhe. Waziri unipatie maelezo juu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya matengenezo ya ofisi, katika fungu la 0013, Idara ya Uzalishaji wa wanyama Pemba, ambayo ni milioni 4,000,000. Fungu 0014 Idara ya Huduma za Utibabu na Mifugo Pemba, mmetuomba tuidhinishhe milioni 15,000,000 kwa ajili ya matengenezo ya ofisi. Fungu 0401 Idara ya Uendeshaji Utumishi milioni 3,000,000 na Fungu 0601 Idara ya Maendeleo ya mifugo milioni 12,000,000 naomba utupatie maelezo yake kwa sababu ofisi hizi hazijatimia hata mwaka mmoja tangu kuzinduliwa kwake. Leo mkija kutuambia kwamba tuidhinishhe fedha kwa ajili ya matengenezo, itabidi sasa tuanze kuchakurana angu aliyeanza kujenga nani na kwa nini ofisi hizi zikaanza kubomoka ndani ya kipindi cha miezi michache tu. Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii muhimu ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, wizara ambayo, kama ambavyo wenzangu walivyotangulia kusema kuwa imebeba idadi kubwa ya wananchi wa visiwa hivi vya Zanzibar, wananchi wetu idadi kubwa ni wavuvi na wafugaji na ni walalahoi. Kwa hivyo, ni vyema na sisi tukapata kuweka michango yetu katika bajeti hii ya Mhe. Waziri.

Kabla sijaanza kufanya hivyo, kwanza nitumie nafasi hii adhimu kumshukuru na kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiagiza Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kutafuta fedha kwa ajili ya ununuzi wa meli ya kisasa. Kwa kweli tunamshukuru sana na inaonekana Mhe. Rais anaguswa sana na matatizo haya yanayojitokeza kila siku ya kuzama kwa meli. Kwa hivyo, tunampongeza kwa hatua hii nzuri na muhimu aliyochukua katika kipindi hiki kifupi.

Mhe. Spika, mimi nianze hotuba yangu katika sekta ya uvuvi. Mhe. Waziri hapa ametueleza kwamba katika kitabu chake kuwa sekta ya uvuvi imepata mafanikio makubwa katika kipindi hiki. Ametueleza kwamba kiwango cha uvuvi wa samaki kimeongezeka, na akazitaja idadi ya tani ambazo zimeongezeka kutoka kipindi cha mwaka uliopita na kipindi cha mwaka huu.

Mhe. Spika, kama ndivyo hivyo, basi nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa ongezeko hilo. Lakini Mhe. Spika, mimi nina mashaka juu ya hizi takwim ambazo Mhe. Waziri ametueleza. Kwanza sielewi jinsi gani au takwimu hizi wanazikusanya vipi? Ukizingatia kwamba Zanzibar eneo lote la Zanzibar takriban lina wavuvi wanaovua. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze ni kwa kiasi gani au ni kwa namna gani wanaweza kuzikusanya hizi takwimu, takwimu ambazo ametuwasilishia katika Baraza hili.

Mhe. Spika, bado suala la uvuvi hususan wa bahari kuu, bado serikali haijalipa kipaumbele na ni eneo ambalo kama litashughulikiwa na serikali, basi linaweza likaongeza kiwango kikubwa cha

tani za samaki, kuliko huu uvuvi uliopo hivi sasa. Mimi niungane na wajumbe waliotangulia kusema kwamba bado serikali haijaweka kipaumbele katika suala la uvuvi wa bahari kuu, mbali na haya malengo ambayo wenzetu wametuelezea hapa. Malengo waliyotuelezea hapa ya kutoa mafunzo ya vijana 60, hayaoneshi dalili kwamba serikali kwa kweli imeazimia kutumia uvuvi wa bahari kuu kwa ajili ya kuendeleza uchumi wa watu wetu na kuondosha tatizo la kitoweo hapa kwetu kisiwani. Mhe. Spika, moja kati ya eneo ambalo linachangi kwa kiasi kikubwa mfumko wa bei ni suala la kitoweo, ambapo wananchi takriban wote hutegemea samaki kwa ajili ya kitoweo na kitoweo sasa hivi kimekuwa hali mno hususan samaki. Kwa hivyo, tunategemea serikali itowe kipaumbele sana katika eneo la bahari kuu.

Wenzetu Mhe. Spika, wana maeneo mengi kama madini, dhahabu, almasi na mambo mengine. Lakini sisi Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu ametujaalia kuwa na bahari, lakini inaonekana serikali haijaweza kuitumia rasilimali hii ya bahari kwa ajili ya kunyanyua uchumi wa nchi yetu. Suala hili Wizara ya Mifugo na Uvuvi na serikali kwa jumla inatakiwa itowe kipaumbele juu ya uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Spika, tuliwahi kupokea taarifa hapa juu ya utafiti unaofanywa kwa wenzetu wa Sri Lanka, ambao ni watu wa visiwa kama sisi, ambapo uchumi yao au mapato yao ya kila mtu ni zaidi ya dola 10,000 kwa mwaka. Maendeleo hayo wameyapata kutokana na uvuvi wa bahari kuu, na wao walikuwa maskini kama sisi na hawatumi meli kubwa za uvuvi ni meli za wastani ambazo serikali yetu ina uwezo wa kushajihisha makampuni ya kule kuja kueleza katika maeneo haya. Lakini imebakia ni hadithi utekelezaji hatuoni, maendeleo yake hatuyaoni, tumekuwa tukipokea taarifa za matumaini lakini kwa kweli utekelezaji hauonekani.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho, mbali ya hizi taarifa unazotupa za kuongezeka kwa tani za samaki. Hebu uje utuelezee ni mikakati gani serikali imeweka katika kuhakikisha kwamba tunaitumia rasilimali ile ya bahari kuu kwa ajili ya uchumi wetu na maendeleo ya watu wetu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa katika hotuba yake ametuelezea mradi wa kuimarisha miundombinu ya mifugo. Katika eneo hili kuna malengo mengi ambayo yamelengwa, ametuelezea hapa malengo ambayo yamelengwa. Lengo moja ni suala zima la ujenzi wa chinjio jipya la kisasa huko Kisakasaka. Lakini pamoja na malengo mengine kwa jumla. Pamoja na kwamba mradi huu ni wa miaka minne, lakini bado miradi hii inaonekana *speed* wake au utekelezaji wake ambapo tayari mwaka mmoja umeshakamilika, basi hauoneshi matumaini.

Mhe. Spika, malengo ambayo yamelengwa katika mradi huu ambao unajumla ya shilingi bilioni 7,200,000,000 kwa muda wa miaka minne kama alivyotueleza, ambapo kuna jumla ya fedha ambazo zimetumika, zilizotengwa mwaka jana 2011/2012 ambazo ni shilingi milioni 243,000,000. Hebu Mhe. Waziri uje utueleze, fedha hizi zimetumikaje katika maeneo mbali mbali haya ambayo umetuelezea kwenye ukurasa wa 57.

Mhe. Spika, pia kuna mradi huu wa ujenzi wa chinjio jipya la kisasa huko Kisakasaka, ambapo ametuelezea kwamba utekelezaji wake kwa mwaka 2011/2012 ni ziara ya wataalamu tu ambao wametembelea machinjio ya Tanzania Bara, ambako ni Sumbawanga, Dodoma na Arusha kwa ajili ya kutayarisha hadudi rejea ya kutafuta mzabuni na kuandaa mchoro.

Aidha mchakato wa kumpata mzabuni wa kutayari mchoro kwa ajili ya chinjio jipya la kisasa ulianza, pamoja na mambo mengine ambayo alituelezea Mhe. Waziri, ambapo jumla ya shilingi milioni 200,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huu katika kipindi kijacho.

Sasa Mhe. Spika, mradi wa ujenzi wa chinjio la Kisakasaka umekuwa ni hadithi. Leo katika kipindi cha mwaka mzima bado wataalamu wametembelea maeneo ya michoro na wanatuambia kwamba mchakato huo umeanza upya na unategemea kuendelea hadi mwaka ujao wa fedha, yaani sio mwaka huu tena. Kuna fedha zimetengwa, lakini mchakato wa ujenzi wa chinjio utaanza mwakani, sio mwaka huu, ambapo suala la ujenzi wa chinjio tumelizungumza tokea Baraza lililopita. Leo inasikitisha kuwa chinjio lile muhimu na linahudumia maeneo makubwa hususan ya mjini, lakini chinjio lile ni bovu halifai, lakini bado utekelezaji wa jambo hili unaonekana ni hadithi. Kwa kweli Mhe. Spika, jambo hili linasikitisha sana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hebu tupe hasa malengo yako na mipango yako juu ya ujenzi huu. Kwa sababu mmetembelea maeneo mengine, mmefanya michoro, lakini unatueleza utekelezaji wake hasa utaanza mwakani. Mhe. Waziri tueleze ili tupate kufahamu.

Jengine Mhe. Spika, ni suala la mradi wa *MACEMP*. Mradi wa *MACEMP* ambapo mradi huu umeanza tokea mwaka 2006 na tunategemea utamalizika mwaka huu. Mhe. Waziri hapa ametuelezea mafanikio yake. Kwa kweli Mhe. Spika, mradi huu umepata mafanikio makubwa, umewawezesha wavuvi wetu, wafugaji wetu na umewawezesha watu wengi sana, kwa sababu ni fedha ambazo kwa kiasi fulani zimetumika hasa na ni fedha ambazo kwa kiasi fulani zimekwenda kwa walala hoi. Mhe. Spika, mimi ni mmoja kati ya waliokuwa wakisimamia mradi huu kwa kupitia Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, katika kipindi kilichopita kabla ya kuhamishiwa katika wizara hii ya mifugo ni mradi ambao umepata mafanikio.

Mhe. Spika, inashangaza kwamba mradi huu ambao unamalizika mwezi wa Disemba mwaka huu, umetegewa jumla ya shilingi milioni 100,000,000 katika kuuendeleza. Ambapo mwaka jana mradi wa *MACEMP* serikali ilitoa shilingi milioni 216,000,000. Kwa nini Mhe. Spika, fedha hizi zimepunguzwa na wakati mradi huu unahitaji kuendelezwa. Kwa kweli Mhe. Spika, tumekuwa na kawaida kwamba miradi inapopata wafadhili, wafadhili wanapotusaidia katika miradi mbali mbali na miradi hii inapokamilika sisi SMZ miradi ile huwa tunaiwacha na kuitelekeza, badala ya kuishughulikia na kuona kwamba inaendelea, kwa lugha ya leo inaitwa endelevu, yaani miradi inakuwa endelevu, lakini tunaitelekeza na hatimaye miradi hii inafifia.

Mimi Mhe. Spika, nilitegemea kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika miradi hii, serikali mbali ya kutafuta wahisani wa namna ya kuendeleza, basi itenge fedha ambayo wahasika wanaweza kuuendeleza mradi huu, jambo sio kwa kiasi kikubwa kwa kiasi kile cha wahisani. Lakini zitengwe fedha ambazo zingesaidia kuendeleza miradi ile kuliko hivi ilivyo na kinyume chake sasa hivi, SMZ imekuwa ikipunguza michango katika miradi hii. Kwa kweli hili jambo linasikitisha sana na hili linaweza likasababisha miradi hii au nguvu zile ambazo zimetolewa na wahisani ziwe zimefifia. Kwa hivyo, niombe serikali kwamba itenge fedha za kutosha, sio kwa mradi huu tu wa *MACEMP* ni kwa miradi yote ambayo ilikuwa inafadhiliwa na wahisani na muda wake unamalizika, ili miradi ile iwe endelevu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tano.

Mhe. Omar Ali Shehe: Ahsante Mhe. Spika, suala la wakulima wa mwani. Mhe. Spika, wizara hii inawasimamia kwa karibu sana wakulima wa mwani. Wakulima wa mwani kwa asilimia kubwa ni kinamama. Kwa kweli kina mama wanahangaika sana katika kujipatia kipato na riziki zao za kila siku, lakini bei ya mazao hayo bado inaonekana ni ndogo, hatujui serikali inafanya juhudi gani ili kutafuta namna ya kuongeza bei ya zao hili.

Kamati yangu ilipata nafasi ya kutembelea wakulima fulani wa Mwani Chwaka na walituelezea *concern* yao, namna gani wanaweza kufaidika walimu wa mwani na zao hili kuliko ilivyo sasa. Vile vile walitueleza kwamba utafiti wao unaonesha kuwa mwani unatumika katika maeneo ya vipodozi na ni eneo ambalo mwani unapata thamani kubwa.

Sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba atakapokuja hapa atuelezee wizara yake juu ya eneo hili la matumizi ya mwani inachukua hatua gani, ili kuona wakulima wa mwani wanafaidika na rasilimali hii kuliko ilivyo hivi sasa, kwani bei ya mwani ni ndogo na usumbufu umekuwa mkubwa.

Mhe. Spika, mwisho nimeangalia kitabu cha Mhe. Waziri namna ya bajeti zilivyopangwa na mtiririko mzima wa fedha zilizoombwa. Kwa kweli mipango ni mizuri na *follow* ya fedha ni nzuri, isipokuwa nataka aje anieleze katika eneo moja la mishahara katika Idara ya Maendeleo ya Mifugo. Eneo hili limekua sana ni kubwa ukilinganisha na mwaka jana na mwenyewe akiangalia ataziona na wala sitaki kuzitaja hizi takwimu, lakini eneo la mishahara limekua mara dufu ukilinganisha na mwaka jana.

Vile vile katika Idara ya Uzalishaji wa Wanyama nalo limeonesha sura ya kukua sana katika eneo la mishahara zaidi ya mara tatu ya kiwango cha mwaka uliopita. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe maelezo kidogo, kwani kiwango cha mishahara ukilinganisha na mwaka jana kimekua zaidi ya mara tatu au nne na kile cha mwaka jana uliopita.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunashukuru. Sasa tumkaribishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadaye Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema pamoja na rehema zake tukiwa hai tena wazima na tunaendelea na vikao hivi katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie machache katika Bajeti hii ya Wizara hii muhimu ya Mifugo na Uvuvi. Vile vile naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo inajieleza vizuri nini malengo yao kwa mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, eneo la kwanza ambalo napenda nichangie na niungane na Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kwamtipura Mhe. Hamza Hassan Juma kwa yale aliyoyasema. Mhe. Spika, Baraza lako linapita katika kipindi muhimu hivi sasa na wananchi wamejenga matumaini makubwa na Baraza hili. *(Makofi)*

Kwa kweli kwa sababu hiyo wapo vitimbakwiri wachache ambao wanajali zaidi maslahi yao binafsi kuliko maslahi ya wananchi wa Zanzibar, ambao wanafanya kila liwezekanalo kujaribu kutugawa tena Mhe. Spika. Mimi naamini kwamba njama zao hizo na vitimbi vyao hivyo vitawarejea wenyewe, kwa sababu wananchi wa Zanzibar hawajawahi kuamka kama ambavyo wameamka katika kipindi hichi tunachokizungumza. *(Makofi)*

Kwa hivyo, yeyote atakayejaribu kutaka kutugawa na kupandikiza tena chuki za itikadi za kisiasa, akatamka kwamba sisi bado ni maadui wa asili, basi huyu ni adui wa nafsi yake na atajimaliza mwenyewe Mhe. Spika katika zama hizi mpya za siasa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wananchi wa Zanzibar hivi sasa wanachotaki ni haki zao katika Muungano, lakini pia wanataka serikali yao iwajibike, ili maslahi yao yaweze kulindwa na fedha waliyoitoa kama walipa kodi iweze kuwanufaisha wao. Masuala ya kuvutana mara nyingi tumeshazungumza, kwamba tumevuta vyakutosha, tumepambana vya kutosha na wala hakuna aliyenufaika zaidi ya kwamba sote tumekula hasara.

Kwa maana hiyo, nawaomba wananchi wa Zanzibar wawe makini na hata wale wenye vigazeti uchara Mhe. Spika, ambao wamehizika kwa sababu wameshindwa kuwatumikia wananchi kwenye majimbo na wakaja wengine na kuonesha uwezo wao. Sasa wanajaribu kuficha nyuso zao chini kwa kuandika maneno ya uchochezi kwenye vigazeti vyao, hawa pia watahizika na watamalizika katika siasa hizi mpya ambazo zinaendelea katika nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo nadhani salamu zimewafika naomba sasa nije katika bajeti hii. Naomba nianze tena kwa kuungana na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura katika suala zima alilolizungumza linalohusu Sekta ya Mifugo hasa katika eneo la Uwekezaji Mkubwa katika Uzalishaji wa Kuku.

Mhe. Spika, mwaka jana katika mchango wangu Mhe. Waziri akenda kuangalia *Hansard* atakuta, niligusia sana suala hili kwamba hivi sasa angalau kama kuna sekta moja ambayo wananchi wa Zanzibar wamejitokeza na kuwekeza ni katika Sekta ya Uzalishaji wa Mifugo hasa kuku na hii ina wawekezaji wa kati mpaka wawekezaji wa mitaani wanakuja na kufanya mashauriano na Wawakilishi pamoja na Wabunge wao kutaka kusaidiwa wamejiwekeza huko.

Kwa hivyo, tukasema utakapoleta uwekezaji mkubwa Mhe. Spika hawa utawaua na hili ndilo ambalo linajitokeza hivi sasa, wengi zimewashinda njiani. Mhe. Spika, nasema uwekezaji wa ndani lakini hata uagizaji wa kiasi kikubwa wa kuku kutoka nje unaua uwekezaji mdogo mdogo wa watu wetu.

Mhe. Spika, naomba suala hili wizara ilitazame au ilifikirie tena na Mhe. Hamza Hassan Juma ametoa rai nzuri sana kama kuna wawekezaji basi wao wajikite zaidi katika uzalishaji wa hivi vifaranga ambavyo watu wetu hawana ujuzi navyo, kwa sababu hawa wanao uwezo mkubwa wa

kifedha, wana-*contact* duniani na wanaweza kujiingiza huko, lakini baadaye hivi vifaranga wawasaidie hawa wafugaji wadogo wadogo na wao waweze kupata chochote Mhe. Spika. (Makofi)

Sasa ikiwa sisi hatuwezi kuwasaidia, hivi nani ataweza kuwasaidia wananchi wetu ambao ni masikini kabisa. Kwa hiyo, naomba hilo Mhe. Waziri na niliomba mwaka jana nalisema kwa ufupi na mwaka huu naomba pia alitazame tena. (Makofi)

Vile vile katika upande wa Sekta ya Mifugo na mimi niungane kuhusu suala la udhalilishaji na utesaji wa wanyama na watu wameshalizungumza vya kutosha na wala sina haja ya kuliingia kwa undani. Lakini sote ni mashahidi jinsi wanyama hasa punda na ng'ombe wanavyotumikishwa kupita kiasi na wakawa wanadhaliishwa, yaani hata Dini yetu inakataza Mhe. Spika.

Kwa mfano, kuna Hadith maarufu ya Mtume Muhammad (S.A.W), ambapo aliwaonya waumini katika kuwaadhibu wanyama, kwa sababu na wao ni viumbe wa Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, na hilo naomba wizara ituambie inalingalia vipi kwa sababu limeshatolewa kauli sana na huku Baraza limeshazungumzwa sana, lakini bado ukitizama hali hairidhishi Mhe. Spika. Kwa mfano, unaweza kumkuta mnyama amejaa makovu na madonda kutokana na hilaki anazopatishwa na wenye kuwamiliki. Kwa hiyo, na hili naomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja alitolee ufafanuzi. (Makofi)

Jambo jengine Mhe. Spika, naomba nigusie Sekta ya Mifugo na pia itahusu Sekta ya Uvuvi ni suala zima na pengine wao wizara yao hauhusiki moja kwa moja, lakini hawawezi kukwepa kwa sababu wanahusika wanayo machinjio na masoko ya samaki, suala zima la usafi wa sehemu hizi Mhe. Spika na mara nyingi tumekuwa tukilizungumza.

Kwa kweli bado tunalo tatizo kubwa sana la kutozingatia Kanuni za Usafi katika masuala haya na mara nyingi nimekuwa nikilisema Mhe. Spika, kwa sababu hivi vyakula vinaliwa na binadamu. Sasa ukija kuangalia masoko ambayo yanasimamiwa na wizara hii baadhi yao na mengine yako katika Wizara ya Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa sababu ndio inayosimamia mambo ya Manispaa pamoja na Halmashauri za Wilaya, basi ni vyema kushirikiana kwa sababu serikali hii ni moja, ili kuona kuna utunzaji wa mazingira.

Mhe. Spika, haipendezi chakula anachokula binadamu unakuta mtu amejitwika, samaki wanabururwa ovyo mitaani, nyama zikitoka machinjioni watu wanajibebea tu, yaani uchafu mtupu, haya hayapendezi katika karne hizi hayapendezi, hasa kwa sababu katika sekta ambazo tumekusudia kuziimarisha katika uchumi wetu ni Sekta ya Utalii, sasa utalii Mhe. Spika ni pamoja na kuweka maadili pamoja na usafi wa mazingira kwa wageni wetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili alitazame vizuri.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Spika na watu wamezungumzia masoko na mimi mwaka jana nilizungumzia kuhusu soko juu ya haja ya kuliangalia tena Soko la Malindi na mwaka jana nilitoa hoja kwamba wakati umefika wizara iangalie kujenga Soko jipya kwa eneo la Mjini la Samaki na wengi mwaka jana tulitoa mapendekezo kwamba tulisema eneo la Kizingo litizamwe Mhe. Spika, kwa ajili ya kujenga Soko jipya.

Kwa hivyo, nashukuru kwa Tumbe wameshapata, sasa hebu wakutizame na mjini, kwa sababu pale lilipo Soko Kuu hivi sasa pamekuwa wengi watu wengi wanakimbilia Malindi, kwa sababu wakitoka baharini pale ndipo wanapofikia, lakini pamezidiwa mno na mara nyingi panasababisha uchafuzi wa mazingira Mhe. Spika kuliko hiyo biashara yenyewe kufanyika katika mazingira mazuri. Kwa hiyo, hili pia namuomba Mhe. Waziri alitizame sana, ili aone haja ya kuwasaidia.

Mhe. Spika, nataka nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana vijana wa Polisi Jamii wa Mji Mkongwe hasa wanaoshughulika na Shehia ya Malindi, mwaka jana nilipiga kelele sana juu ya uchafu wa sehemu ile. Lakini nashukuru kwamba vijana wa Polisi Jamii wameshirikiana na Baraza la Manispaa katika eneo lile la Soko la Malindi angalau hivi sasa linatizamika, nawapongeza sana.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo naomba nije katika hii kadhia ambayo wengi wameizungumza na kila Mwakilishi anafuatwa na wananchi wanapiga kelele suala zima la hii Sheria ya Uvuvi ambayo wavuvi wengi wanaipigia kelele kwamba haikuwashirikisha ipasavyo na ndio maana inaleta matatizo mwakubwa katika utekelezaji wake.

Mhe. Spika, ninayo hapa risala ambayo nadhani Mhe. Waziri atakuwa nayo ni Risala ya Jumuiya ya Maendeleo ya Wavuvi wa Kojani waliomsomea Mhe. Waziri katika Ukumbi wa zamani wa Baraza la Wawakilishi Kikwajuni tarehe 03/07/2012.

Kwa kweli yapo mambo ya msingi na wala sitaki kuyasoma, lakini yale mambo waliyoyaeleza mule Mhe. Waziri aje atusaidie amechukua hatua gani baada ya kupewa hii risala, kwa sababu wamelalamika hapa kwamba hawakushirikishwa katika uandaaji wa sheria ile, pia wamelalamika kwamba wizara inao wataalamu wazuri sana wa kutunga sheria, lakini haionekani inao wataalamu wazuri wa mambo ya uvuvi kiasi ambacho cha kuweza kutambua zana zipi zinafaa, zipi hazifai.

Kwa mfano, anasema hapa mbona kuna kupingana, serikali inahimiza wananchi wale dagaa, lakini vifaa vya kuvulia dagaa vinapigwa marufuku, sasa hao dagaa wanaohimizwa wananchi wale watapatikana vipi ikiwa vifaa vya kuvulia dagaa vinapigwa marufuku.

Kwa hivyo, wanaona kuna *contradictions* na pengine hawa ndio wavuvi kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba Mwakilishi wa Kojani amelieleza vizuri kwa sababu wanaelewa haya mambo kuliko sisi wengine. (*Makofi*)

Mhe. Spika, yako mambo mengi ya msingi, ambayo yameelezwa katika risala yao hii na wala sitaki kuisoma hapa, hivyo namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja atusaidie kwamba amechukua hatua gani kuyashughulikia haya mambo ya msingi ambayo wavuvi hawa waliyaeleza.

Mhe. Spika, sasa naomba nije katika suala la Uvuvi wa Bahari Kuu. Mhe. Spika, mwaka jana mimi nilihoji suala la mgao wa fedha au mapato yanayotokana na Uvuvi wa Bahari Kuu kwa upande wa Zanzibar. Kwa kweli kama tunavyojua kuwa tumeunda Mamlaka moja ya Uvuvi wa

Bahari Kuu kwa pande au nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano, tukitambua kwamba uvuvi si suala la Muungano.

Kwa hivyo, pakawekwa *formula* ya mgawanyo wa mapato, kwamba asilimia 50 ya mapato itatumika katika kusimamia masuala ya utawala na uendeshaji wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, asilimia 30 itakuwa ni mapato kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na asilimia 20 itakuwa kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mwaka jana nilionesha katika swali ambalo liliulizwa Bungeni, kwamba ukitizama yale mapato halisi na mgao tulipewa sisi ulikuwa haulingani, lakini nashukuru Waziri ayekuwepo wakati ule aliahidi kulifuatilia na hivi karibuni nilipata nakala ya Mhe. Spika tarehe 18 Julai, barua iliyokuja kwako na mimi nilipewa nakala kama mtu niliyetaka maelezo juu ya mgao ule wa fedha.

Kwa kweli nashukuru kwamba wameweza kuthibitisha hoja yangu tulichotakiwa tukipate kilikuwa hakipungui shilingi milioni 600,000,000/= na wamenithibitishia mwisho zilipatikana shilingi milioni 634,677,276/=.

Lakini Mhe. Spika, napata matatizo hii ilikuwa kwa mwaka 2010/2011, mwaka jana au mwaka wa fedha uliomalizika Mhe. Spika, kwa mujibu wa hotuba ya Mhe. Waziri mapato ya Uvuvi wa Bahari Kuu yalitegemewa kuwa ni shilingi milioni 900,000,000/= ambayo ingekuwa kama nyongeza ya asilimia 50 kutoka mwaka 2010/2011. Kwa hivyo, kilichopatikana ni shilingi 133,770,234/=, ambapo kwa maelezo ya Mhe. Waziri mwenyewe ni asilimia 15 ya makisio.

Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie kumepita nini huko, kwa sababu sisi ndio tunaosimamia moja kwa moja kiasi cha kwamba mapato haya mwaka juzi yalikuwa yamefika shilingi milioni 600 na zaidi, lakini mwaka jana yamepungua hadi kufika shilingi milioni 133/= tu, ambayo ni asilimia 15 ya makisio.

Mhe. Spika, na hili naliomba maelezo kwa sababu ninalo Gazeti hapa la *Citizen* la tarehe 18 Julai, 2012, siku ambayo niliyojibiwa barua yangu kuna habari hapa ambayo inayosema.

“The Paradox of Tanzania Fishing Industry” Mhe. Spika, *story* hii naomba niisome kidogo *paragraphs* mbili tu, naomba kunukuu, ambayo inayosema. *“Despite the country earning shilling 1.2 trillion in 2012 from the Fishing Industry from hundred and seventy seven thousand two hundred, five hundred and twenty seven License Fisherman yet the Sector’s contribution to the National Economy remains minimum.*

In the same year the country exported fish and Fisheries Products worth shilling 30.01 billion, ambazo ni Dollar hundred and seventy six thousand seventy ninety seventy point eight million dollar. However the government earned shilling five point eight six six billions in review”

Mhe. Spika, hii namuomba Mhe. Waziri alitafute hili Gazeti la *Citizen* tarehe 08 Julai, 2012, linaonesha ni kiasi gani kuna upotevu mkubwa sana wa mapato kutokana na kutokuwa na usimamizi mzuri katika Sekta nzima ya Uvuvi. Sasa hii imeambiwa Jamhuri ya Muungano kwa

jumla wake, lakini kwa sababu Uvuvi wa Bahari Kuu unasimamiwa kwa pamoja hatujui sisi tunathirika kiasi gani.

Mhe. Spika, hapa tunaambiwa kwamba nchi inapata 1.2 *trillion* katika uvuvi, lakini kinachokiingia katika serikali hata kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano ni kima kidogo sana, hili nasema sio kwa sababu tunadhulumiwa hata huko Bara nao pia hawapati. Kwa hivyo, nasema inaonekana kuna hitilafu hapa katika kufuatilia mapato haya.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie je, suala hili liko mikononi mwa Jamhuri ya Muungano kwa Zanzibar athari yake ni kiasi gani katika utafiti wao na sisi tunakosa kiasi gani kutokana na mapato haya? (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika hili naomba nimalizie moja suala la Uvuvi wa Bahari Kuu linajumuisha pia suala zima la udhibiti wa eneo Huru la Bahari au Ukanda wa Bahari (*Exclusive Economic Zone*), ambalo tulilijadili katika Baraza hili Mhe. Spika.

Sasa sisi bado hatujapata nafasi ya kuliambia Mhe. Spika, kwa sababu mjadala wake uliuhairisha baada ya kutaka tujadili Ripoti ya Serikali. Lakini tunaambiwa hivi sasa tunavyozungumza Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati akifuatana na Mjumbe mmoja wa Baraza la Wawakilishi wamekwenda Marekani kwa ajili ya kuendeleza mazungumzo ya suala hili ambalo sisi Baraza la Wawakilishi bado hatujamaliza kulizungumza Mhe. Spika.

Kwa hivyo, sijui ni kiasi gani katika suala la Uvuvi wa Bahari Kuu, suala hili lina muingiliano na ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie wamefikia wapi?

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naomba nipate maelezo ya matumizi. Kwa kweli mwaka jana kabla sijaja katika vifungu kwenye Mradi wa *MACEMP*, ambao ulikuwa na jumla ya *Dollar* za Kimarekani mafungu mawili, fungu la kwanza ni *Dollar* milioni \$4,044,35.65 zilizotolewa na *IDA* na *Dollar* milioni \$1,740,262 zilizotolewa na *GEF* na Serikali ya Zanzibar nayo ikatoa shilingi milioni 216,000,000/=.

Mhe. Spika, katika jumla ya miradi ambayo ilipangwa kusimamiwa na mradi huu ilikuwa ni kuendelea na ukarabati wa maeneo mawili ya kihistoria *Palace Museum*, *Beit-el-Ajab* na *Mtoni Palace*. Aidha maeneo mengine 25 ya Unguja na Pemba yatapimwa na taarifa zake kuhifadhiwa kwa matumizi ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Hivi karibuni niliuliza swali Mhe. Spika, kwamba nikenda kuangalia hali halisi ya matengenezo, sijui katika hizi fedha ambazo nimejitaja ni kiasi gani zilitengwa kwa ajili ya matengenezo haya. Lakini nimuombe Mhe. Waziri alitizame tena, kwa sababu katika kitabu chake cha mwaka huu anaambiwa kwamba utengenezaji wa *Palace Museum* umefanyika vizuri sana.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri akakague na mimi nilikwenda hivi karibuni na wala hakuna matengenezo ya maana yaliyofanyika pale, ukienda Beit-el-Ajab ndio kabisa na humu tumeambiwa kuna mradi wa kuunga umeme wakati lile jengo liko katika hali mbaya kwenye maeneo mengi sana na pale hivi sasa ndipo palipohamishiwa Makumbusho ya Taifa Mhe. Spika. Kwa hivyo, naomba haya Mhe. Waziri atakapokuja anieleze, kwamba fedha zile zimetumika

kiasi gani katika kuhudumia maeneo haya yaliyotajwa wakati sisi tunaokaa Mji Mkongwe bado hatujaona marekebisho yoyote.

Mhe. Spika, eneo jengine la matumizi ambalo naliombea maelezo na namshukuru kwamba bajeti yake kiasi kikubwa imekaa vizuri, hili namshukuru na ninampongeza sana. Lakini kuna mafungu mawili au matatu yamenishtua naomba maelezo.

Kwanza kama kawaida fungu la safari inaonekana ni *priority* ya kila wizara yetu na wala sitaki kusema moja moja, lakini nimezifanya hesabu idara zote 6 ambazo unaziwaga mara 12, maana yake ni 6 Unguja na 6 Pemba. Fungu la Safari peke yake Mhe. Spika, lina jumla ya shilingi milioni 239,300,000/= kwa wizara hii. Lakini fungu jengine la Mafunzo lina jumla ya shilingi milioni 157,823,000/= kwa jumla ya idara zote ukizijumlisha kwa pamoja.

Mhe. Spika, ukijumlisha mafunzo na safari peke yake zimechukua shilingi milioni 397,123,000/= kwa wizara hii, katika bajeti ambayo jumla yake ni shilingi bilioni 3,529,000,000/=. Kwa hivyo, tunaomba maelezo katika haya, hivi kwa nini *priority* za wizara zetu zote ni kusafiri na mafunzo tu kuliko tija ya shughuli ambazo wanazifanya zikaonekana kwa wananchi.

Lakini ukiondoa mafungu hayo, mafungu madogo madogo ambayo ninayoyaomba maelezo naomba pia aje anieleze katika Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Pemba kwenye *Sundry items* mwaka huu kumetengewa shilingi milioni 11,700,000/= kutoka shilingi milioni 1,000,000/= mwaka jana. Kwa hivyo, kuna ongezeko kubwa sana la *Sundry items* katika idara hii kwa upande wa Pemba.

Vile vile katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwenye ukusawa wa 294 buku kubwa kuna Fungu la Sera na Sheria limetengewa shilingi milioni 21, 286,000/= naomba maelezo juu ya Sera na Sheria hizi ambazo zinategemewa kufanyiwa kazi katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Fungu la Ruzuku kwenye sehemu ya utafiti kumetengwa shilingi milioni 18,871,000/=. Sasa mimi Mhe. Spika, kwa mtazamo wangu katika Idara moja ya Mipango, Sera na Utafiti mambo ya sera na sheria yanaendana na utafiti, sasa kule kuna fungu la shilingi milioni 21,286,000/=. Lakini halafu kuna sehemu ya utafiti tena ruzuku ni shilingi milioni 18,781,000/=. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anipatie maelezo, ili niridhike na niweze kumpitishia bajeti yake.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kama nilivyosema kwa jumla maeneo mengine sina matatizo nayo na ninaiunga mkono hoja. Lakini naomba maelezo ya kina katika mafungu haya ambayo nimeyahoji. Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa nimkaribishe Mhe. Panya Ali Abdalla na baadaye Mhe. Kazija Khamis Kona.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii. Kwanza kabisa na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukakutana hapa asubuhi hii. Pili nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, ambaye umenipatia hii

nafasi. Tatu nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanajitahidi kuifanya.

Mhe. Spika, kusema kweli mimi mchango wangu utakuwa mdogo kidogo, kwa sababu wenzangu wengi wametangulia kusema na wamenifilishi. Lakini naomba nichangie angalau kidogo nataka nianze na hii Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo. Mhe. Spika, idara hii inajishughulisha na tiba pamoja na kutoa elimu ya ukatili wa wanyama.

Kwa kweli hapa mimi nataka nimshauri Mhe. Waziri, kwamba hii tiba ambayo wanawapatia mifugo kuweza kuwashajihisha wenyewe wafugaji kuwapatia elimu, ili waweze kukabiliana na matatizo haya ya kuwatibu wanyama wao pale inapotokea ugonjwa, isipokuwa ule ugonjwa utakaokuwa mkubwa ndio waweze kuwatafuta wataalamu wenyewe kwa ajili ya kuwasaidia zaidi.

Maana ya kusema hayo, ni kwamba ugonjwa kwa mnyama unaweza kutokea wakati wowote na wataalamu kama alivyotangulia mwenyewe kusema kuwa wataalamu ni kidogo. Kwa hivyo, watakapowapatia hawa wafugaji elimu basi inaweza kuwasaidia na wakaweza kukabiliana na mambo ya kuwatibu wanyama wao, kuliko kusubiri wale wataalamu ambapo inaweza kutokea hasara kubwa kwa wafugaji na mifugo ikaweza kufa.

Mhe. Spika, naomba nizungumzie suala la ukatili wa wanyama, ambapo wenzangu wamelisema sana na amenifilisi sana Mhe. Rufai Said Rufai pale alipotaja ng'ombe aliyekwenda kushtaki. Hali hii inaonesha kwa kweli wanyama hatuwatendei haki. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kwamba hii Sheria ya Kuwakinga na Ukatili Wanyama kama ipo, basi huu ni wakati muafaka itumike, kwani wanyama tunawaona wanateseka na wengine tukipita tunashindwa kwenda safari zetu, tunasimama na kugombana nao kwanza. Mhe. Spika, kama sheria ipo basi itumike, ili waweze kuchukuliwa hatua wale wanaowasumbua wanyama.

Vile vile nichukue fursa hii kutoa wito kwa wale wafugaji wetu ambao wanafuga wanyama hawa na wanyama ndio wanaowaingizia kipato cha kupata riziki za kila siku na kuweza kukimu maisha yao.

Mhe. Spika, nawaomba sana wafugaji wawahurumie sana wanyama wao, wakizingatia kuwa hawa ndio wanaowasababishia maisha yao kwenda vizuri kila siku. Kwa maana hiyo, kumuhurumia mnyama wako kwa kubebesha mizigo ambayo itakuwa inaunafuu kwake pamoja na kumuondoshea ule usumbufu wa kumpiga hali ya kuwa huku umembebesha mzigo ambao ni mkubwa. Kwa kweli suala hili tujenge imani sisi wenyewe, ili tuweze kuwadumisha wale wanyama wetu na tuweze kuwatumia kwa muda mrefu.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie Idara ya Utumishi na Uendeshaji napo wenzangu wamezungumzia sana hasa katika ufugaji wa kuku. Mhe. Spika, nataka nimshauri Mhe. Waziri kufanya ziara ya makusudi kuwatembelea hawa wafugaji wa kuku, ili mkaweza kugundua zile changamoto zao na wakaweza kupata ushauri wa kitaalamu.

Vile vile kuliangalia vizuri soko la wafugaji hawa ambalo linawasumbua kila siku kuona wao wanafuga, lakini bado wanaendelea kupata kuku sehemu nyengine na wao wanashindwa kuuza wale wa kwao.

Mhe. Spika, pia namuomba sana Mhe. Waziri katika ufugaji awatembelee sana hawa wafugaji wa mbuzi wa maziwa. Kwa kweli wafugaji hawa wanakabiliwa na changamoto pia wanapenda kupata ushauri wa mara kwa mara kutoka kwa wataalamu, ili waweze kuendesha vizuri mifugo hii na kuweza kupata tija.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu Idara ya Mazao ya Baharini. Mhe. Spika, hapa pia Mhe. Waziri ametueleza neno zuri ambalo kidogo lina mvuto na ninaomba kwa ruhusa yako Mhe. Spika ninukuu hichi kifungu cha 8(1)(d).

Ukurasa wa 40 kifungu cha 8(1)(d) ambacho kinaeleza hivi:-

“Kuhamasisha wanajamii kujihusisha na ufugaji wa samaki, chaza, uzalishaji wa lulu na kaa pamoja na kuimarisha usarifu na uuzaji wa mazao hayo katika masoko ya ndani na nje ya nchi”.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuliona hilo, kwa sababu hivi sasa tayari tumekuwa na wafugaji hawa. Lakini nimuombe kwamba niwe karibu naye sana kwa ajili ya kufuatilia, kwa sababu katika mkoa wangu wapo wafugaji wa namna hii kama vile wafugaji wa kaa, chaza pamoja na samaki.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri usinichoke kuniona ofisini kwako kwa ajili ya kufuatilia, ili kuona wazalishaji wetu hawa tunaweza kuwapatia utaalamu wa mara kwa mara, kwa ajili ya kuendesha shughuli zao hizi, ili waweze kujikimu katika maisha yao na kuondokana na umasikini. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika mazao ya baharini kuna wanawake ambao wanajishughulisha na utandaji wa dagaa. Kwa kweli katika mkoa wangu hawa ni wafanyabiashara wakubwa na Mhe. Haroun Ali Suleiman (Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika) atakuwa shahidi, kwa sababu hivi karibuni alikuja kutufungulia benki na wanawake wameshakopa fedha nyingi.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri labda aniambie ataweza kuwasaidia vipi wanawake hawa waweze kuendesha miradi hii na waweze kulipa fedha hizi, ili ziweze kuwasaidia wengine, kwa sababu biashara hii inasumbua wakati wa mvua. Mhe. Spika, wakati wa mvua waanikaji wa dagaa wanapata shida sana na ndio maana hata katika bajeti iliyopita niliweza kusema kama Mhe. Waziri angefanya utaratibu wa kuwajengea kiwanda cha kukaushia madagaa hawa, ili wakawa wazalishaji wazuri kila wakati pamoja na kulipa deni kwa wakati pia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu yale mashamba yetu ya Serikali ambayo wenzangu wameyataja hapa. Kwa kweli nafurahi sana tunapokuwa na yale mashamba yetu ambayo tumeyamiliki sisi wenyewe serikali na tukawa wazalishaji na hapo wafugaji wetu wanaweza kuwa na sehemu nzuri ya kwenda kukopia, kwa sababu tayari serikalini mradi huu upo na tulikuwa na Mashamba ya Ufugaji wa Ng’ombe kama walivyoeleza wenzangu sehemu za Pangeni na nyengine tulikuwa nayo mashamba haya.

Mhe. Spika, wakati huo yalikuwa yakizalisha uzalishaji mzuri, kwa sababu tulikuwa tunacho hata Kiwanda cha Siagi, Maziwa vilikuwepo, kwa sababu ng'ombe tulikuwa nao wa kutosha.

Kwa hivyo, mimi nataka kujua suala hili na Mhe. Waziri wakati utakapokuja hapa unieleze, je ni lini mashamba haya yataweza kurejea katika hali yake ile, ili wafugaji wetu hawa wawe na sehemu za kwenda kuangalia na wala isiwe tunategemea wafugaji wa kibinafsi ambao hatuna tamaa nao kubwa sana. Kwa maana hiyo, naiomba sana serikali iweze kufufua ile miradi yake ambayo itaweza kujiendesha na hata kuiingizia mapato serikali yetu.

Baada ya hayo, niseme kwamba sina la kusema kwamba sababu wenzangu wamenifilisi. Lakini naomba kusema mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunashukuru. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Kazija Khamis Kona, atatumia dakika 8 kama alivyoomba na baadaye Mhe. Abdi Mosi Kombo. *(Makofi)*

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mhe. Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia hai ya uzima na tukakutana hapa.

Vile vile naomba kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wa wizara. Mhe. Spika, naomba nimpongeze kijana mwenzangu Mhe. Viwe Khamis Abdulla kwa kuwasilisha maoni yetu ya kamati. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nianze na mchango na suala linalohusu Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010. Kwa kweli niliuliza swali hapa Mhe. Spika, Mhe. Waziri alinjibu kwamba hii ni kitu cha mwanzo tu, kama kitu cha mwanzo cha kuanza lazima kitaleta tabu.

Lakini mimi nasema kwamba sheria hii imeshazeeka na wala si ya mwanzo, kwa sababu tokea mwaka 2010 hadi hivi sasa, hivyo ni vyema nimuombe Mhe. Waziri kwamba sheria hii aifanyie marekebisho na tuletewe hapa na sisi tuipe msasa, ili iwalettee faida wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nimueleze Mhe. Waziri atakapoifanyia marekebisho Sheria ya Uvuvi, basi lazima awatafute wadau hawa wenye kushughulika na shughuli za uvuvi, kwa ajili ya kupata maoni yao na sheria hiyo iwape haki sana wavuvi. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 22, ambapo hapa ametuambia ni ng'ombe wawili tu ambao wamenunuliwa na Mhe. Spika naomba ninukuu kidogo.

Ukurasa wa 22 kifungu cha 5(2) (b) ambapo kinaeleza hivi:-

“Kazi za ujenzi wa uzio wa ukuta katika Kituo cha Upandishaji Ng'ombe kwa sindao imeanza na madume bora mawili ya mbegu yamenunuliwa”...

Mhe. Spika, hapa nimuombe Mhe. Waziri kwamba haya madume ya mbegu hayatoshelezi kwa sababu wafugaji wetu ni wengi. Kwa hivyo, wizara yake iongeze kununua madume ya mbegu, ili wafugaji wetu wapate mbegu kwa ajili ya kuzalishaji wa bora wa ng'ombe.

Halafu Mhe. Spika, pia nimuombe Mhe. Waziri katika Shehia ya Matembwe Kijini, Nungwi kuna mgogoro ule na wala sijui umefikia wapi na nimuombMhe. Waziri wakati atakapokuja anieleze kwamba mgogoro ule umefikia wapi, kwa sababu kuna tetesi zinasema mgogoro ule umesababishwa na Mkurugenzi wa Uvuvi. (*Makofi*)

Sasa ikiwa Mkurugenzi wa Uvuvi anasababisha migogoro hiyo na wala sidhani kama itakaa sawa, hivyo nimuombe Mhe. Waziri aje atufafanulie migogoro ile imefika, imesababishwa. Kwa kweli chanzo baada ya kuitwa kule wanakikiji hao katika hizo shehia nne, kutokana na eneo la Mnemba, baada ya kukusanywa wana vijiji wale walikubaliana, baada ya kukubaliana Mkurugenzi aliwaendea kinyume. Walikubaliana kila mwaka wapatiwe mapato. Sijui Mhe. Waziri hili unalijua au kama hulijui ulifanyie kazi ili ulijue na uwafuate wana Shehia yao kuweza kulijua hili suala.

Suala hili limezua mgogoro mzito hasa kwa kuongezwa na hizi shehia nyengine. Hapa niulize Mhe. Waziri ni sababu zipi zilizopelekea kuongezwa Shehia nyengine baada ya Shehia ya Kijini, Nungwi ikaonekana ile haifai zikaongezwa nyengine. Tunaomba utuelezee.

Mhe. Spika, niende katika wafugaji wetu. Wafugaji wetu wana kazi ngumu na serikali iwasaidie. Wafugaji wa ng'ombe Kamati yetu tunapokwenda kuwaangalia ng'ombe hawatizamiki utasema mgonjwa wa Ukimwi. Sijui kabla ya kuwakabidhi wafugaji wetu hawa ng'ombe sijui taaluma gani mnazowapa au mnawapa taaluma hawafahamu au vipi. Ng'ombe anakuwa hana siha ya aina yoyote, kabananaa. Mhe. Waziri uwafuatilie wafugaji wetu mara kwa mara uwape taaluma. Kwa sababu pengine taaluma wanapewa lakini mambo mengi yanawatoka. Ufuatilie wataalamu wako mara kwa mara wapewe taaluma hizo.

Mhe. Spika, nije katika ufugaji huu wa kuku nao pia vile vile upungufu mkubwa wa taaluma ndio unaosababisha wananchi wetu wakifuga kuku wawe wanakufa haraka haraka hasa kwa vifaranga, na hauendelei ufugaji wao na hauna tija ya aina yoyote. Kwa maana hiyo wizara yako ijipange upya ya kuwahakikisha kuwapatia mafunzo wafugaji wetu.

Mhe. Spika, niende kwa wakulima mwani, wakulima hawa wana kazi mno. Tulikwenda Pemba tukawaangalia wakulima wa mwani kuna mzee mmoja alisema wazee wote wameshafanya hijabu kwa ukulima wa mwani. Mhe. Waziri wakulima wa mwani wana kazi kubwa ukilinganisha bei ni ndogo. Kwa hivyo Mhe. Waziri wizara yako ifanye utafiti ili iwaongeze wakulima wa mwani bei ya mwani.

Vile vile niombe serikali huu mwani tunasikia unatengenezwa juisi, keki, vipodozi na mambo mengine. Mhe. Waziri hawa wakulima wetu wa mwani tuwape taaluma na humu mmelezea kuwa watatafutiwa viwanda vidogo vidogo, kwa maana hiyo watafutiwe na wao hivyo viwanda ili wapate mapato yanayostahiki na kazi zao. Kazi ya mwani ni ngumu mno. Mhe. Waziri wewe mwenyewe huwezi kuifanya kazi hiyo ya mwani, ngumu.

Mhe. Spika, ukilinganisha kazi ya mwani na kipato ni kidogo mno, basi serikali hili suala la uuzaji wa mwani baada ya kuwa inawapa sekta binafsi hebu kwanza hili ilibebe hii serikali, ihakikishe kuwa na wakulima wa mwani wanafaidika.

Mhe. Spika, baada ya hayo ahsante sana nakushukuru.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kwa kutujaalia leo kufika hapa na kujadili bajeti ya Wizara yetu ya Uvuvi. Vile vile nakushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia leo. Pia nampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kukipanga kitabu hiki.

Mheshimiwa mimi naanza katika Sekta ya Uvuvi. Mhe. Spika, nchi yetu ya Zanzibar ina wavuvi wengi na wengi ni wavuvi masikini. Serikali inawahimiza sana wananchi wajiajiri katika sekta nyingi sana na hasa sekta ya uvuvi. Lakini wavuvi wetu wa Zanzibar hawana uwezo wala hawana vifaa vya kuweza kufanya shughuli hizi za uvuvi ili kwa kujipatia ruzuku.

Naiomba serikali kupitia Wizara ya Uvuvi Mhe. Waziri wa Uvuvi ajitahidi sana kuwawezesha wavuvi wetu ili kuwakopesha boti na zana za uvuvi. Sheria yetu ya kuweka Mazingira ya Bahari inakataza nyavu ndogo ndogo, na wavuvi wetu wa Zanzibar wengi uwezo wao wa nyavu ndogo ndogo. Hawawezi kwenda kuvua bahari kuu kwa sababu hawana vyombo vya kuvulia. Naiomba Wizara iwasaidie wavuvi zana za kuvulia, iwawezeshe wavuvi wetu zana za kuvulia kama boti na nyavu nyengine ambazo zinahusika katika sheria yetu inayoruhusu uvuvi halali.

Nikienda katika jimbo langu la Matemwe ni asilimia 70 ni wavuvi tena ni wavuvi wanyonge; ambao hawamiliki zana za bahari kuu, zana zao ni hizo hizo za kuvua bahari ndogo ndogo. Naiomba Wizara iwafikirie sana wavuvi, hususan wavuvi wa Matemwe ni wavuvi ambao ni wanyonge hawawezi kuvua bahari kubwa zinazosemekana hivi sasa ukavue kwa meli. Bahari kuu huwezi kuvua isipokuwa uvue kwa meli. Naiomba wizara iwafikirie sana hususan wavuvi wa Matemwe ambao bado wapo katika kumbukumbu za unyonge.

Mhe. Spika, nikienda katika huduma za utibabu wa mifugo. Serikali iliwahimiza sana wananchi wafuge kama kuku, mbuzi, ng'ombe, lakini wananchi wetu wengi hawana uwezo sasa hivi wa kuweza kununua hii mifugo, hawana uwezo wa kuilishia, wala hawana uwezo wa kununua dawa. Naiomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo Mhe. Waziri awafikirie sana kuwakopesha wananchi wetu mifugo. Wakikopeshwa mifugo wananchi wanakusanywa; kwa mfano ushirika wa watu ishirini wanapewa mbuzi watatu au kuku hamsini. Kweli watakwenda?

Kwa hivyo naiomba Wizara ijikite hasa kuwakopesha wananchi na kuwaelimisha wananchi mifugo, wapewe elimu ya mifugo na dawa za mifugo, mifugo yetu inateketea kwa sababu haina dawa. Naiomba wizara ilianganalie sana jambo hili.

Vile vile, Mhe. Rais wetu katika kuwatembelea wananchi; wafugaji na wakulima walitembea katika sehemu moja katika jimbo langu la Kambi, alimtembelea kijana mmoja anaitwa Ame Khamis. Kijana yule ana kuku wengi lakini huduma zinamshinda kwa sababu mnyonge, kijana yule alipokwenda Rais alimuomba apatiwe huduma ya umeme, kwa vile Rais alimkubalia lakini bado kijana yule katika kufuatilia kwake amechoka hivi sasa. Kwa hivyo namuomba Waziri amkumbuke kijana yule aliyekwenda kutembelewa na Rais pale Kambi amuonee huruma kile alichokiomba kwa Mhe. Rais wamtekelezee.

Mhe. Spika, ili nisipoteze wakati wako nakwenda katika mazao ya baharini, kama wenzangu walivyosema kwamba kuna wazee wetu wafunga mwani. Mwani Mhe. Spika, ni kazi kubwa sana tena ni kazi ambayo inakondesha. Ukimkuta mfunga mwani alivyokonda basi tutamuonea huruma. Ningelimuomba Mhe. Waziri wafunga mwani nao wafikiriwe kuongezewa bei ya mwani. Kwa sababu ni moja katika ajira kubwa sana kwa wazee wetu hususan wanaoishi Matemwe, Nungwi na kwengineko, sehemu yoyote ya bahari yetu hii wafunga mwani hivi sasa wamekuwa wengi sana. Namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana kuwafikiria akina mama wanaofunga mwani.

Mhe. Spika, bila ya kupoteza wakati, *wakati ni mali*; namuomba Mhe. Waziri amuhudumie yule kijana ambaye niliyemtaja hapa, aliyetembelewa na Rais ana kuku wengi sana na ni kijana mzuri sana kwa kufuga, lakini anashindwa kujiendeleza kwa sababu ni mnyonge. Namuomba Mheshimiwa Waziri namkumbusha sana na Mhe. Waziri Said Ali Mbarouk aliwahi kufika pahali kule na anamjua. Mhe. Said Ali Mbarouk kwa ujasiri wake haidhuru hii Wizara amepewa mtu mwengine lakini analijua hilo na atashirikiana na Mhe. Waziri Jihadi, watakwenda kumfikiria kijana huyo. Yule kijana Mhe. Waziri Jihadi kama hamjui mimi namuomba tukimaliza kikao cha Bajeti nimpeleke kwa kijana yule akamuone.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia wakati wako naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Mifugo, mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti ya Wizara ya Uvuvi. Kwanza nianze na sekta ya mifugo kwa kufuata kitabu chetu hichi cha mapitio ya hali ya uchumi na utekelezaji wa mpango wa maendeleo Zanzibar. Kuna eneo katika ukurasa wa 73 linaelekeza kwa kuzingatia malengo ya Mkuza II, sekta hii inalenga kutekeleza lengo la pili la kuwa na uchumi endelevu na wenye kujali masikini.

Vile vile sekta hii imepanga kufikia shabaha ya kuongezeka mifugo na bidhaa zitokanazo na bidhaa zenye ubora. Mchango wa sekta ya mifugo kwenye pato la taifa umepungua kutoka asilimia 4.7 mwaka 2010/2011 hadi kufikia uzalishaji wa asilimia 4.2 mwaka 2011/2012 na kuelekea.

Mhe. Spika, tukiangalia takwimu hizi za wenzetu ndizo hasa zinazosababisha kuweza kuwapata wale wageni ambao wanakuja katika nchi yetu na kuweza kusaidia uletaji wa kuku ambao wamekuwa tayari wamekamilika. Tukiangalia mahitaji ya kuku katika visiwa vyetu vya Zanzibar ni zaidi ya asilimia 120. Lakini uzalishaji wa kuku hawa ambao wananchi wetu wanafanya si zaidi ya asilimia 50. Mimi ningelipenda kutoa wito maalum kwa Mhe. Waziri ili atusaidie kwa wafugaji wetu tulionao ndani ya nchi ya Zanzibar kwa ujumla wake, tuwasaidie uwezo, tuwasaidie taaluma na tuwasaidie mambo mengine yote ambayo yanalazima kwa upande wao, ili na wao waweze kuingia katika soko hili katika misingi ya kuweza kushindana na wale watu wanaoleta kuku katika nchi zetu za Zanzibar.

Mhe. Spika, la pili nichangie ukurasa wa 6, Mhe. Waziri alipofika hapa alitwambia katika sekta ya uvuvi kwamba sekta hii imekuwa na uwezo wa kuzalisha tani 25,693 kwa mwaka 2010/2011 na tani 28,759 mwaka 2011/2012. Pamoja na uzalishaji huu ambao tunaendelea nao sijui Mhe.

Waziri ana mikakati gani ya kuweza kuona hawa wavuvi ambao wanafanya uzalishaji wa samaki hawa wakasaidiwa wakaweza kuondokana na umasikini, ambao unaendelea kuwakabili na kuweza kuwatafutia soko hadi nje ya nchi ili waweze kuendelea kuzalisha samaki zaidi au kuvua samaki zaidi na kuweza kuwauza nje na kuwatosheleza wananchi ndani ya nchi yetu.

Jengine naelekea katika ukurasa wa 65 wa kitabu chetu hichi, kuna eneo katika jaduveli letu ambalo tunalo hapa, Utekelezaji Halisi wa Mwaka 2011/2012 hadi kufikia mwezi Aprili 2012 kazi zifuatazo zilikuwa zimekamilika. Katika kazi zilizokamilika katika ukurasa wa 65 (1) tunasema kwamba kuna vifaa vya kutendea kazi mbali mbali vya maabara vimenunuliwa. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje atuthibitishie je, vifaa hivi pamoja na kununuliwa vimeshafungwa kwa ajili ya matumizi haya ambayo yamelengwa tukaweza kupoteza hata ule uhalali wa kuweza kuuona kama vile vifaa vina kasoro tukaweza kurejesha katika ule muda wa *guarantee* uliowekwa ili tuweze kubadilishiwa na kuletewa vyengine.

Eneo jengine ni ukurasa wa 67. Katika ukurasa huo malengo ya mwaka wa 2011/2012, mradi ulikuwa na malengo yafuatayo. Pamoja na malengo yaliyokuwa yamepangwa Nam. 2 wamesema ni kufanya mapitio ya sheria ya haki za wanyama. Je, nataka Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuelekeze, malengo haya katika kupitia sheria hizi za haki za wanyama yalifikiwa katika mwaka huu mwaka ule ambao tunamalizia.

Mhe. Spika, jengine tunaelekea katika ukurasa wa 68, katika utekelezaji halisi mwaka 2011/2012, Mhe. Waziri atakapokuja hapa tutaomba utusaidie hapa kidogo. Nam. 4 inasema kwa kushirikiana na wafugaji mbwa 262 wamefungwa uzazi. Hebu tusaidiane lakini paka waliofungwa uzazi ni 435, malengo ni nini, kwamba wanyama hawa baada ya kipindi fulani wasikuwepo tena au kitu gani. Mhe. Waziri utakapokuja hapa tutaomba utusaidie zaidi.

Baada ya maelezo hayo sasa niseme mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kikwajuni naomba kuuliza swali moja atakapokuja Mhe. Waziri hapa, lile soko la samaki katika eneo la Kizingo je, litakamilishwa lini kujengwa au serikali ina mpango gani juu ya soko lile la samaki. Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii fupi ya kuchangia kidogo katika bajeti hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Kabla yote Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri na Mhe. Viwe Khamis Abdalla yeye kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Utalii, Uwezeshaji na Habari, kwa namna wote wawili walivyowasilisha taarifa zao vizuri kwa ufasaha na kufahamika.

Mhe. Spika, nianze kwa sababu wizara hii moja kwa moja ni Wizara ya kitaalamu na mambo yake ni ya kitaalamu, naomba moja kwa moja nianze kwenye kiambatanisho Nam. 3 na 4 ikiwa kwenye ukurasa wa 64

Mhe. Spika, kiambatanisho Nam. 3 kinaonesha orodha ya Wafanyakazi katika Wizara ya Mifungo na Uvuvi, *colum* ya pili chini kwenye kiambatanisho hichi ambacho kinahusiana na Idara ya Mipango Sera na Utafiti kwa Pemba jumla ya wafanyakazi waliokuwemo ni watatu na

wote ni wanaume hakuna mwanamke hata mmoja. Ningeliomba kujua hakuna uwezekano wa kumpata mtaalamu wa kike na yeye akaingia katika Idara hii. Kwa nini Idara nzima iachiwe wanaume watupu.

Mhe. Spika, tukija katika kiambatanisho Nam. 4 ambacho kipo kwenye ukurasa wa 51. Hapa imeelezwa orodha ya wafanyakazi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na viwango vyao vya elimu. Tukiangalia nambari mbili za mwisho yaani Nam. 9 na Nam. 10 tutakutia kuwa katika jumla ya wafanyakazi 739 ikiwa ndio asilimia 100 ndio wote kuna asilimia 12.7 ikiwa hawa ni darasa la 12, na kuna asilimia 37.9 hii ni asilimia kubwa hawa ni kuanzia mpaka kidato cha 3. Hawa elimu yao haizidi kitato cha 3 kwa vile hii ni wizara ya wataalamu na kwa wafanyakazi hawa waliokuwemo 739 hawa wa kundi la pili la kidato cha nne na waliomaliza kidato cha 3 ni asilimia 50.6 ni asilimia kubwa sana.

Ningeiuliza Wizara ina mpango gani wa kuwaelimisha watu hawa ili hii wizara iende kama wizara ilivyo, iwe na wataalamu wa kutosha kuliko kuachiwa katika hali hii. Tumeona hata wengine wanaojishughulisha katika matibabu ya wanyama ni wafanyakazi wa darasa la 12 kwa muda mrefu, na bado hawajapata kuendelezwa kimasomo. Hilo naomba kupewa maelezo.

Jengine Mhe. Spika, moja kwa moja niende kwenye ufugaji wa kuku. Nitaeleza yaliyokuwemo kwa ufupi katika ukurasa wa 23. Tukitizama ukurasa wa 21 kwanza utaona Idara ilikusudia kufanya mambo mengi katika kipindi cha mwaka uliopita, na moja ni kuanzisha utafiti shirikishi wa kuku katika kupata kuku wanaokuwa haraka, wanaotaga zaidi, na wanaostahamili maradhi. Katika utekelezaji katika ukurasa wa 23, tumeona kuwa utafiti shirikishi wa kuku unaendelea na hadi sasa aina tatu za kuku chotara, zimepatikana na chotara hao ni mchanganyiko wa kishingo na *osolop* halafu kishingo na *road island* na kishingo na *white leghorns*. Kwanza nataka niulize hawa kuku vishingo wana sifa gani ya pekee mpaka wakatafutwa machotara kutokana na mbebu za asili ya kiume, tofauti ni ya ulezi, ni ya kustahamili maradhi, au wana sifa gani. Lakini mradi huo wa kuku Mhe. Spika, unaendelea miaka mingi sana.

Mwanzo kulikuwa kuna ufugaji wa *white leghorns*, *road islands*, halafu hivi sasa tunaendeleza ufugaji wa kuku wa kienyeji wa kutumia madume ambayo ni mbegu ambazo zilichoguliwa makusudi ili kuweza kupata kuku wazuri. Kwa mfano hivi sasa majogoo 511 yamesambazwa kwa wafugaji Unguja na Pemba ili kuongeza uzalishaji wa kuku wa kienyeji. Hapa wenyewe wanajikita moja kwa moja kwenye vishingo tu. Kule ufugaji mwengine unakuwa unaendelea, unakuwa katika mparaganyiko, huu sijui utafiti wetu utatualizikia wapi, naomba nielezwe. Huu unaofanywa kupitia majogoo wenye sifa kutoka nje, na huu wa kutumia kuku vishingo kuna tofauti gani ni huo katika kutafuta au kutahitaji maelezo zaidi.

Halafu kwa vile ufugaji umeanza zamani na hivi sasa ndio kwanza wanaendelea na utafiti, wale waliokuwa wameshafuga zamani na kuzaa wameshazaa na kadhalika, sijui Wizara inajifunza nini, naomba nipate maelezo.

Mhe. Spika, tukija katika Idara hii ya uzalishaji mifugo ukurasa wa 22, kifungu 5.2 kinaeleza ng'ombe ambao walikuwa wazalishwe kwa njia ya sindano ilikuwa wawe 6000, lakini kutokana na matatizo ya kushuka kwa umeme kwa hivyo mtambo wetu wa kuzalisha *liquid nitrogen* haikupatikana ya kutosha huko mashamba na matokeo yake ng'ombe ambao wamezalishwa kwa sindano ni 2867 ni chini kiwango kwa asilimia kubwa sana.

Mhe. Spika, ukiangalia mtambo huu wa *liquid nitrogen* huu ni mtambo muhimu sana kwetu sisi, na bila ya huu uzalishaji hakuna. Hapa hapo nyuma uzalishaji ulikwama kwa sababu ilikuwa hatuna hii *liquid nitrogen*. Katika taarifa ya kitabu hichi ni kuwa mtambo huu umetengenezwa mara mbili au umefanyiwa matengenezo mara mbili na wataalamu wanakotoka huko unakotoka mtambo wenyewe.

Mhe. Spika, mimi hapa nina maswali mawili. Kwanza hii hali iliyozungumzwa ya kushuka kwa kiwango cha Umeme hakiathiri ule mtambo wenyewe ikiwa umeme utashuka. Maana kuna vifaa vyengine umeme ukishuka na kupanda vinaathirika. Huu mtambo ambao ni wa ghali sana ni vipi. Mtambo huu ni wetu wenyewe na upo si muda mrefu sana lakini umeshatusaidia sana. Nilipoona kuwa mafundi waliokuja ni kule ulikotoka mtambo kuja kufanya matengenezo mara mbili katika mwaka huu uliopita. Je, Wizara haioni kuwa kuna ulazima wa kuhakikisha kuwa wanapeleka watu wao kujifunza kuhusu mtambo huu ili ikitokea dharura yoyote wenyewe waweze kushughulikia badala ya kungojea wataalamu kutoka nje, hilo ni swali na naomba nipate jibu.

Mhe. Spika, jengine nililoliona katika kitabu hichi ni kuwa kuna maeneo ya karantini, kuna Kisakasaka na sasa hivi kuna na sehemu nyengine ambazo zinaendelea katika shughuli ya upimaji. Kisakasaka shamba lile kwa mujibu wa kitabu ni kuwa wamefyeka au kusafisha eka 60 tu kati ya 100. Ninavyojua lile shamba ni kubwa na ninavyojua lile shamba limevamiwa sana. Halafu vile vile Wizara inatafuta maeneo mengine ya karantini.

Swali langu je, matatizo ya shamba lile yamemalizika, lote limekuwa letu, wale watu waliohamia na wengine walikuwa wanatishia hata kuondoka lakini wameondoka. Halafu haya mengine wana mpango gani na wizara husika kutokana kuwa moja katika wizara inayohangaikia hati miliki ni hii na sehemu nyingi hawana hati miliki. Kwa haya maeneo mengine mawili ambayo wanataka kuyafanya kuwa ya karantini.

Kule Pemba eneo ambalo limechaguliwa kuwa karantini ni eneo la Nziwengi ni la muda mrefu. Sijui kwa nini mpaka leo kuwa kunaendelea na shughuli ya upimaji ikawa hatua hazijachukuliwa.

Jengine Mhe. Spika, ambalo naomba kulizungumza ni kuwa kuna ufugaji huu wa samaki. Mimi jambo linalonisikitisha sana ni kuona kuwa mashamba darasa ambayo ni muhimu sana yote yapo Pemba, sijui kwa nini mpaka leo hapa Unguja hapajawekwa shamba moja darasa, kwa vile kuna ufugaji mkubwa wa samaki na wenzetu wakienda wakachukua mafunzo wanaweza wakahamasika kwa kutumia mashamba hayo. Hii mimi ningeliomba kwa hapa tutumie sera yetu ya haki sawa kwa wote tuone kuwa ndugu zetu Unguja wamepata hili shamba darasa.

Mhe. Spika, ufugaji wa samaki ni kazi ngumu sana, kazi ya kuchimba mashimo na kufuga samaki ni kazi ngumu sana na wanaofanya kazi hii ni masikini. Lakini baada ya kufanya kazi kubwa sana mwishoni hua wanakwama kwa kukosa misaada ya lazima. Kama majenereta na kadhalika ya kutolea maji nguvu zile kuwa hawana.

Halafu kuna tatizo jengine kubwa ambalo linajitokeza kwa sababu watu wetu wamehamasishwa na kuhamasika, bahati nzuri huingia tu katika maeneo bila ya kufuata taratibu za awali zinazohusika, kama vile kuonana na watu wa mazingira ili wakakubaliana na kupewa idhini ya

kufanya hiyo kazi humo wanamofanya hayo mashimo yao ya kufugia samaki kutokana na kuwa ni sehemu ambazo ni sehemu za wazi kwenye mikandaa. Kwa maana hii husababisha wakati mwengine kufanya kazi ambayo haina tija.

Mimi ninaloomba kwa vile shughuli hii huwa inafanywa sana, na ni lazima ifanyiwe kwa kule Pemba Mikandaani, na ni mbali na watu kwenye mikoko wengine wanasema pia ni sawa na watu wanaachiwa tu wanajiendeleza na shughuli hizi. Ningeliomba Wizara ifuate nyayo za Mhe. Said Ali Mbarouk kuwa mfuatiliaji wa kweli kule sehemu ambazo watu wanatumia nguvu zao ili nguvu zao zisije zikapotea bure.

Mwisho Mheshimiwa kwa sababu hii ni kazi ya kitaalamu na Kamati ya Mifugo, Utalii Uwezeshaji na Habari ni Kamati inayoshughulikia pia Wizara hii. Wizara hii nashukuru sana imepeleka watu wengi nje kwenda kusoma mambo ya ufugaji na kadhalika. Lakini hiyo Kamati inayofuatilia ambayo ni Kamati hamasishi kama ingelikuwa inatoa taaluma hakuna hata moja aliyekwenda hata hapo Baraza kuangalia mambo yanavyokwenda.

Kwa hivyo kwa niaba ya Mwenyekiti, naomba kama wizara itakavyojiweza ione kuwa hawa Wajumbe wa Kamati hii, wanakwenda kama Wajumbe wa Kamati nyengine kupata taaluma ya ufugaji wa samaki na mambo mengineyo, pamoja na wafugaji wa wanyama ili wakija hapa wasiwe ni wanakamati tu, lakini waweze pia kuisaidia jamii katika shughuli zao. Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, nami kwanza kabla ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) aliyeniwezesha kusimama hapa kwa uwezo wake. Huu si uwezo wangu wala nguvu zangu wala akili yangu ni neema yake Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, nataka kumshukuru kusema *Alhamdulillah*. Vile vile Mhe. Spika, kama sikukushukuru wewe nitakuwa si mwingi wa fadhila kuniruhusu kuzungumza mawili matatu.

Mhe. Spika, mimi nianze moja kwa moja kwenye ukurasa wa 34 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi. Mhe. Spika, hapa nitaomba ufafanuzi kidogo juu ya maendeleo ya Idara ya Uvuvi kuwa maendeleo haya yanahusu uvuvi au yanahusu idara yenyewe? Hoja yangu ya msingi ninayotaka kuchangia Mhe. Spika, nataka kufahamu wavuvi wadogo ni wepi na wakubwa ni wepi. Kumekuwa na kilio kikubwa kwa wavuvi wadogo hasa wavuvi wetu wa dagaa aina ya saladini, ukuzi na vibua.

Mhe. Spika, hawa wamepigwa marufuku kutumia nyavu za macho madogo watavua vipi hawa watu na hiki ni kitendo cha mnyonge wa hali ya chini. Sasa Mhe. Waziri atapokuja naomba anisaidie, watumie aina gani za zana hizi za kuvulia. Hawa ni wavuvi wa aina ya chini kabisa Mhe. Spika.

Baada ya hapo naomba Mhe. Waziri pia anieleze kuna sababu gani za kuzuia wavuvi kutumia viatu vya kuogelea, *oxygen*, mitungi ya gesi wanayobeba huku nyuma wakati watalii wanaruhusiwa kufanya vitu hivyo. Pana umakini gani hapa Mhe. Waziri, wakati wananchi ndio ajira yao wanayotafutia riziki zao leo watalii ambao si wenye nchi wanatumia vitu kama hivi, kweli pana uyakinifu kiasi gani hapa Mhe. Spika.

Nikitoka hapo kidogo nije katika huu Mradi wa *MACEMP*, huu umekuwa ni gumzo kweli kweli na hapa mimi nafikiri ipo haja kamati yako Mhe. Spika, kwenda kuangalia uhalali wa miradi hii, kuunda tume makusudi, miradi inakuja waheshimiwa wale wanaohusika hasa kupewa vile vitendea kazi hawapati wananufaika watu wengine ambao hawahusiki. Hapa ni pazito kweli kweli Mhe. Spika, wale walengwa wa ule mradi hawapati wanakwenda kuneemeka watu ambao hakulengwa na mradi huu.

Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi nitahitaji maelezo ya kina akija Mhe. Waziri kuhusu wananchi wa Jimbo la Muyuni wamepewa boti, lakini kwa masikitiko makubwa baada ya muda boti ile imechukuliwa kupelekwa Kizimkazi, imehusu nini Kizimkazi na Muyuni. Hapa Mhe. Waziri huu ni wakati wa Mwezi wa Ramadhani kuzuwia kifungu nitafanya makosa lakini hapa kidogo nitakaza nati ili nipate maelezo ya kina kabisa Mhe. Waziri kwa nini wananchi wa Muyuni wamenyang'anywa boti ile na ikapelekwa Kizimkazi. Je walikuwa hawana haki wananchi wale wa Muyuni kupewa boti ile ya uvuvi, na suala hilo ni la muda mrefu karibu mwaka mmoja unakaribia toka enzi za Mhe. Said Ali Mbarouk. Kilio hiki tumekwenda Mhe. Said akatumia hekima zake na maneno yake na tukafika pahali lakini bado kimekuwa kizungumkuti.

Sasa hivi Mhe. Spika, nije katika suala la Mifugo. Sasa hivi wafugaji wetu wamekuwa na mitihani, mtu anafuga ng'ombe, kuku kama hakuweka mlinzi basi hapati kitu, wizi umekuwa wa hali ya juu lazima uweke mlinzi kwenye banda. Kwa hivyo, nashauri kwa masheha na maafisa wa kilimo watumie zile sheria za kuleta vyeti kama vile zamani, wananchi wetu wanapata shida kuhusu wizi wa mifugo.

Jengine kuhusu punda wamekuwa wakiteswa sana hasa katika Jimbo la Mji Mkongwe, wanabebeshwa mizigo ambayo haiwezi kuibeba kwenye magari, matofani yamekuwa mengi yanapitishwa kwenye vichochoro vya Mji Mkongwe kuliko uwezo wake wanaobeba punda mizigo.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Spika, kwanza napenda kukushukuru kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii. Pia nampongeza Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wake kwa kuandaa hotuba hii ambayo ni nzuri.

Mhe. Spika, mimi napenda nichangia katika ukurasa wa 71 kifungu nambari moja naomba uniruhusu ninukuu, “ufuatiliaji wa mradi kwa vikundi 322 umefanyika katika miradi ya jamii kwa Unguja na Pemba. Aidha, tathmini iliyofanywa imebainika kuwa, asilimia 85 ya mradi wa uvuvi, ufugaji wa kuku, ufugaji wa nyuki, uhifadhi na utunzaji wa mikoko na miradi ya mbuzi wa maziwa inafanya vizuri. Hata hivyo, kwa baadhi ya miradi ya uvuvi bado haijafika malengo yaliyokusudiwa kwa sababu ya upungufu wa samaki wanaotokana na uvuvi haramu”.

Sasa hapa ningejaribu kumuuliza Mhe. Waziri kwanza katika hivyo vikundi 322 ningeomba anieleze kwamba, ni vikundi vingapi ambavyo viko hai na hasa nimelenga katika vikundi vile vyenye miradi vilivyopewa boti na nyavu katika shehia mbali mbali kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, nataka Mhe. Waziri anieleze ni shehia ngapi au vikundi vingapi wamepewa nyavu hizo na vingapi viko hai, vingapi vimekufa na katika vilivyokufa kuna changamoto gani ambazo

zimewakabili katika vikundi hivyo. Vile vile wizara naomba inieleze katika kujipanga itatua vipi changamoto hizo ili kuisaidia jamii waendeleo katika shughuli zao za kunyanyua hali zao za maisha na hatimaye kupunguza umasikini katika hali zao.

Jengine Mhe. Spika, miradi ya jamii ambayo inaanzishwa inategemea na ufuatiliaji wa karibu. Mradi unakuwa hauko endelevu kwa sababu aidha inakuwa ufuatiliaji wake unakuwa ni mdogo, ukifuatilia mradi kwa karibu kwa mfano ukijipangia taratibu za kufuatilia utakuwa unajua zile changamoto ambazo zinawakabili wananchi wale. Aidha, changamoto zile unakuweza kuzitatua kwa kipindi kifupi ambapo utakuwa unafuatilia. Kwa mfano ukiweka mradi na utakuwa huufuatilia ina maana unapelekea ule mradi kufa kabisa.

Kwa hivyo, ninachoshauri hapa wizara Mhe. Spika, iwe na ufuatiliaji wa karibu kabisa katika hii miradi ambayo imeanzishwa kwa wananchi na ukiangalia mradi wa *MACEMP* imeanzisha miradi mingi sana kwa wananchi, miradi ya uvuvi, miradi ya kuku, miradi ya ufugaji, kwa hivyo inakuwa inakosa kuendelea kutokana na aidha pengine wafadhili wale kuondoka kabisa wakaacha kuwa hawapitiwi na pengine huo ufuatiliaji niliosema wa karibu. Kwa hivyo, wawe wanafuatilia kwa karibu sana ili kusaidia hii miradi iwe endelevu na wananchi wetu nao wanufaike kwa miradi hii ili kuendeleza hali zao za kiuchumi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Uvuvi na Mifugo ya Mhe. Waziri Abdillahi Jihadi Hassan.

Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka niungane na wenzangu kuzungumza suala la mifugo. Mhe. Spika, kipindi kilichopita nilizungumza katika kama mnapotoa mifugo basi tuangalie mifugo ili kukuza watu wetu katika hivi vikundi vya mifugo na nilizungumza kama huwezi kumpa mtu mbuzi ambaye ni beberu usimpe mbuzi mke. Kwa sababu ukimpa beberu tupu atafanyia nini, lakini unampa mbuzi mke na beberu kwa ajili ya kuwa wazalishe sasa na tuliambiwa kwamba wizara imejipanga kutoa mbuzi wa maziwa ili kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu, lakini naona mpaka leo sijaona mbuzi hata mmoja kule Jimboni kwangu Micheweni wa maziwa. Ikiwa ni ufugaji wa mbuzi Micheweni basi naweza kusema kama inaongoza, kwa sababu Micheweni hasa ndiko kunakofugwa mbuzi, karibu wengi walioko Pemba wanatowelea kitoweo cha mbuzi kwa kupitia micheweni.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kama huu mpango wa kufuga mbuzi wa maziwa upo basi awaone wananchi wa Micheweni kama wao ni wafugaji wazuri wa mbuzi na waweze kupatiwa hawa mbuzi kwa ajili ya mifugo.

Mhe. Spika, suala jengine nitakalozungumza ni suala la ufugaji wa samaki. Mhe. Spika, tuna vikundi vingi vya ufugaji wa samaki na wizara kila ikija mnatueleza kwamba kuna ufugaji wa samaki. Kipindi kilichopita nilisema na leo nasema tena, kwamba ufugaji wetu wa samaki bado hatujawekeza ufugaji wa samaki wa kuleta mapato katika nchi yetu, tunafuga samaki wa vitoweo tu na samaki wa kitoweo hawezi kumuendesha mwananchi wakamsaidia, kama si samaki wa kitoweo anambie Mhe. Waziri kama kuna wafugaji gani wamezalisha samaki wakauza kwa ajili ya kipato cha kutosha na wakaonekana kwamba hawa ni samaki wameuzwa

wa mifugo. Kwa hivyo, tujue je, ni tani ngapi atwambie Mhe. Waziri tumeuza za samaki hawa wa kufuga. Kwa maana hiyo, mimi namwambia Mhe. Waziri kama tunataka kufuga samaki tuzalishe samaki wa mifugo tuwawezeshe wananchi wafuge samaki wa biashara sio samaki wa kitoweo hawamsaidii mtu hao.

Mhe. Spika, suala jengine ninalotaka kuzungumza ni suala la wavuvi wetu wanaokwenda wakivua dago Dar es Salaam, wanatoka wavuvi hapa Zanzibar wanakwenda kule kuvua, lakini linalowapata wavuvi wetu wanateswa sana kwa kukamatwa ovyo ovyo kuwa hawana leseni, wanapoonsha leseni za Zanzibar wanakataliwa wanaambiwa hizi hatuzijui kamwe. Kwa hivyo, nataka atwambie Mhe. Waziri atawasaidia vipi wavuvi wetu wakienda kule ili wasipate mateso kwa sababu wananyanyaswa sana na mateso ya kukamatwa kamatwa. Kwa hivyo atueleze Mhe. Waziri ni kweli uvuvi mdogo mdogo si Muungano lakini hii nchi ni ya Muungano, basi wale wavuvi wetu wanapoteswa atwambie atachukua juhudi gani kuona kwamba wavuvi wetu hawateswi. Hilo ni suala jengine.

Suala jengine Mhe. Spika, ni suala la wavuvi wadogo wadogo. Mhe. Spika, hili limekuwa ni suala sugu sana, sote ni mashahidi kwamba wavuvi wetu wametoa ajira kwa wananchi wa Zanzibar walio wengi na atakae aone kuwa uvuvi umetoa ajira na aende pale Malindi akaangalie ni wananchi wangapi waliopo pale Malindi wanaopata ajira kutokana na uvuvi, aangalie ni wachuuzi wangapi wanaojijiri kutokana na uvuvi, ni wanawake wangapi wanaopika chakula na kupata ajira kwa ajili ya uvuvi. Leo Mhe. Spika, wavuvi wetu tunawatesa wavuvi wa Zanzibar hawana haki ya kukaa kama wamo katika nchi yao inakuwa tunawapa mateso ya hali ya juu. Kwa sababu haujulikani uvuvi haramu ni upi na uvuvi halali ni upi.

Leo Mhe. Spika, watu wanavua *ring net* anaambiwa ni uvuv haramu mtu huyo anakwenda majini anachukua kioo anaambiwa ni haramu, utamuonaje samaki chini, baharini mna mambo mengi ya hatari, kuna samaki wanafuma, mna masamaki makubwa yanaweza yakakula, leo ukienda kama hukuvaa kioo uharamu wa kioo ni nini tuambiwe. Mhe. Waziri akija atueleze uharamu wake kioo ni nini, kwa sababu mvuvi hawezi kwenda majini kama hana kioo, leo unamwambia mtu kama asivae kiato mana akivaa kiato cha kuvulia, cha kuogelea ni haramu, leo anakwenda baharini mtu wakati hana kiato wakati yeye anavaa kiato kile kwa ajili ya kuwa samaki mkubwa akija aone kwamba huyu hana umbo tena la binadamu ana umbo la samaki akishavaa kile kiato, samaki hawezi kumzuru leo mnataka avue viatu akienda kuzama kule aliwe na samaki. Kwa hivyo uharamu wake ni nini?

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba tangu nilipofahamu mimi huwezi kumkamata pweza bila ya kumchokoa, leo samaki au pweza ukienda ukimchokoa utaambiwa ni haramu akamatwe vipi na pweza anakaa kwenye majumba yam awe, wako chini kwenye mawe utampataje ama hatutaki tena kula pweza watalii wakija wasipewe tena, je kama wamo ndani yam awe wavuliwe kwa nini. Pweza havuliwi kwa utupa anavuliwa kwa kuchokolewa sasa tuambiwe uharamu wa kumchokoa pweza ni upi.

Suala jengine ni suala la bunduki, kama samaki ukienda ukipiga bunduki basi inapiga samaki anayepita mmoja mmoja na huwezi kupiga samaki mchanga kwa bunduki humpati lazima upige samaki aliyekuwa ni mkubwa. Leo ukimfuma ni haramu jamani uharamu huu unatoka wapi.

Mhe. Spika, suala jengine naomba uniruhusu ninukuu karatasi hii. Mhe. Spika, kuna wavuvi ambao walikamatwa Chwaka kwa kuambiwa kuwa wamevua uvuvi haramu walipokamatwa wavuvi hawa ikabidi mitego yao ikikamatwa inatiwa moto, wao wakasema aa sisi tusitiliwe moto mitego yetu tupelekwe Mahkamani kwa sababu Mahkama ndio itakayokwendaamua. Wavuvi walichukuliwa wakapelekwa Mahkamani walipopelekwa kule wakachukuliwa na vielelezo vyao na mitego yao, walipokwenda Mahkamani Mhe. Spika, naomba ninukuu karatasi hii, lakini mengine nitayaacha, inasema kwamba:

“Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mahkama ya Mkoa Mwera, Mhe. Spika, Mahkama iliamua tarehe 9/02/2012 kwa yeyote anayehusika alipelekwa barua hii na Mahkama, kuhusu kesi ya jinai yenye Nam. 430 mshtakiwa Abdalla Makame Mwelezi husika na mada iliyotajwa hapo juu, washtakiwa waliotajwa hapo juu walishitakiwa mbele ya Mahkama ya Wilaya kwa mashtaka ya kuvua uvuvi haramu. Kifungu 21(1)(b) na kifungu 27 (c) na Kigungu 30(1) cha sheria ya uvuvi Nam. 7 ya mwaka 2010, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mahkama baada ya kusikiliza ushahidi kutoka kwa washtakiwa imeamua kwamba washtakiwa hawana kesi ya kujibu. Hivyo, wanaachiwa huru chini ya kifungu Nam. 214 cha sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai, sheria Nam. 7 ya mwaka 2005. Kwa barua hii unatakiwa uwakabidhi washtakiwa vifaa vyao vyote vilivyokamatwa kwa ajili ya vielelezo vya kesi hii. Imetiwa saini na Mahkama leo tarehe 9/02/2012”.

Mhe. Spika, cha kusikitisha ni kwamba Mahkama ishaamua kama hawa watu washakwenda huko washashinda kesi na ishaamua Mahkama watu wapewe vitu vyao vyote vilivyokamatwa, leo Mahakama mpaka hivi ninavyozungumza Mhe. Spika, watu hawa hawakupewa vitu vyyao na wakati Mahkama imeshaamua. Je, huku kwanza sikuidharau hiyo Mahkama? Sasa kama imewekwa Mahkama kwa ajili ya kusikiliza kesi sisi tuna maana gani hii Mahkama basi kama imeamua na leo watu hawapewi vitu vyao kwa nini wasipewe vitu vyao. Vitu vyao vyote hawajapewa mpaka hivi leo ninavyozungumza.

Mhe. Spika, kuna barua ya pili hii naisoma, barua hii ni ya tarehe 23/5/2012 ya kwana ilikuwa ni ya tarehe 9/2/2012, hii ya tarehe 23/5/2012 yaani ni barua ya kurejea tena. Barua inasema, “Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mahakama ya Wilaya Mwera Zanzibar, sanduku la posta hilo hapo naliacha, aliandikiwa Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kuhusu kesi ya jinai Nam. 430 ya mwaka 2011, aliyeshitakiwa ni Abdalla Makame Mwelezi na wenzake 23, husika na mada iliyotajwa hapo juu, washtakiwa waliotajwa hapo juu wameshtakiwa mbele ya Mahkama ya Wilaya kwa shaka ya kuvua uvuvi haramu. Kifungu Nam. 2(1) (b) na kifungu 27(c) na Kifungu 30(1) cha sheria Nam. 7 ya mwaka 2010 ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mahkama baada ya kusikiliza ushahidi uliotoka upande wa mashtaka kwa washtakiwa hawa hawana kesi.

Samahani Mhe. Spika, narudia tena, “Mahkama baada ya kusikiliza ushahidi uliotoka upande wa mashtaka umeona kwamba washtakiwa hawana kesi ya kujibu. Hivyo, wakaachiwa huru chini ya kifungu cha sheria Nam. 214 ya Mwenendo wa Kesi ya Mahkama ya Jinai, sheria Nam. 7 ya mwaka 2004, wakati wa kusikiliza kesi hii Mahkamani kulitolewa vielelezo mbali mbali vilivyodai kukamatwa navyo washtakiwa, vielelezo vyenyewe ni kama hivi vifuatavyo:

Nyavu 47, vioo 16, samaki na madau sita, leo Mhe. Spika, kwanza watu wakikamatwa wakopwa samaki wao, wanauziwa bila ya kupewa pesa zao vipi tunawadhalilisha wavuvi wetu. Kwa hivyo, nataka anambia Mhe. Waziri lini watu hao watapewa vitu vyao si hivyo fungu hili la pesa hizi za wavuvi haramu mimi naweka mguu. Sasa Mhe. Waziri aje atwambie kama lini watapewa vitu vyao hivi na watu wenyewe Mhe. Spika, naomba kwa idhini yako niwataje.

Orodha ya Washtakiwa wa kesi ya uvuvi wa Chwaka: Mwelezi Makame Mwelezi, Ali Mjaka Kheri Khamis, Yussuf Hassan Mjombo, Iddi Mohamed Omar, Mhe. Spika, wengine nawaacha kwa niaba yako.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba wavuvi wetu wa Zanzibar tusiwatese hawa ndio wanaotusaidia wanaisaidia serikali kutoa ajira. Kwa hivyo naomba kwanza Mhe. Waziri watueleze hasa watubagulie ni nyavu gani hasa zinazotakiwa zivuliwe. Kwa sababu kuna dagaa ni dagaa wa maisha mpaka atakufa hawezi akakua akawa vyengine, leo wavuvi tunawatesa kama waliokuwa hawamo kwenye nchi yao jamani, tukisema sijui tunaonekana vipi sisi. Leo tumewaonea wavuvi kwa sababu tushakuja kupewa pesa na wafadhili tuwatese wavuvi wetu kila inavyokuwa, tusiwatese wavuvi wetu wanasaidia nchi yao jamani, Mheshimiwa tupangeni sheria hii sheria ya uvuvi mimi naomba iletwe hapa Barazani tuifanyieni marekebisho kama tulifanya makosa kuipitisha sheria bila kuangalia, basi iletwe Barazani tuifanyie marekebisho lakini sheria inasema sheria yoyote ile inayoonesha kumdhalilisha mwananchi wa nchi ile haifai. Kwa hivyo, sheria hii iletwe hapa tuje tuifanyie marekebisho tusiwatese wavuvi wetu jamani wanatusaidia ajira hawa, wanaisaidia serikali, wanaingiza mapato katika serikali.

Mhe. Spika, siungi mkono mpaka nitakapopata maelezo mazuri.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuuba yake iliyo nzuri na ambayo imejipanga vizuri na kufafanua jinsi ya vituo vyote vilivyokuwa vimepangwa mle. Kwa hivyo nampongeza Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nikianza na sekta hii ni kuwa hii ni sekta muhimu sana kwa wananchi pamoja na serikali kwa ujumla. Mhe. Spika, kwa hivyo sekta hii inahitaji kuwezesha ili wananchi wake waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi.

Mhe. Spika, nianze na Sekta ya Uvuvi. Zanzibar tunao wavuvi wengi ambao hushindwa kuvua kutokana na kukosa zana za uvuvi. Wavuvi hawa wanaoshindwa kuvua ambao hawana nyavu, madau, mashine na hii yote Mhe. Spika, imetokana na kupigwa vita kwa uvuvi haramu. Kwa hivyo Mhe. Spika, wako baadhi ya watu wengine ambao walikuwa wanavua uvuvi huu haramu na sasa hivi hawana uwezo wa kuweza kuvua bahari kuu kutokana na kutokuwa na zana za kuvulia katika bahari hiyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awaone wavuvi wetu hawa kwa kuwapatia vifaa kwa wale wavuvi ambao wamechomewa nyavu zao moto ili waweze kuvua katika bahari kuu.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Mazao ya Baharini. Naipongeza Idara hii Mhe. Spika, pamoja na majukumu yake ya kuendeleza ufugaji wa mazao baharini bado kunahitajika elimu zaidi kwa wakulima wetu wa mwani. Mhe. Spika, wakulima wetu wa mwani bado wanahitaji elimu kwa

sababu elimu yao ni ndogo hasa ya upandaji wa mwani na ukaushaji. Hili wananchi wetu ni hali ngumu kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri kuwapitia watu wetu hawa ili kuwapa elimu ya upandaji wa mwani ili tupate mwani ulio mwema na ulio bora na wenye ufanisi.

Mhe. Spika, lakini pia nimwambie Mhe. Waziri kuwapatia mbegu inayoleta tija wakulima wetu wa mwani kwa mfano mwani mnene ambao mwani huu unaitwa *cottonnee* kuloikoni mwani mwembamba wa mvinje ambao hauna faida na wala hauleti tija.

Mhe. Spika, pia kuwapatia boti za kubebea mwani kutoka baharini na kupeleka nchi kavu. Baada ya kuvua mwani wao Mhe. Spika, watu hawa huwa wanapata tabu sana kwa sababu kubeba mwani kutoka chini ya bahari na kupeleka juu kuanika ni tatizo kubwa. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aangalie sana wananchi wetu hawa kuwapatia maboti ya kubebea mwani ili waweze kuupangisha juu.

Pia Mhe. Spika, nije katika changamoto ukurasa wa 9. Hapa zipo changamoto zinazosema kwamba kuongeza shindikizo la uvuvi katika maeneo ya hifadhi kutokana na kuongeza kwa idadi ya wavuvi. Mhe. Spika, changamoto hizi ni nyingi sana, lakini pia nimpe changamoto nyengine ambayo hii nayo ni tatizo kubwa. Tulipokuwa na Mhe. Said Ali Mbarouk alipokuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi tulitembelea katika Wilaya ya Mkoani ambayo Mhe. Spika, kuna wavuvi hufunga madebe na kutumbukiza katika bahari, ambapo badebe hayo yafike chini ya bahari kwenye matumbawe na kukoroga ili samaki wapate kuja juu. Mhe. Spika, hili ni tatizo kubwa ambalo pia huharibu matumbawe na pia huharibu vizazi vidogo vimelea vya samaki katika bahari yetu. Hili Mhe. Waziri kama analielewa au kama halielewi basi alifuatilie hili ni tatizo ambalo linaharibu matumbawe.

Nikija katika mifugo Mhe. Spika, tunao wafugaji wetu lakini cha kusikitisha wafugaji hawa wa ng'ombe, kopa ng'ombe ulipe ng'ombe. Wafugaji hawa sasa hivi wamekata tamaa kutokana na ufugaji. Kwanza Mhe. Spika, ufugaji wa ng'ombe unakuwa ni mgumu na ngombe hawa wanaotoka Bara aidha siju kama mandhari ya huku haiwafai au vipi kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri anapowapa watu mifugo awatafutie ng'ombe ambao wanatoka hapa hapa kwetu Zanzibar kuliko ng'ombe wanaotoka Bara ambao ngombe hao wakifika huku hawahimili baridi ya huku na hatimaye ng'ombe wale hufa. Kwa hiyo Mhe. Spika, wananchi hawa wamekata tamaa kubwa sana kwa sababu ng'ombe wale wanapozaliwa mtu keshategemea ng'ombe yule kwamba apate na yeye achunge hatimaye baada ya miezi miwili mitatu hufa, hiyo sijui inatokana na sababu gani.

Mhe. Spika, pia niende katika wafugaji wa samaki. Hili limekuwa ni kubwa sana kwa Kisiwa cha Pemba. Mhe. Spika, vile vile tulitembea na Mhe. Said Ali Mbarouk tukapitia mabwawa ya samaki ambayo ni mengi, tulikwenda Shamiani pale tukaona ufugaji wa samaki ulivyo, kwa pale Mhe. Waziri aliweka ahadi ambapo alisema atalichukulia hatua lile ili pawekwe kituo kidogo cha ufugaji. Sasa namuomba Mhe. Waziri aonane na aliyekuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi ili wapange vipi hatua ile ilivyofikia.

Vile vile katika ufugaji huo wa samaki nafsi yangu Mhe. Spika, nimeanzisha bwawa baada ya kumuona Mhe. Waziri aliyepita wa Wizara hii alipotutembeza katika Wilaya ya Mkoani kuona mabwawa yale jinsi watu wanavyofuga. Na mimi nikaanzisha bwawa lile Mhe. Spika, lakini kwa

bahati hili bwawa nimewekeza samaki kiasi cha 5,000 lakini hivi karibu napigiwa simu samaki 1,200 ambao wameibiwa sasa hivi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri afanye ziara zake kwenda kisiwani Pemba na ikiwezekana afike katika Shehia ya Pangani kwenda kuliona bwawa hili na aweke mikakati iliyo madhubuti ili wananchi waliokuwa hawapendi maendeleo ya wenzao awape mikakati hiyo na kuweza kufahamu nini maana ya ufugaji.

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, nami nichukue fursa hii ndogo kuweza kuchangia hotuba hii inayoendelea. Kwanza nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii lakini vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri sana ambayo ameitoa hapa na anaonesha dhamira halisi ya kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Lakini vile vile niwapongeze watendaji wake wakuu na wale wote ambao wamemsaidia kwa kuweza kusimama kwa miguu yake miwili akatupa lile somo bora ambalo amelitoa muda mfupi tu uliopita.

Nianze basi moja kwa moja katika ukurasa wa 9 Idara ya Uzalishaji wa Mifugo. Mhe. Spika, niipongeze serikali kwa madhumuni yake makubwa ya kuchukua hatua hii muhimu sana, kwanza kwa kushajihisha kuleta ajira kwa vijana wetu, vile vile imechukua muundo mkubwa sana wa kuweza kuchukua hatua kubwa ya kuboresha mifugo yote hapa Zanzibar, lakini changamoto kubwa tuliyonayo katika hali halisi ya mifugo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kuna kituo cha Upandishaji wa Ng'ombe. Kituo kile tunaishukuru sana serikali na tunaipongeza kwa hatua kubwa tangu Waziri aliyepita mpaka waziri huyu aliyepo sasa kwa kukiimarisha kituo kile na kuwa kituo bora ambacho sasa tunapata mbegu nyingi za ng'ombe wa kisasa. Lakini Mhe. Spika, kituo kile tulikuwa zamani tunahangaika na *liquid nitrogen*, ambapo *liquid nitrogen* ilikuwa tunanunua Arusha, lakini kipindi kirefu tangu serikali kuona nia halisi ya wananchi wa Zanzibar kuweka kwenye mifugo imetununulia kwa pesa nyingi mtambo ule na tayari umeshafungwa, na sasa tunaanza kuona matunda yake halisi yamepatikana. Tunaipongeza sana serikali lakini vile vile tunataka kuishauri wizara.

Pamoja na *liquid nitrogen* nyingi ambayo inatoka pale, sasa sisi tulikuwa tunanunua *liquid nitrogen* ile lakini sisi tunazalisha kupita uwezo wetu. Kwa hivyo tunaishauri wizara itafute masoko iweze kuuza basi katika zile pesa zitazopatikana tuanze kuhudumia vitu vingine.

Mhe. Spika, mimi niende tena kwenye ukurasa wa 27 Idara ya Huduma za Matibabu ya Wanyama. Mhe. Spika, tunakabiliwa na changamoto nyingi sana, madaktari ingawa hatunao wengi lakini tunao wataalamu wa kutosha pale ambao tunaweza kuwatumia kutibu mifugo yetu. Kwa sababu mifugo inapoumwa hatuwezi kupata maendeleo halisi, lakini tuwe na madaktari wengi, tuwe na vifaa vya kazi ambavyo vitaweza kuwasaidia madaktari wale. Hawa madaktari kidogo tulio nao wataweza kutusaidia lakini wanakosa nyenzo za kuweza kufanyia kazi hususan pikipiki na petroli.

Mhe. Spika, kuna mifugo mingi inapata maradhi na yatimaye kufa katika vijiji mbali mbali. Kamati yangu ilipotembelea kule Pemba tuliona vijiji vingi wanyama wanakufa pale lakini

matokeo yake madaktari wanashindwa kwenda kwa wakati, wanashindwa kujua ni maradhi gani waliyokufia wanyama wale.

Mhe. Spika, hata *post-mortem* inashindwa kufanyika na *post-mortem* tunapopata *sudden death* vile vifo vya ghafla vya wanyama wetu tunataka tuchunguze ni kitu gani ambacho wanyama wale kimewasababishia kufa, ni maradhi gani wanyama wale wameyapata hata ikatokea vifo vya ghafla kama vile. Sasa mimi naiomba serikali kupitia wizara yetu ijitahidi kuwapatia nyenzo hao wataalamu wetu; ili waende *field* na kuweza kujua ni kitu gani wale wanyama wanaathirika.

Lakini vile vile nichukue tena fursa hii kuipongeza serikali yetu kwa kuweza kujenga maabara zile mbili ya Zanzibar kufanyia ukarabati na ile ya Wete Pemba. Hizi maabara ni kiungo muhimu sana kwa kujua maradhi ya wanyama. Mhe. Spika, hivi karibuni tulikuwa tukipeleka *sample* za maradhi yale au zile *specimen* za wanyama kupeleka Arusha ili kupata majibu, hatujui tulikuwa tukichukua siku ngapi kama mwezi, miezi miwili. Lakini mimi naipongeza Wizara kwa kuweza kujua umuhimu wa maabara ile na kuweza kuleta pale vitu mbali mbali vya kuweza kupimia maradhi yale. Sasa hivi tunaweza kujua kwamba tukipata *brucellosis* tunajua tukapime wapi, tukipata *anthrax* lakini Mwenyezi Mungu atuekishie mbali, lakini wanafanya kazi vizuri sana kuweza kujua wanyama wetu kitu kinachowasumbua.

Mhe. Spika, kuna shamba lile ambalo limejengwa au linawekewa karantini la Chamanangwe. Shamba lile wizara imeweka hatua kubwa sana ya kuweza kuliimarisha, lakini mpaka sasa inashindwa na bajeti kubwa ambayo imepangiwa pale. Bajeti haitoshelezi, tungeiomba serikali iweze kuwapa fedha za kutosha kuweza kuweka shamba lile la karantini na umuhimu wake ni mkubwa sana, kama hatutaweka karantini Mhe. Spika, wanyama wengi wanatoka nje lakini bahati mbaya sana hakuna karantini yoyote inayowekwa, tutaweza kuleta maradhi katika nchi yetu na hatimaye basi tutakuwa hatuna hata wale wanyama ambao tutaweza kuwafanyia kazi.

Mhe. Spika, sasa nije katika chinjio letu la Kisakasaka. Naipongeza serikali kwa sababu matengenezo yote yaliyotengenezwa pale ni makubwa, mazuri ambapo sasa hivi ukienda kwenye chinjio lile unaweza kuona upeo wa macho yako, lakini ukitofautisha na zamani kulikuwa na msitu mkubwa sana. Tunaipongeza sana serikali kwa hatua hii ambayo imefanya.

Mimi nimeanza kuwashangaa baadhi ya Wajumbe wako Mhe. Spika, kusema kwa nini wizara imetenga fedha kwa kichaa cha mbwa. Namuomba Mhe. Waziri siku moja atumie wataalamu wake kuweza kuwajuilisha au kuwafanyia semina Wajumbe wa Baraza hili kujua kichaa cha mbwa athari zake ni nini. Mbwa akipata kichaa haathiriki peke yake, mnyama mwengine yoyote aliyepo karibu yake hata binadamu, na kutibika kwake inakuwa shughuli pevu sana.

Mhe. Spika, nije tena kwenye Idara ya Maendeleo ya Uvuvi. Nimpongeze sana ndugu yangu Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi Baharini kwa hatua zake kubwa sana anazozichukua. Kwa sababu ameanza kutuelewisha nini athari za uvuvi haramu, nini faida zake na wapi tunapogonga. Lakini *mnyonge mnyongeni haki yake mpeni*, kwa kweli kijana anajitahidi sana nimemshuhudia kule Pemba kulikuwa na mgogoro vile vile aliwaita akaonesha mpaka *film* za *video* ambazo zinaweza zikaathiri maendeleo yetu, na wale wavuvi wote walipoondoka pale walipatana wakawa kitu kimoja. Tumpe haki yake na tumsifu sana kwa hatua kama hizo.

Mhe. Spika, sisi baada ya kwenda mbele tumekuwa tunarudi nyuma hapa Zanzibar. Zamani tulikuwa na skuli ya sekondari ya bahari na uvuvi ambapo wanafunzi wanaotoka pale ndio waliokuwa wanaingia vyuoni, lakini skuli ile sasa ule mtaala umeondolewa. Sasa nataka nijue au Mhe. Waziri atakapokuja aniambie ni lini basi ataleta sera ya kuweka angalau kurudisha mtaala ule na kuweka Chuo ambacho kitaweza kusaidia bahari yote na vitu vyengine vya sayansi za baharini.

Kwa sababu sisi tumezungukwa na bahari; leo itakuwa kitu cha aibu sana kuwa hata wataalamu tunaanza kupeleka nje hatuwezi kusomesha hapa. Mimi naamini tunao wataalamu wa kuweza kutusomesha na tunaweza kupata wataalamu bora kuliko kupeleka nje.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa kuzungumza machache kuhusu mada iliyopo mbele yetu. Kwanza na mimi ningempongeza *College mate* wangu kwa juhudi yake anayoifanya ya kuona vitoweo vimekuwa rahisi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, na mimi kidogo niingie katika vifungu nina imani kwamba tukizipunguza vijisenti hivi pengine tutakuwa na uwezo wa haraka haraka kutafuta meli ambayo itatusaidia katika kupunguza majanga. Mhe. Spika, labda ningepata maelezo kidogo kutoka kwa Mhe. Waziri katika vifungu. Katika fungu 220505 nimeona kwamba mwaka jana walikuwa na shilingi milioni moja katika ununuzi wa *sundry* (vifaa vidogo vidogo), lakini fungu hili limepanda mpaka kufikia shilingi milioni kumi na moja na laki saba. Sasa ukija kiwastani unaweza kukuta kwamba kila mwezi hapo ni shilingi milioni moja sijui wao watakuwa wananunua nini kila mwezi, *sundry* za kiasi gani na ni vipi hata ifike shilingi milioni moja kwa kila mwezi.

Lakini jengine ni kuwa nina imani kwamba wakati wowote watahamia katika nyumba yao mpya, jengo jipya lile. Lakini ukiangalia humu kuna mafungu tofauti kila idara imeweka fungu la umeme shilingi milioni sita, Idara ya Utumishi shilingi milioni saba, Idara ya Mifugo, Idara ya Mazao ya Baharini shilingi milioni mbili kitu kama hicho, hebu anipe maelezo sijui mwaka huu atahamia hizi pesa za umeme zitakuwa kwa sehemu tafauti tafauti; au vile watapokwenda kuhamia kwenye ofisi yao kutakuwa na fungu moja tu la matumizi ya umeme, naona matumizi ya umeme yamekuwa mengi zaidi.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakwenda katika hii chati waliyotupa. Kidogo wamenipa mshangao kwa sababu hii ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi, nikiangalia nakuta kwamba wafanyakazi walioko katika Sekta ya uvuvi ni wachache sana lakini walioko katika Sekta ya mifugo ni wengi sana. Sasa mimi mtazamo wangu ni kwamba, labda sekta ya uvuvi ina wigo mpana sana na tunaweza tukaendelea zaidi kama tutaelekeza nguvu zetu katika sekta ya uvuvi kuliko sekta ya mifugo. Lakini cha kushangaza ni kwamba sekta ya mifugo ndio iliyo na watendaji wengi zaidi kuliko hii sekta ya uvuvi, sasa sijui hatuoni kwamba kufanya hivyo kidogo kutarudisha nyuma hii sekta ya uvuvi ambayo mapana yake yanaturuhusu sisi kwenda mbele zaidi kuliko hii Sekta ya Mifugo.

Lakini katika hilo nimeangalia kwenye Sekta ya Utaalamu. Katika sekta hii Mhe. Spika, unakuta kwamba kuna wataalamu ambao wana *Msc*, wataalamu hawa wako 13 lakini wataalamu hawa

wote wako kisiwani Unguja sijui hivi sasa hakuna haja ya mtaalamu yoyote aliye na fani ya *Msc* katika kile kisiwa cha Pemba angalau nao wakajua utalamu wake unatasaidia katika kukuza , aidha hiyo mifugo au kuendeleza sekta yetu ya baharini au vipi, labda Mhe. Waziri angenipa maelekezo pamoja na ufafanuzi kwa nini hakuna mtaalamu hata mmoja wa *Msc* katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, niondoke hapo sasa kidogo niende katika tabu kubwa. Mhe. Spika, hivi sasa kuna malalamiko mengi kutoka kwa wavuvi, na kila nikiangalia naweza kukuta kwamba malalamiko haya yanawezekana yakawa na sababu zake. Kwamba sheria iliyotungwa miaka miwili iliyopita haikuzingatia mambo mengi sana, kama wenzangu waliokwisha tangulia kusema kwamba sheria hii ina mapungufu, na mapungufu haya yanawanyanya watumiaji wake.

Kwa mfano matumizi ya viatu kama walivyosema wengine, kwamba matumizi haya wao hawaoni sababu kwa nini watu hawa wakapigiwa marufuku matumizi kama haya. Lakini la ziada ni kwamba kuna nyenzo kubwa ambazo wanazitumia wavuvi wetu hawa nyenzo hizi pia wamepigiwa marufuku wasitumie. Lakini juu ya hayo kuwa wamepigiwa marufuku kanuni zetu na katiba yetu inatuelekeza kwamba, mtu yeyote ambaye atakuwa amechukuliwa amana yake basi apewe fidia, sasa la kushangaza ni kwamba wenzetu hawa hawakupewa fidia yoyote na wao wanataka wajiajiri katika sekta yao hii. Sasa je, sheria hizi zilizotungwa hazikuzingatia mambo hayo, kwamba sisi kutakuwa na watu ambao wataathirika katika kuitunga sheria hii.

Kwa hivyo, kama alivyosema Mhe. Subeit Khamis Faki kwamba kwa nini hatuoni kuwa iko haja ya sheria hii kuja tena hapa tukaifanyia marekebisho. Kwa sababu wenzetu ambao imewahusu moja kwa moja inawaumiza. Mimi nahisi Waziri hii aiangalie kwa kina kwamba sheria ipo lakini inahitaji ifanyiwe marekebisho kwa sababu wanaohusika wanaathirika sana.

Lakini juu ya hilo ni kwamba pia kuna utoaji wa leseni. Mimi nafikiri katika kisiwa chetu wengi sana ni wavuvi, hata mimi hapa nikimaliza katika shughuli zangu za hapa basi huwa nina uhuru wa kwenda katika bahari nikajitafutia kitoweleo, lakini utakuta lazima uwe na leseni wewe kwa nini uwe na leseni? Hii sijui Mhe. Waziri imewekwa kama ni njia moja ya kuongeza pato la taifa au imeletwa kwa sababu gani. Kwa sababu ukimuwekea mtu leseni leo huyu ni fundi muwashiki lakini kesho anaona kazi ya uashi mimi sina sasa nataka kwenda baharini, mjomba wangu analo dau kwa nini asiende kwa vile hana leseni. Mimi nafikiri sheria hii ingebadilishwa, kwa vile chombo tayari kimeshawekewa leseni basi sheria hii nayo ya kumfanya mtu lazima awe na leseni itakuwa ni kama njia ya kumfanyia *exploitation* raia wetu, lakini msingi wake wa kuwa nayo haupo.

Huko nyuma tulisema kwamba atakae aje katika kisiwa hiki, sasa na hii vile vile ni kama vile unaingia msikitini tu ukiwa na udhu unaingia na ukiwa huna udhu pia unaingia, sasa na mtu kwenda baharini ni jambo la kawaida tu, mtoto anaweza kusema baba leo sikwenda skuli twende basi anamchukua anakwenda kumsaidia katika shughuli zake, lakini unamwambia lazima awe na leseni. Mhe. Spika, hii mimi nafikiri Mhe. Waziri sheria hii nayo wangeiangalia kwa kina kwa nini tukaweka sheria hii au na mafundi waashi, mafundi seremala na wao watakuwa wana leseni kwa zile kazi zao. Hii naona ingeangaliwa tena kwa kina tukaangalia namna gani ya kuwasaidia wananchi wetu, kwa sababu ni sekta ambayo iko *free* tusiiwekee masharti yoyote, watu

tuwaruhusu kila mmoja anayetaka basi aende kwa sababu ndio sekta pekee ambayo inatoa ajira kwa kila raia wetu.

Jengine Mhe. Spika, ni kwamba hivi kuna ongezeko na upungufu wa upatikanaji wa mazao ya baharini hasa samaki. Katika mwezi huu wa Ramadhani wananchi walaji tunalalamika sana kwamba vitoweleo vimekuwa katika hali ya juu. Ukiangalia pepo zetu ziko yaani uvuvi ni kitu cha *seasonal*, unaweza kwenda wakati ukakuta upepo unaweza kwenda baharini ukapata samaki kwa wingi, na kuna wakati ukakuta labda huwezi kwenda samaki wanapatikana kwa kidogo. Kwa hivyo, hili ndio linaathiri bei, pengine bei inawezekana ikawa kubwa kwa sababu fulani au ndogo kwa sababu fulani.

Sasa mimi wasiwasi wangu ni kwamba haya pia yanamfanya mvuvi aathirike pengine mlaji nae pia aathirike. Sasa labda Waziri ana kumbukumbu kwamba huko miaka ya nyuma tulikuwa tunanunua samaki kwa kupima, labda zoezi hili wamelifanyia utafiti wowote kuwa labda tukiweka ununuaji wa samaki kwa kilo atafaidika mvuvi, atafaidika na mwananchi ili kuondoa yale manung'uniko ya kwamba kipindi hiki hivi, kipindi hiki vile suala kama hilo sijui wamelifanyia utafiti wakaona labda suala hili linaweza likasaidia.

Kwa sababu katika sekta moja mfano ya utalii kama pweza hivi sasa wanakwenda katika mfumo kama huo na ukiangalia hakuna malalamiko makubwa, utakuta mnunuaji yuko tayari na muuzaji na yeye anafaidika kwa upande wake. Sasa je, suala hili wizara imekaa imefanya utafiti na kuona labda tukifanya mfumo kama huu basi wananchi kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kitengo cha kumlinda mlaji labda litawasaidia wananchi kupungukiwa na suala hili.

Lakini je, katika hilo pia hawa wavuvi wetu tunawapa taaluma gani labda katika utumiaji wa mambo ya *meteorology*. Kuna taaluma yoyote kwa mfano kama upepo leo utakuwa katika kiwango fulani kwa hivyo huruhusiki kwenda baharini, au leo mnaweza mkenda au hakuna masuala kama hayo ambayo yanatumika tunawaachia wanakwenda zao tu matokeo yake wakifika katika maeneo ambayo hayastahiki basi wanaathirika.

Lakini jengine Mhe. Spika, ni hili la Bahari Kuu. Nafikiria kwamba bado wizara au serikali kwa ujumla haijalitilia mkazo hasa suala hili, na ukiangalia hii ni sekta ambayo labda ajira nyingi zitaweza kupatikana. Kwa kumbukumbu zangu mwaka jana Mhe. Waziri aliyepita alifuatana na ujumbe kutoka Serikali ya Uturuki; na ujumbe huu ulitembelea maeneo ya Pemba kama vile maeneo ya Mkoani na maeneo ya Ole kwenda kukagua njia gani za kuweza kuzalisha zile *fiber* za uvuvi na pia kukagua sehemu ambayo labda wangeweza kuwekeza viwanda kwa ajili ya kusindika samaki na mengineyo. Mwaka umepita sasa sijui niulize wale wananchi wetu tuliowatia tamaa waendeleo kukaa nayo tamaa ile au waondoshe. Wale wawekezaji wameondoka hawapo tena, kwa hivyo wao waendeleo kutumia maeneo hayo kwa kulima au kujenga nyumba zao. Mhe. Spika, naomba nimalizie hapo.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kidogo ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi; hotuba ambayo imepangika, yenye mwelekeo mzuri. Nampongeza sana pamoja na watendaji wake na namuombea kila la kheri

kulivusha jahazi hili ambalo limejaa shehena ya ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kuiletea maendeleo nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa kuanza tu naomba kuanzia katika ukurasa wa 7 katika Sekta ya Uvuvi kwenye mafanikio ya sekta hii ya uvuvi naomba kunukuu hapa kidogo Mhe. Spika.

Ukurasa 7 kifungu (d) kinasema kwamba:

“Kumalizika kwa mchakato wa kuanzisha Kitengo cha Hifadhi (MCU) kitakachosimamia bahari ya Mji Mkongwe na Kisiwa cha Tumbatu kwa kuanzisha sheria ndogo”.

Mhe. Spika, mchakato huu wa hifadhi ambao umeelezewa hapa kwamba unaendeshwa vizuri, lakini kwa taarifa tulizonazo bado hali ni tete hususan katika kisiwa hiki cha Tumbatu. Kutokana na kutokamilika kwa hifadhi hiyo inaleta athari kubwa kwa bahari ya kisiwa cha Tumbatu pamoja na wananchi wa Tumbatu kwa ujumla. Kwa hivyo mimi ningemuomba Mhe. Waziri wakati anapokuja basi atueleze ni lini hasa mchakato ule unaweza kumaliza, kwa sababu bado mchakato ule haujamalizika.

Lakini nikitoka hapo Mhe. Spika, nije katika suala zima la ujenzi wa solo la Kisakasaka pale. Mhe. Spika, soko lile ambalo limefanyiwa ukarabati mkubwa katika maeneo yale na bado katika taarifa yake ni kwamba kuna ujenzi mpya pale ambao utajengwa. Sasa nilikuwa nataka kujua Mhe. Spika, kwamba huu ukarabati ambao umefanywa katika soko lile ametumia kiasi gani, kwa sababu chinjio lile liliopo pale marekebisho yale yameshakamilika na taarifa zipo kwamba kunataka kujengwa kituo kipya pale. Sasa hayo marekebisho ambayo yamefanywa pale nadhani yametosheleza vizuri niwapongeze, lakini nilitaka kujua tu kwamba wametumia kiasi gani.

Lakini wakati kinafanyiwa ukarabati kisoko au kichinjio kile wizara iliweza kuweka umeme pale wakati wao wanaendeleza ujenzi ule. Lakini tatizo liliopo ni kwamba umeme ule ambao umewekwa ulikuwa pia uwafikie wananchi wengine walioko pale, na wananchi mbali mbali walioko pale ambao ni uthibitisho sahihi ninayo *list* ya wananchi hao waliokuweco pale ambao walichangia ili kuweza kupata huduma zile za umeme ambao uliwekwa na wizara kwa ajili ya chinjio lile la Kisakasaka. Kwa hivyo Mhe. Waziri atapokuja atwambie ni kampuni gani ambayo ilipewa *tender* ya kuweka umeme ule na uligharimu shilingi ngapi.

Kwa sababu wananchi wa pale walichangia zaidi ya shilingi milioni tano, sasa tunataka kujua ni kiasi gani gharama zilizotumika na kampuni waliyopewa kwa ajili ya kuweka umeme ule.

Mhe. Spika, katika chinjio lile kuna chuma kikubwa ambacho hutumika kwa kuweka mapaja ya nyama baada ya ng’ombe kuchinjwa, lakini chuma kile kimepotea au hakionekani. Sasa Mhe. Waziri nataka kumuuliza chuma kile kimekwenda wapi, na kuondoka kwa chuma kile naona kwamba kutakuwa na usumbufu mkubwa sana kwa nyama ambazo zinachinjwa pale ambazo baada ya kuchinjwa huwekwa pale. Kwa hivyo akija atueleze chuma kile kimepotea na kimekwenda wapi.

Lakini Mhe. Spika, nikija katika suala zima la Mradi wa Mafua ya Ndege, katika taarifa yake hapa Mhe. Waziri ameeleza kwamba katika mwaka wa fedha 2011/2012 kulikuwa na shilingi milioni hamsini na tano na mwaka wa fedha 2012/2013 kuna milioni thamanini. Lakini na

maradhi haya ya ndege hatujapata taarifa kwamba yapo hapa Unguja au Pemba, kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja basi atueleze kwamba maradhi haya ya mafua ya ndege, na kwa sababu bajeti yake ipo hapa, mwaka jana ni milioni hamsini na tano kama nilivyosema na mwaka huu ni milioni thamanini.

Kwa hivyo akija atueleze kwamba fedha hizi ambazo zimetengwa shughuli zake hasa ni nini, kwa sababu maradhi Zanzibar nina imani kwamba maradhi haya hayapo lakini fedha bado zinaendelea kuwekwa katika vifungu hivi. Kwa hivyo Mhe. Waziri akija atueleze haya. Mhe. Spika, suala hili zima ni suala ambalo lazima wananchi kwanza waeleweshwe, wafahamishwe vizuri kuhusu mchakato mzima wa maradhi haya ya mafua ya ndege.

Vile vile Mhe. Spika, nikija suala hili la wanyama. Suala hili kwa kweli limekuwa likipigiwa kelele katika Baraza lako tukufu hili hususan katika wanyama hawa punda wamekuwa wakipata mateso. Katika ripoti ya kitabu hiki imeeleza kwamba kumekuwa na matibabu wanyama walikuwa wanapata akiwemo punda, mbuzi, ng'ombe, kuku. Lakini wale wanyama ambao wanapata vipigo kutoka kwa wananchi au kutoka wafugaji. Sasa nilikuwa nikitaka kumuuliza Mhe. Waziri baada ya kupata vipigo vile kuna utaratibu wowote pengine kuwanusuru wanyama wale kuweza kupata tiba na kuwaweka katika hali nzuri ya maisha ya wanyama wale. Kwa hivyo Mhe. Waziri akija na taratibu gani anaziweka ili kuwadhibiti wale ambao wanaowapiga na kuwatesa wanyama wale.

Lakini Mhe. Spika, mimi niunge mkono sheria hii ya kudhibiti au kulinda viumbe hivi vya baharini. Kwa sababu bila ya kuweka sheria hii watoto wetu, wajukuu zetu watakuja kukosa samaki. Samaki ni kitoweo kizuri. Kwa hivyo ni wajibu wetu na ni wajibu wa Mhe. Waziri kulinda hivi viumbe ambavyo vipo baharini kwa faida ya vizazi vyetu vinavyokuja. Bila ya kuweka sheria hii madhubuti na bila ya kuwalinda Mhe. Spika, kweli itakuwa ni matatizo huko mbele tunakokwenda. Kwa hivyo Mhe. Waziri suala hili ulichukulie *serious* kabisa na ulifanyie kazi suala hili kuhakikisha kwamba viumbe hivi vya baharini vinalindwa.

Mhe. Spika, kwa kumalizia mimi niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, kwa sababu ninashukuru nimepata nafasi alau ya kupata kukohoa machache, kwa sababu unapokohoa kidogo unapata nguvu, bila ya kukohoa kidogo nguvu zinakuwa hazipo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii kuchangia bajeti hii. Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema. Pili ninapenda kumpongeza Mhe. Waziri kwa bajeti yake aliyoandaa vizuri.

Mhe. Spika, kwa kuwa wananchi wengi wameupokea uvuvi ambalo ndilo pato lao, lakini kwa vile changamoto nyingi zimewabana wabana wavuvi. Kwa kuwa wananchi wengi wameanguka kiuchumi hususan wavuvi. Jee Mhe. Waziri atawanyanyua vipi wavuvi hawa, wapo wavuvi wa makundi na wapo wavuvi mmoja mmoja.

Mhe. Spika, sheria hii inawabana wavuvi kwa vile, nitaelezea historia kidogo. Mhe. Spika, kipo kikundi cha watu wa Paje ambacho kikundi hicho kilizuiwa uvuvi wao ambao walikuwa wanavua kwa kuambiwa nyavu haramu. Sasa wakaja kwangu kwa kusikitika na mimi nikawapeleka kwa Mhe. Waziri siku ya kwanza akawasikiliza na siku ya pili nikawapeleka tena, siku ya tatu tukapelekwa kwa kurugenzi, Mkurugenzi akatupa elimu, akatusomesha na tukaelewa.

Pale pale wakaambiwa kwamba nyavu zile wazirejeshe na watapewa nyavu nyengine. Hadi hii leo mpaka hivi sasa bado hawajapewa nyavu nyengine na zile wamezirejesha, wameanguka kiuchumi hawana kazi yoyote ya kufanya. Mhe. Waziri jee utawaangalia vipi watu wa Paje.

Mhe. Spika, ninakuja kuhusu ufugaji. Katika Shehia yangu ya Jambiani upo ufugaji wa mbuzi. Mbuzi wale kwenye bajeti iliyopita nilisema wapo mbuzi ambao hawaleti tija, ni mbuzi ambao ni wadogo wadogo, hawazai vizuri. Ninaiomba wizara kwamba iwaangalie watu wale, wawaletee mbuzi ambao ni bora wanazaa watoto wengi na wanatoa maziwa mengi.

Mhe. Spika, kuhusu mwani. Mwani ni zao kubwa ambalo wananchi wamelipokea kwa wingi lakini zao lile ni gumu linahatarisha afya zao. Ningeiomba Wizara kutokana na kazi wanayoifanya ni ngumu lakini pato lao ni dogo, iwaongeze pato hili wale ambao wanafanya kazi hii, yaani wanunuzi waongeze wateja hawa angalau kwa kilo moja shilingi elfu moja na mia tano wananchi hawa wanufaike na zao hili.

Mhe. Spika, ninakuja kuhusu ufugaji wa samaki. Katika eneo langu la Shungi, lipo eneo ambalo lina koko. Safari moja Mhe. Waziri alinialika katika wilaya yangu kwenda kuangalia ufugaji wa samaki, kasa na kaa. Kwa bahati nilipofika katika eneo langu nikaangalia wapi panafaa kwa ufugaji wa vitu hivi.

Kwa bahati nzuri lipo eneo linaitwa Shungi. Likatafuta watu likawauliza nani mwenye eneo lile ambalo lina koko kwa vile waende wakafaidike na uzalishaji ule. Kwa bahati nikawapata wenye eneo nikawaeleza na kuwaambia kwamba itabidi sasa mwende mukachimbe ili kuna ufugaji wa samaki, munaposhindwa nitawasaidia na nitamuita Mkurugenzi.

Kwa bahati nzuri nikawapata. Wakati wa kufanya kazi akatokea mtu mmoja tu akenda kuchimba na akafanikiwa. Kwa bahati nzuri mimi nikamuita Mkurugenzi, akafika Mkurugenzi na akaangalia akasema kuwa panafaa. Akaleta samaki kwa bahati wanakua lakini sasa wameingia wengine.

Sasa ninamueleza Mhe. Waziri ningeiomba wizara yake katika eneo lile, wakati eneo lile ni kubwa na linafaa kwa uvuvi ule wa samaki, ningeiomba wizara yake iwashajihishe, iwanyanyue kiuchumi ili iwawezeshe wale wananchi wapate kunufaika na mahitaji yale ya ufugaji wa samaki.

Ahsante sana Mhe. Spika, sina zaidi isipokuwa ninaunga mkono hoja.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza ninashukuru kupata fursa hii ya kuchangia ijapokuwa kwa muhtasari Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Mhe. Abdillahi Jihadi.

Ninachukua nafasi pia ya kumpongeza kwa uwasilishaji wake mzuri ambao takriban haukuwa wa kutabahanika. Halikadhalika ninachukua nafasi ya kuwapongeza watendaji wake wote kwa kushirikiana naye katika kukiandaa kitabu hiki ambacho ni roho ya Wazanzibari kiasi fulani, kwa sababu kitabu hiki ni wizara ambayo *alaa kullihaali* muna mahitaji mengi sana katika mifugo na uvuvi katika maisha ya mwanadamau.

Lakini kabla sijaenda katika kitabu nirudi kidogo kuhusiana na suala zima la ukatili wa wanyama kama walivyotangulia wengine kuzungumza. Mhe. Spika, suala la ukatili wa wanyama kwa kweli hapa Zanzibar ni suala ambalo linatisha sana. Pana Ustadhi mmoja pale Darajabovu siku moja tumekutana katika siku za karibuni hivi, akaniambia Mheshimiwa nyinyi munazungumza mambo mengi tu katika Baraza la Wawakilishi lakini mbona suala hili la ukatili wa wanyama hamulizungumzi.

Munajua kwamba wanyama ni sehemu ya maisha na wao ni viumbe kama sisi. Kwa nini munakuwa hamlizungumzi suala hili wanyama wanateseka. Kwa hivyo ninashukuru kupata nafasi hii kwamba *message* imefika katika jamii yetu ya Wazanzibari juu ya suala zima la kuwakatili wanyama.

Mhe. Spika, kama sheria za wanyama zipo. Jee, nimuulize Mhe. Waziri ni wizara gani au ni taasisi gani iliyopewa jukumu la kulinda haki za wanyama. Kama taasisi hiyo haijapewa jukumu la kulinda haki za wanyama, lini wizara itatoa tamko rasmi na taasisi yoyote ambayo itaiona isimamie masuala haya ili wanyama na wao wawe na mapenzi kwa wafugaji wao.

Mhe. Spika, kwa kweli niseme kwamba baadhi ya wapakiaji wa gari za ng'ombe na punda wanakosa hata kujihurumia wao wenyewe bila ya kuwawahurumia wale wanyama, kwa nini. Kwa sababu wale ni kitendea kazi chao. Kinapofika pahali pa kuvunjika au kufa mnyama yule basi ameumia yeye kwa upande mwingine kwa sababu ile ndio njia yake ya kumpatia maisha. Kwa hivyo mimi niseme kwamba wafugaji hawa wawaonee huruma kwa kiasi kikubwa wanyama wetu ili iwe na wao ni kichocheo chao cha maisha ya kila siku.

Mhe. Spika, nikiachilia hilo niende kidogo kuhusu suala zima la ufugaji wa samaki. Mhe. Spika, kuna maeneo mengi Zanzibar; Unguja na Pemba watu wameshajihika katika suala zima la ufugaji wa samaki. Lakini wanafuga samaki kwa ajili ya kitoweo tu, kwa sababu hakuna tija yoyote ya maisha ambayo wanaipata kutokana na miradi hii, kwa sababu ya umasikini ambao umewakabili kwenye vikundi hivi.

Kwa hivyo labda mimi nimuombe Mhe. Waziri pamoja na juhudi zake kubwa lakini suala hili la wafugaji wa samaki aliangalie vizuri awawezeshe, ili waweze kupata samaki watakaowasaidia katika maisha yao na kujikomboa kwenye umaskini.

Mhe. Spika, katika Jimbo langu la Chambani ninayo mabwawa hayapungui matano au zaidi wamejikita watu kushirikiana pamoja katika ufugaji huu wa samaki. Lakini mabwawa yote hayo ukenda ukiangalia kila unapofika katika msimu wenyewe wanaita funua wimbi, basi yale matuta yao yanakatika, vifaranga vyao vya samaki vinatoweka. Jee Mhe. Waziri ni mbinu gani au ni

utaratibu gani utawawezesha wananchi wanaofuga samaki ili samaki wao wawe ni wenye kudumu katika mabwawa yao na kufikia wakati wa kuuza na kujiondoa katika umaskini.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende katika suala zima la ufugaji wa ng'ombe. Mhe. Spika, suala hili kuna ng'ombe labda niseme kwamba wapo wa kienyeji ambao kwa asilimia kubwa katika visiwa vyetu ndio ng'ombe ambao wanafugwa hasa katika maeneo ya vijijini. Jee Mhe. Waziri mbali ya ng'ombe hawa wa maziwa, unawaendeleza vipi wafugaji wa vijijini katika ng'ombe wao wa asili ambao mara kwa mara huwa wanapata maradhi. Kwa hivyo Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri kwamba katika taratibu zake na ziara zake za kuwatembelea wafugaji basi awatayarisha watendaji wake wapite vijijini kuwaelimisha wafugaji wa ng'ombe wa vijijini, kwani kwa asilimia kubwa sana Zanzibar ndio mifugo yetu.

Mhe. Spika, nikiacha hapo niseme kwamba kuna masuala ya kuwatibu wanyama. Niseme kuwa majimbo mengi ya vijijini ukiachilia mbali mijini na yale maeneo ambayo yana utaratibu wa kufuga ng'ombe labda kijumla jumla. Ni utaratibu gani ambao wizara yako Mhe. Waziri imepanga kuwapitia wafugaji wa vijijini ili kwa kila baada ya kipindi kuwatibu ng'ombe hawa ambao kwa kiasi fulani ni kitoweo.

Mhe. Spika, nikiachilia mbali hayo niende katika ufugaji wa kuku. Mhe. Spika, kuku ni miongoni mwa mifugo yetu. Mwaka jana kulikuwa na vikundi vimepewa utaratibu wa ufugaji wa kuku, wamejenga mabanda kwa gharama kubwa lakini mpaka leo hawajapewa kuku hawa. Kwa hivyo niseme Mhe. Spika, sijui lini watu hawa ambao wameshajenga mabanda yao watakabidhiwa kuku hawa ili na wao kujiendeleza katika suala hili.

Kwa haya machache Mhe. Spika, niseme kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi ya kuwashukuru, tumejaribu kujitahidi kupata Wajumbe wengi wa kutosha ili kuichangia hotuba kama alivyoomba Mhe. Waziri. Lakini hata hivyo wachangiaji walikuwa ni wengi na wengine wamekosa nafasi.

Naomba radhi basi Waheshimiwa wafuatao ambao wamekosa kuchangia na wanaweza kufanya utaratibu wa kuchangia pengine kwa maandishi wakipenda. Nao ni:-

1. Mhe. Saleh Nassor Juma
2. Mhe. Ashura Sharif Ali
3. Mhe. Mohammed Haji Khalid
4. Mhe. Fatma Mbarouk Said
5. Mhe. Asaa Othman Hamad

Hapa ndio mwisho wa kuchukua michango kwa leo isipokuwa tumbekiwa na Mheshimiwa mmoja ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambaye yeye atachangia kesho mapema asubuhi kabla ya Mhe. Waziri. Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe niakhirishe kikao hiki hadi tarehe 31 Julai, 2012 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 8.56 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 31/07/2012 saa 3.00 asubuhi)